ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.

18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi zaWanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini na Tatu - Tarehe 17 Juni,2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka 2014/2015

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka 2014/2015.

HOJA ZA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kama ambavyo tulikuwa tumezungumza pale jana wakati tunaahirisha Baraza hili kuna jumla ya watu kumi ambao bado wanataka kuchangia, katika watu hawa kumi nitawateua watu wasiozidi watano au sita ili wachangie na waliobakia wachangie kwa maandishi, nitakaowapa nafasi kwa asubuhi ya leo ni. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Salma Mohammed Ali na tutaangalia baadae vipi tutaendelea.

Kabla ya hapo tutamuomba Mhe. Panya Ali Abdalla amalizie zile dakika zake tano zilizobakia baadae Mhe. Jaku Hashim Ayoub ataendelea.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana hapa leo, lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa hizi dakika, lakini Mwenyekiti umenipunja dakika zangu.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu jana nilikomea pale ambapo nilielezea elimu ya watu wazima na nikawapongeza wale wanawake waliofikia 101 kwa ajili ya kujiunga na madarasa haya na nikawasisitiza wanaume na wao waendelee kufuta ujinga kwa kujiendeleza na masomo haya, mimi nilitaka kujua katika elimu hii ya watu wazima tuna madarasa mangapi Unguja na Pemba, lakini pia nilitaka kujua wale ambao wanafikia kiwango cha ufaulu katika *level* yao huwa tunawafanyia hamasa gani labda baada ya kumaliza pale, na wao tunawatumikia vyeti angalau kuwapa hamasa na kuwafanya wengine wavutike na jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naendelea katika mchango wangu naelezea kuhusu maafisa wa elimu wa Wilaya, Mhe. Mwenyekiti, maafisa hawa zamani kulikuwa na afisa wa msingi na afisa wa sekondari, lakini sasa hivi naona amepunguzwa afisa mmoja na amebakia mmoja afisa wa elimu na maandalizi kwa kweli kazi za Wilaya si ndogo, na tukitaka tufanye kazi kufikia ufanisi basi ni bora wangelibaki vile vile wawili ili wakaweza kugawana majukumu haya na wanayafanya katika mazingira magumu kwa sababu hata vyombo wanakuwa hawana na wakiwa na vyombo basi hawana mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia maafisa hawa huwa wanakuwa katika utata kwa sababu wanapotaka maendeleo ya kujiendeleza hawajui waende wapi wanakuwa kama wako njia panda, wakija katika Wizara ya Elimu wanaambiwa nyinyi mko Tawala za Mikoa, wakija Tawala za Mikoa wanaambiwa aa nyinyi nendeni Wizarani kwenu, tungewawekea wazi hawa ili wakaweza kujijua wako wapi na haki zao wadai wapi.

Mhe. Mwenyekiti, pia maafisa hawa bado viwango vyao vya mishahara bado ni vidogo, vinalingana na walimu wakuu lakini ukizingatia majukumu yao kwa sasa yamekuwa makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu na mimi nakuja katika skuli zetu za sekondari hizi mpya, kwa kweli skuli zetu utaziona nzuri zinavutia lakini skuli hizi hazikufikia kiwango, inavyoonesha kwa kweli skuli hizi ni mbovu na ukitaka ushahidi kamili basi nakuomba ndani ya jimbo lako katika Skuli ile ya Karume basi labda utakapomaliza mchakato huu wa bajeti labda tutoke mimi na wewe mguu kwa mguu twende ili tukakague pale, lakini panaonekana pametitia na vyumba vyengine tayari vina mipasuko.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu pia nije kwenye kituo hiki cha TC Mkwajuni, kwa kweli kituo hichi ni kituo ambacho ni msaada sana kwa walimu wa Kaskazini, kwa hivyo naomba sana kituo hichi tukiingizie fedha kwa wakati ili kiweze kuwasaidia walimu na yaweze kupatikana yale malengo ambayo yamekusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika skuli za maandalizi. Skuli hizi kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Wizara haikujipanga vizuri katika kuzianzisha skuli hizi za maandalizi kuzileta katika skuli za msingi, nafasi inaonekana ni finyu sana, kwa hivyo niiombe sana Serikali ilizingatie hili na iweze kujipanga vizuri katika kuziweka skuli hizi za maandalizi katika skuli za msingi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika elimu mjumuisho. Elimu mjumuisho kwa kweli hii ni elimu ya watu wenye mahitaji maalum, lakini pia tuwaangalie walimu pia na wao ni sawa na wana mahitaji maalum vile vile, kwa sababu tunaelewa kazi ya kusomesha ni kubwa sana ukizingatia hawa ambao wao tayari tunasema wana mahitaji maalum basi bila ya shaka kuna ziada hapo ya kazi.

Kwa hivyo mimi niiombe sana Wizara iwaone walimu hawa na kuwaongezea maposho yao na wengine huwa wanabahatika kusoma na wakamaliza kozi lakini pia mnachelewa kuwaingizia fedha zao, kwa kweli walimu hawa na wao wana mazingira magumu tuchukue mfano mdogo tu tokea tumeingia hapa Barazani tunamuona kijana wetu yule ambaye anatoa lugha ya alama. Sisi tumo humu lakini hakuna hata mmoja anayeweza kusema mimi najua tafsiri pale anasema nini, kwa hivyo tuweze kuelewa kwamba walimu hawa wana mazingira magumu katika kuwafundisha watoto hawa. Kwa hivyo mimi naomba sana uwajali na tuweze na wao kuwafikiria.

Mhe. Mwenyekiti niende kwenye kitengo cha michezo, kwanza niipongeze Wizara kwa kurejesha michezo maskulini, kwa kweli hapa kutaibua vipaji vizuri kwa watoto wetu kwa sababu mtu anapofundwa jambo akiwa bado mdogo ni rahisi kufahamu vizuri, lakini tu niombe Wizara kuwa makini katika kuliingiza hili, kwa sababu lazima tuwatendee haki wale watoto ambao wanabahatika kuchaguliwa katika maskuli kuingia katika michezo ili tusije tukawanyima haki ya masomo ikawa wao wako kwenye michezo wenzao anasoma, lazima tutenge muda maalum ambao wao wanafanya michezo lakini hawaathiriki na ule muda wa masomo.

Mhe. Mwenyekiti pia nataka niombe jambo moja kilio chetu ni historia kusomeshwa maskulini, historia lazima tuirejeshe lazima watoto wetu wajue historia ili waweze kujua nchi yao waweze kujenga uzalendo katika nchi yao; hili ni jambo muhimu asiyejua historia ya nchi yake ni sawa na mtumwa, lakini niombe jambo jengine gwaride nalo naomba sana lirejeshwe kufundishwa maskulini, kwa sababu Mwenyekiti wanafunzi wanaomaliza pale wanagawika katika mafungu mbali mbali kuna wanaokwenda ualimu, lakini kuna wanaobahatika uaskari, kwa hivyo tukirejesha gwaride skuli maana yake tayari tutaandaa askari tangu pale tuko maskulini, lakini hivi sasa tunajua mtoto akimaliza skuli anatakiwa apitie JKU akipita pale hajui hata ile shoto kulia hajui, lakini tukimuandaa kutoka skuli maana yake tukitoka pale tunaweza kutoa askari wazuri ambao watakuwa hawana tabu ya mafunzo ya kufundishwa gwaride.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru lakini nitake kuzungumzia jambo moja tu dogo la kumalizia hili la ushauri nasaha, kuna mwalimu ambaye mwaka jana nilieleza kesi yake, mwalimu huyu alikwenda kusomea katika fani hii ya ushauri nasaha lakini alivyorudi aliambiwa chuo hiki hakitambuliki wala yeye hakuruhusiwa kusoma masomo hayo.

Mimi ningeomba Wizara kutokana na suala hili ambalo kutokana na Wizara zote sasa lazima kuwe na kitengo cha Ukimwi ambavyo vinatoa ushauri nasaha, si vizuri tukipata mtu ambaye amesoma atakuwa mtaalamu ataweza kuisaidia Wizara, mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hili tulijali, mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti hili tulijali na tuone kwamba litakuwa na manufaa kwetu, lakini pia mwalimu huyo aliweza kuzuiliwa mishahara yake, mimi ningependa kujua amefikiriwa vipi mishahara yake.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo nashukuru na naitakia kheria bajeti hii naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa fursa hii kuchangia Wizara ambayo ni muhimu sijui ukilinganisha Afya na elimu ipi bora, lakini ni Wizara moja nyeti kabisa, nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kwa kuweza kukamilisha kutuletea kitabu hichi na leo hii kimo ndani humu kwa kukifanyia kazi; panapo makosa tukakosoa.

Mhe. Mwenyekiti nianze na ukurasa wa 59. Kitu cha kusikitisha kuhusu mkopo wa elimu ya juu, huwezi kusonga mbele bila ya kuwa na elimu, huwezi kufanya chochote bila ya kuwa na elimu, lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya masihara au mzaha tena mkubwa sana. Serikali yoyote duniani haiwezi kupiga hatua yoyote duniani bila ya kuwepo na wataalamu mbali mbali sisi Zanzibar tunaanza kuidharau Elimu, nasema hivyo Mwenyekiti kwa sababu gani, mwaka jana tumechukua watu 1410 kuwapa mkopo, leo tunakuja kuchukua 1000 si mashara haya, hapa nataka kujua sababu gani iliyofanya Wizara kupunguza ruzuku, nataka kufahamu imepunguzwa kwa asilimia ngapi, hapa nataka kufahamu, leo ikiwa 1410 leo unachukua 1000 mwakani watoto wanaongezeka watoto wasisome ndio yale niliyosema tunafanya masihara na mzaha, serikali haijawa tayari tuangalie ukurasa wa 59 si maneno yangu yaangaliwe kwenye kitabu.

Hapa nitahitaji maelezo ya kina baada ya kwenda mbele tunarudi kwa kuwa serikali imepunguza ruzuku, masihara makubwa tunafanya hayo, hapa nahitaji maelezo ya kina kabisa kama mchezo wenyewe ndio huu hatuwezi kwenda mbele. Uamuzi huu sio wa kuwa tunarudi nyuma hatua moja haiwezekani.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hapo nije kwenye elimu Stadi na maisha ukurasa wa 71. Pamoja na nia njema ya Serikali kuanzisha elimu mjumuiko bado wanafunzi hawa wanasoma katika mazingira magumu, hasa wenye ulemavu wa macho na masikio. Wizara ililazimu itafute wataalamu wa kutosha wenye uwezo na ujuzi taaluma hii ya kutafuta watoto wenye ulemavu wa macho bado ni kitendawili kikubwa kwao, katika skuli za msingi Sekondari hadi vyuo vikuu vifaa hawana hawa watu, kwa hivyo na hapa nitahitaji maelezo vile vile.

Nikitoka hapo nije kwenye ukurasa wa 75 kuhusu ujauzito. Jumla ya kesi 12 zimeripotiwa kesi 2 za wanafunzi wenyewe kwa wenyewe, hapa dhahiri ule mmong'onyoko wa maadili tuliokuwa tukipigia kelele humu ndani unazidi kuporomoka ndio huu, na hali hii tukikaa kimya itazidi kuendelea Mhe. Mwenyekiti, leo mtoto utamkuta na simu ya laki sita ukitazama uwezo wake hamna mwanafunzi wa skuli huyo.

Kwa hivyo walimu hivi vitu wakae na waangalie au nguo wanazovaa wanafunzi sasa hivi ziangalie utakuta mtu anavaa hata mengine hayawezi kusemeka wanaita wenyewe kata buno sijui staili ile, walimu hili suala waliangalie; utamkuta mwanafunzi kauli anazozitoa huwezi kuamini, utamkuta mwanafunzi ana gari anampakia mwalimu anampa lifti patakuwa pana heshima tena hapo? Kuna siku mwanafunzi atamdharau tu mwalimu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije kunako ualimu wenye vituo. Hapa nitakuwa mkaidi sana Mhe. Waziri, walimu wenye vituo tuchukulie mfano skuli ya Muyuni anaishi mjini, nauli anayopakiwa ni shilingi 1,700/= anapewa shs. 1000/= tuna nia kweli ya kuweza kutaka kuboresha walimu hii hali hairidhishi, nauli kapangiwa mtu shilingi 1,700/= unakwenda kumpa shilingi 1000/= atakwenda kule na inafika wakati walimu wanaomba uhamisho kwa nguvu wabaki huku huku mjini, washamba hawapati kusoma. Cha kusikitisha zaidi katika hichi kitabu nilitegemea mwaka jana hapa Mhe. Naibu Waziri, alipojibu swali langu aliahidi Skuli ya Muyuni kuwa itaezekwa lakini katika katika kitabu hiki sijaiona.

Mhe. Mwenyekiti, naomba suala lenyewe nilinukuu "Serikali imekuwa ikichukua hatua na kuimarisha kiwango bora ya Elimu ikiwemo skuli zenye hadhi na ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Wilaya, Skuli ya Msingi ya Muyuni imekuwa katika kadhia ya uchakavu inasababisha watoto wasome katika unyonge mkubwa kinyume na malengo ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964".

(a) Kwa kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha inakaa pamoja na Kamati ya skuli na kulipatia ufumbuzi tatizo hilo la uchakavu wa skuli ambalo limesababisha wanafunzi kusoma katika mazingira magumu kutokana na mapaa yake kuvuja.

Mhe. Naibu Waziri nimshukuru sana na alikwenda akaliona suala hili na akaahidi katika kipindi cha maswali na majibu katika bajeti hii itakuwemo, lakini bahati mbaya sikuwahi kuona, na hili ndio lililoniajiri kuja humu ndani wananchi wa jimbo la Muyuni kwa hili nalo kidogo nitakuwa mkaidi nitahitaji maelezo. Haya maneno Mhe. Waziri kakiri humu ndani, katika bajeti hii inayokuja itafanyiwa kazi lakini bado imekuwa kitendawili.

Nije katika nyumba za walimu za Jambiani kuna walimu wanakatwa shs. 7000/= kwa mwezi kule, katika zile nyumba leo mwaka wa tatu wanakaa zile nyumba zinavuja, pana nyumba nne; moja nzuri imeezekwa na hizi nitahitaji maelezo Mhe. Waziri ikiwa mwalimu analipishwa shilingi 7000 nyumba zile zinavuja kwa miaka mitatu mpaka leo patapatikana elimu bora kweli? Hapo ni mtihani, hizi ziko Jambiani katika jimbo langu, nilikuwa nikipiga kelele kila siku kuhusu walimu wa sayansi bado mimi katika skuli yangu sijasaidiwa hata mwalimu mmoja wa sayansi, bado kitandawili kikubwa sana.

Kuna mkato wa walimu mwaka juzi wamekatwa shilingi 60000 na 70000 kuhusu vyeti vyao, wengine wameruhusiwa wengine hawakurudishiwa, nalo hili nitahitaji maelezo, hii Wizara kwa kweli sijui ni yatima au vipi katika bajeti zote zinazokuja Mhe. Mwenyekiti utafikiri tuko katika Jimbo la Kikwajuni, Uwanja wa Mao sasa hivi kuna vespa tupu huko za wafanyakazi, hazipungui 50 au 100, hii Wizara lazima ikae ifikiriwe bajeti zote humu watu wanakuja na magari hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mimi sina mchango mkubwa nitahitaji maelezo kwa sehemu nne hizo; Skuli ya Msingi ya Muyuni, nyumba ya Skuli za walimu Jambiani, nauli za walimu na shilingi 60,000. Baada ya maelezo Waziri atakapokuja kunijibu nitaunga mkono hoja hii lakini vyengine vyote sitounga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, asubuhi hii ya leo na mimi kupata fursa kusema maneno mawili katika Wizara hii muhimu; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii kumshukuru Waziri kwa uwasilishaji wake pia nimshukuru Makamo Mwenyekiti kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa uwasilishaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nianze kwa kusema kwamba bado tuna matatizo ya walimu hasa katika Wilaya yetu ya Micheweni. Na bahati mbaya mno kuna wale walimu ambao wanasaidia bado hawajaajiriwa wanakuwa wanapata kazi kubwa ya kuwasaidia watoto wetu kuwafundisha, lakini hawasaidiwi hata kidogo angalau sabuni, wanalazimika wazee wa watoto kuchangia ili kuwasaidia walimu. Na kwa kweli kila siku hapa mnazungumza kwamba Micheweni ina watu maskini sana, sasa pamoja na umaskini wao halafu tukiwalazimisha wazee kuchangia ili kuwasaidia walimu kwa ajili ya kuwa watoto wapate elimu hili ni tatizo. Kwa hivyo ninamuomba sana Mhe. Waziri aone kama wale vijana wanaosaidia walioko Micheweni ambao wameshachukua Diploma ya Ualimu au wameshasoma katika Chuo cha Ualimu basi ni bora kuwaajiri.

Halafu kuna tatizo moja huwa linajitokeza tatizo la watu kuajiriwa wakapelekwa lakini baada ya kukaa tu kama ni miezi 5, 6 au mwaka mmoja watu wale hupewa uhamisho au huchukua uhamisho wakahama wakaenda Skuli nyengine. Sasa bila ya kujua sababu za msingi ni zipi Mhe. Mwenyekiti, naomba sana, ninamuomba Mhe. Waziri suala hili basi walishughulikie kama walimu wanahama basi ni bora walimu kuajiriwa wale walio karibu na maeneo yale yale kuliko kuajiriwa watu ambao wanakuja kuchukua ajira katika maeneo halafu wanahama.
Kwa hivyo hili suala naomba Mhe. Waziri aliangalie kwa umakini mkubwa, isiwe watu wanaajiriwa wanaotoka sehemu mbali halafu wanachukua uhamisho wanahama katika maeneo yale halafu watoto vile vile wanapata tabu ya walimu.

Swali jengine naomba niungane na wenzangu, kwa sababu Zanzibar tuna matatizo ya walimu wa sayansi basi hawa wanafunzi wanaosoma sayansi wasaidiwe, wawe ni watu ambao wanasaidiwa kupewa hiyo elimu kuanzishwe madarasa maalum.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tumpe nafasi Mhe. Subeit azungumze na Mhe. Waziri aweze kusikia. Kwa hivyo mkizungumza Mhe. Waziri anapata tabu ya kusikia huku. Naomba sana tuzingatie hilo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka nimuulize Mhe. Waziri na anipe ufafanuzi kidogo ni kuhusu Skuli mpya ya Kiembesamaki. Skuli hii inachukua wanafunzi wa Chuo cha Kiislam ambao wanafunzi hawa ni wa Michepuo na wao wana vipaji maalum vya michepuo na wana vipaji maalum vya kusoma ndio maana wakapelekwa Michepuo, lakini sasa wamechukuliwa wamechanganywa pamoja na wanafunzi wa Skuli ya Kiembesamaki, hii Skuli mpya ambao ni wanafunzi wa kawaida.

Sasa naomba Mhe. Waziri anisaidie inakuwaje sasa katika masomo yao, je hatuoni kama katika makundi haya mawili moja linapata udhaifu kidogo. Aidha waliokuwa wana kipaji wakawa wanasomeshwa na watu ambao hawana kipaji au hawa ni wanafunzi wa kawaida wakasomeshwa na hawa je, huoni kama hili suala ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka nizungumze ambalo limezungumzwa sana ni suala la hawa wanafunzi wa Elimu Mjumuisho. Kipindi kilichopita nilisema sana lakini bado sijasikilikana, lakini na mara hii nasema tena. Mhe. Mwenyekiti, hawa wanafunzi ambao wanaosoma mjumuisho kwa kwetu ni matatizo kwa sababu kwanza madarasa yetu yanakuwa na watu wengi sana.

Darasa moja linakuwa na watoto zaidi ya 70, 80 kwa hivyo sasa hawa wenzetu ambao wana matatizo ni viziwi, wengine hawaoni, wengine ni mabubu sasa tunawachanganya na wanafunzi ambao wana akili timamu, wanasoma pamoja na wanafanya mitihani pamoja. Sasa hatuoni hawa niliuliza kipindi kile, je kuna kiwango maalum wanachoekewa katika mitihani yao hawa ambao wana matatizo?

Kwa sababu kama maksi zao zinazochukuliwa ni sawa sawa na wale ambao hawana matatizo tunawaonea na nilisema je, hawa wanapofanya mitihani wanaekewa kiwango maalum; yaani wanabebwa au wanawekewa kiwango gani. Lakini sikujibiwa kipindi kile basi na mara hii ninamuomba Mhe. Waziri anieleze ni lini hasa hawa wanafunzi ambao wana matatizo wataekewa madarasa yao peke yao si kuwa wanabaguliwa kwa sababu wana matatizo; hapana, kwa sababu wanabaguliwa aidha kwa kukudharauliwa au kukejeliwa hapana, wanabaguliwa kwa sababu na tunataka na wao elimu yao ipande kuliko wenzao.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ninalotaka kulizungumza ni kuhusu nyumba za walimu zilizoko Jambiani. Mhe. Waziri hizi nyumba kwa kweli ni mbovu na chakavu, na wale waliomo waliopo wanakaa kwa kukodishwa na wanalipia, lakini walimu hawa wanaambiwa zile nyumba wazitengeneze wao, wakati wanalipa. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri Wizara yako zile nyumba wazitengeneze, wao wakodi kwa kulipa lakini zile nyumba zitengenezwe ziweze kukaa watu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tano ya ziada.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, walimu kwa kweli wana kazi kubwa kumfundisha mtoto hajui kitu mpaka akaweza kujua kitu mpaka akapata cheti, akapata *degree*, akapata *master* kwa kweli ni kazi kubwa sana. Kwa hivyo walimu wana haki ya kuwa tuwaangalie na tuwaheshimu na tuwatunze, lakini walimu walio wengi wanalalamika kwa sababu wanasomesha masafa mbali pia katika masafa hayo wanaokwenda kusomesha hawapewi nauli.

Kwa hivyo ninakuomba Mhe. Waziri hawa watu waangaliwe watiliwe nauli hawa wakienda wanapata tabu sana hawa, wanaondoka wanarudi usiku, wanawakimbia watoto wao, waume zao nyumbani, lakini wakiondoka hawana nauli.

Mimi nawaona walimu wanapata tabu sana, na kama unataka uone walimu wanapata tabu sana nenda asubuhi pale Amani Tigo, pale ukawatizame walimu wanaokwenda kusomesha shamba uwatizame wanavyopata tabu Mheshimiwa. Au kama si hivyo basi wawekeeni magari maalum iwe wanapata magari hata kama watakuwa magari hayo mnawakata lakini wawe na magari maalum ya kuwapeleka katika maskuli yao wanahangaika kweli kweli. Kwa hivyo naomba sana Mheshimiwa waonewe imani, wahurumiwe, pia watiliwe posho maalum la nauli wawe hawapati tabu kuliko usumbufu kama ule wanaoupata. Mhe. Mwenyekiti tuwahurumieni walimu wetu, tuwatunzeni, tuwajalini, tuwatunze.

Mhe. Mwenyekiti suala jengine ambalo nataka nimalizie kwa kusema kama kuna kipindi Mhe. Waziri alitwambia kama kuna Skuli tumepata ambazo ni za upendeleo, na moja nikaambiwa itawekwa Micheweni, moja nikaambiwa itawekwa Unguja, ninamuomba Mheshimiwa atakapokuja kidogo atupe ufafanuzi kuhusu suala hili, kwa sababu naona siku zishakuwa nyingi hatujui hili suala kama limefifia au bado lipo? Kwa hivyo ninamuomba atakapokuja anipe ufafanuzi kuhusu suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuheshimu muda wako ninakushukuru sana.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na tukaweza kusimama hapa kuichangia bajeti hii ya Wizara ya Elimu. Pili ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni yangu machache katika Wizara hii, lakini vile vile naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa bajeti hii, na pia nitumie nafasi hii kumpa pole Naibu Waziri kwa msiba wa mama yake mzazi alioupata. Mwenyezi Mungu ampe moyo wa subira na *inshaallah* mama yetu huyu alazwe mahala pema peponi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka nianze mchango wangu kwa kusema sisi Wazanzibari kila siku tunaendelea kumshukuru muasisi wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwa jitihada kubwa na dhamira nzuri aliyokuwa nayo ya kutaka sisi Wazanzibari tupate maendeleo; ikiwemo elimu pia na maadili mema. Lakini vile vile ninamshukuru Mzee huyu kwa kuanzisha Chuo cha Kiislam Mazizini, hili ni jambo zuri Mhe. Mwenyekiti na kwa kweli sisi Wazanzibari tulitegemea Chuo kile kitazalisha watu makini ambao watatusomeshea watoto wetu kuwa katika maadili mema.

Na kwa kuwa nyoyo zina njaa na zinahitaji kushibishwa imani tulitegemea watu ambao watakuwa ni mchango mkubwa wa kuwashibisha watoto wetu imani tokea wadogo ni wanafunzi ambao wamesoma Chuo hiki na baada wakatusomeshea watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la kusikitisha serikali imeonekana kuwa na mkakati wa makusudi wa kukiua Chuo hiki, nayasema haya Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia hiki kitabu cha bajeti ukurasa wa 10, kimeeleza mradi wa ujenzi wa Vyuo vya Kiislam ikiwemo Chuo cha Kiislam Mazizini na Chuo cha Kiislam Micheweni. Hapa ilitengwa milioni 100. Milioni 100 haifanyi kitu, lakini la kusikitisha katika hiyo milioni 100 hata shilingi moja haikuingizwa. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, huu ni mkakati.

Lakini la pili, waasisi wetu walitenga eneo kwa ajili ya kuimarisha kile Chuo eneo lile Mhe. Mwenyekiti, limeuzwa na ninahakikisha ni katika mikakati ya kuua hiki Chuo cha Kiislamu, lakini jengine hata Mhe. Subeit kalisema hapa ni kuwachukua wanafunzi ambao wamepasi michepuo kuingia Chuo kile cha Mazizini wakaunganishwa na wananafunzi wa Sekondari ya Kiembesamaki.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo na ni njama makusudi za kukiua hiki Chuo. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hapo nyuma ilikuwa Chuo cha Ualimu cha Nkurumah kilikuwa kikifundisha elimu ya *Secular* na Chuo cha Kiislam Mazizini kilikuwa kikifundisha elimu ya Kiislam licha ya kuwa palikuwa pakisomeshwa masomo ya sayansi, lakini kuna masomo mengi ya kiislam ambayo yalikuwa yakifundishwa pale, ikiwemo *Fiqhi, Tauhid, Balagha, Al-adab* na masomo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, mwanafunzi akisoma pale masomo haya anajengeka imani na hata yale manun'guniko yaliyokuwepo ya kuwa maadili yetu yanapotea yangelipungua, kwa sababu wale wangetusomeshea watoto wetu. Na hasa Mhe. Mwenyekiti, ukizingatia hivi sasa watoto wetu hawana muda wa kusoma vyuo vya *qur*-an muda wote wako maskuli. Kwa hivyo wangelipatikana watu bora waliotoka Chuo kile na wakasomesha watoto wetu kuanzia *primary* basi imani ingelijengeka, na haya manung'uniko yangelipungua. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Wizara ya Elimu kubadilisha dhamira ile ambayo Mzee wetu aliikusudia kwa kweli ni jambo la kusikitisha.

Namshauri sana Mhe. Waziri alizingatie hili, kwa sababu kuna maneno siku zote humu yanatamkwa, kama kilichokufa na kuzikwa ni kiwiliwili tu cha Mzee yule lakini mawazo yake, fikra, busara zote zinazoendelea. Leo nashangaa kuwa ule ni mpango ambao aliuanzisha yeye lakini ukauliwa sasa fikra zipi ambazo zinachukuliwa za mzee huyu?

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie hapo na niingie ukurasa wa 38, ukurasa huu Mhe. Waziri amezungumza suala muhimu la teknolojia ya habari na mawasiliano TEKNOHAMA, hili ni jambo muhimu sana katika ufundishaji ikiwa kweli tunataka. Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wa Rwanda wamekuwa makini, na mpango huu wa TEKNOHAMA, na kwa kweli hivi sasa hali yao iko vizuri, lakini taarifa niliyonayo kila mtoto anayo kompyuta aliyopewa na serikali, lakini sisi hapa tunapoanza hata walimu hawajui hata kufungua hiyo kompyuta, kwa kweli TEKNOHAMA kwa Zanzibar itakuwa na safari kubwa kufikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, labda nimuulize Mhe. Waziri Wizara yake ina mpango gani iliouweka labda ikifika mwaka fulani itakuwa wanafunzi wa Zanzibar na wao wameshapatiwa kompyuta. Ninamuomba Mhe. Waziri akisimama anieleze

ana mpango gani, pengine tayari washakuwa na mpango ikifika mwaka fulani itakuwa na sisi tayari tushafikia suala hili.
Mhe. Mwenyekiti, hili tusishangae kwa sababu wenzetu wa Rwanda wameweza na hawana rasilimali kubwa labda utalii wa kuangalia wanyama sokwe. Sisi Zanzibar tunashindwa nini? Ninamuomba Mhe. Waziri atakaposimama atueleze ana mpango gani wa kuhakikisha wanafunzi kila mmoja anapata kompyuta yake.

Suala jengine ambalo ninaomba Mhe. Mwenyekiti nilizungumzie ni suala la malipo ya wafanyakazi wenye uzoefu.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano ya ziada.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi ninaipongeza sana Serikali kwa kuwaona wafanyakazi wenye uzoefu na wakaamua kuinua maslahi ya watumishi wake, lakini Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu malipo haya hayako wazi na nina wasiwasi kama walimu hawa wanataka kudhulumiwa. Kwa nini kusiwe na uwazi au kwa nini walimu hawa wenye uzoefu hawapewi maelezo mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini hiki kitengo cha Uhasibu hakiwalipi walimu eti mpaka waandike barua na wakati Wizara nyengine hawafanyi hivyo. Ninahakikisha Mhe. Mwenyekiti, huku ni kuwafanya wachoke, kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri atakaposimama anieleze ni utaratibu upi unaotumika kuwapa maslahi walimu wasio na ma-*degree* na ma-*diploma* lakini wana uzoefu. Ninamuomba Mhe. Waziri atakaposimama anifahamishe utaratibu huo.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 93 kuna jadweli linaloeleza wanafunzi waliofaulu. Mhe. Mwenyekiti, katika jadweli hili kuna kiwango cha kufaulu cha *Division Four* ambayo ni wengi sana kila mwaka, na hawa ni wale ambao wanapata "D" ya Dini na ya Kiarabu, hivi Mhe. Waziri aniambie itawachukuaje watu hawa kama wamefaulu wakati hakuna Chuo wanachoruhusiwa kuendelea. Kwa nini Wizara inaona tabu kusema kama watu hawa wamefeli, huku si kujifurahisha kusema watu wamefaulu lakini hawawezi kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri asijifurahishe akatufurahisha na sisi, mtu aliyefaulu ni yule anayepata kuendelea, lakini ikiwa mtu hapati kuendelea na masomo huyo hakufaulu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo namalizia ni kuhusu somo la ujasiriamali katika maskuli. Kama ilivyozunguzwa kwenye aya ya 65 ya kitabu cha Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, hii ni lazima Wizara ya Elimu ibadilike katika mitaala yake, haiwezekani nchi haina ajira, ajira ni kidogo lakini ikawa Wizara ya Elimu haijipangi kusomesha vizuri na kupanga mpango hasa wa ujasiriamali ili wanafunzi watakapomaliza kusoma waweze kujiajiri. Mhe. Mwenyekiti, hatupaswi kuandaa wanafunzi kuwa makarani tu kwani hazipo. Kwa hiyo, Mhe. Waziri namshauri sana aliangalie hili.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda haupo kuna suala moja la uhamisho wa walimu. Mhe. Mwenyekiti, tunajua kama wafanyakazi wa serikali wanatakiwa wahamishwe wasiachwe pahala pamoja, na hii ni nzuri lakini kuna hawa Walimu Wakuu mara nyingi huwa wana mipango ambayo tayari wameshaipanga kwa mwaka. Mhe. Mwenyekiti, kumchukua Mwalimu Mkuu ukamuhamisha kati kati ya mwaka ni kumpotezea malengo, kule anakokwenda aende akajipange tena. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Elimu iliangalie hili ikitaka kuwahamisha walimu watizame ule muda wa kuwahamisha. Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia…

Mhe. Mwenyekiti: Muda wako umekwisha.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa muda wako huu wa dakika 15 nikatoa mchango wangu mdogo katika wizara hii muhimu, Wizara ya Elimu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kuwapongeza wizara pamoja na walimu. Mhe. Mwenyekiti, walimu wetu kama wenzangu waliotangulia kusema kwamba wanafanya kazi kubwa ya kuwasomesha watoto wetu, na wanafanya kazi katika mazingira magumu na maslahi yao ni madogo.

Jambo hili Mhe. Mwenyekiti, serikali inajitahidi kuangalia kwa makini na kwa sababu pale ndipo tunapozalisha, kile ndio kiwanda cha kuzalisha, maendeleo yanazalishwa pale. Sasa kama tutakuwa tunazalisha teknolojia mbovu hatimaye na sisi tutakwenda katika mambo mabovu mabovu huko tunakokwenda.

Kwa hivyo, serikali iangalie sana maslahi ya walimu pamoja na kwamba wanafanya kazi katika mazingira magumu, madarasa wanayosomesha ukienda darasa limesheheni watoto 100 au 120 wako mule tena wako chini, vifaa vya kufanyia kazi hakuna, majengo mabovu yameshachoka hayafanyiwi *repair*, kweli walimu wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu kweli kweli.

Kwa hivyo, mimi niwapongeze kwa juhudi zao wanazozichukua, pamoja na kufanya kazi katika mazingira magumu lakini wameweza kufanya shughuli na wameweza kupasisha katika viwango hivi ambavyo Mhe. Waziri ametueleza, lakini ni lazima hili Mhe. Waziri ulisemee, kuwatetea walimu wako ni jambo zuri na linastahiki, kwa sababu wanafanya kazi vizuri, na mazingira haya basi nayo tuyaboreshe ili tuone kwamba walimu wanakuwa wana masononeko haya ya walimu yanaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, na hili jengine ambalo Mhe. Salma hapa amelizungumza juu ya wale walimu wazoefu ambao wako wanasomesha wengine miaka 30, 40 lakini unakuta mishahara yao ni midogo ukilinganisha na wale walimu ambao wameanza kusomesha leo au wanafanana.

Jambo hili tumekuwa tukilisema sana kwamba uzoefu nao una-*matter*, kuna walimu wanasomesha miaka mingi lakini mishahara yao wameshindwa na wale walimu walioajiriwa leo. Hili hata serikali imesema italifanyia kazi lakini imekuwa maneno tu.

Mhe. Mwenyekiti, tuangalie si walimu karibu wafanyakazi wote wapo ambao wameshafanya kazi muda mkubwa lakini wajukuu zao ambao wanaanza leo basi wanawashinda mishahara. Kwa hivyo, hawa na wao maslahi yao yanatakiwa yaangaliwe angalau na wao waweze kufanya kazi kwa furaha kuliko ilivyo hivi sasa.

Kwa hivyo, mimi nitumie nafasi hii kuwapongeza walimu, na tuwaombe kwamba wasichoke wafanye juhudi zaidi na wasivunjike moyo, na naiomba serikali iangalie zaidi maslahi yao ili kutusomeshea watoto wetu hawa na tupate *product* iliyokuwa nzuri na inayoendana na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo katika suala la utaratibu ambao wizara inautumia sasa hivi, mimi sielewi wanatumia utaratibu gani lakini nilichokiona kwamba sehemu kubwa ya fedha za serikali zinakwenda kwa nauli za walimu.

Kwa mfano, mwaka huu wametumia karibu 1.2 bilioni kwa ajili ya nauli za walimu kwenda huku na huku. Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia nchi masikini kama yetu kiwango kama hiki cha posho ya safari ya walimu kwa kweli ni kiwango kikubwa. Pesa hizi pengine zingeweza kufanya shughuli nyengine, lakini tunatenga fedha kiwango kikubwa kwa ajili ya posho ya nauli ya walimu ni haki yao kupewa, lakini je, wizara au serikali ina mpango gani wa kurekebisha hili.

Mimi naamini kama mtajipanga vizuri linawezekana, na kwa sababu pamoja na posho ya walimu ya nauli ambayo wanapewa kwenda huku na huku lakini pia walimu kutoka sehemu kwenda sehemu nalo linachangia kudumaza masuala ya elimu.

Kwa mfano, mwalimu anatokea Mjini anakwenda kusomesha Nungwi, asubuhi anatoka hapa anahangaika na usafiri akifika pale Nungwi atatafuta utaratibu wa kurudi Mjini sasa. Kwa hiyo, tusitegemee kwamba hapo elimu itakuwa hii ukiangalia karibu Unguja nzima.

Kwa hivyo, mbali ya posho ya walimu ambao wanakwenda huku na huku lakini hata ule usomeshaji wao utakuwa haulingani na ile hali halisi. Haiwezekani mwalimu akae Mjini akasomeshe Matemwe au akae Mjini akasomeshe Muyuni, hayo ni masafa makubwa, muda wake mwingi anautumia kwa kwenda huku na huku.

Kwa hivyo, hili Mhe. Waziri lazima uliangalie kwa pande zote mbili, kwanza kama utakuwa na utaratibu mzuri wa walimu wako kuwapanga walimu gani wawepo wapi ili kupunguza posho ya walimu ya nauli na kupunguza kupata muda wa kushughulikia masuala ya elimu, badala ya kwamba muda wake mwingi anautumia kwa safari za kwenda na kurudi. Kwa hivyo, haya maeneo mawili Mhe. Waziri unatakiwa ukae na ujipange namna gani uta-*solve* hili.

Eneo jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo hili nitalizungumza kwa hisia kubwa kidogo, suala la miradi hii ambayo inafadhiliwa na wenzetu Benki ya Dunia pamoja na *BADEA* na mabenki mengine juu ya miradi hii ya ujenzi wa majengo mapya ya skuli.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu hawa kwa upande mwengine tunasema ni wafadhili, lakini kwa upande mwengine wanatukopesha. Kwa sababu ukisikia benki maana yake inakopesha na unapokopeshwa maana yake pesa hizo zinahitaji kulipwa na walipaji ni wananchi, kwani ni madeni ya nchi, lakini nadhani wenzetu wanafika pahala wanakuwa na hisia kwamba pesa zinazotolewa na mabenki maana yake kama vile ni sadaka, lakini kumbe ni kodi ambayo baadae itakuja kulipwa na wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ujenzi wa majengo haya linasikitisha, bahati nzuri serikali yetu imepata miradi mikubwa sana ya ujenzi wa majengo haya ya ghorofa katika maeneo mbali mbali, lakini la kusikitisha majengo yanayojengwa hayana viwango, fedha zinatoka nyingi majengo hayana viwango, majengo baada ya muda mfupi yameharibika, *tiles* zinatoka, kuta zinapasuka, yanavuja wakati pesa zilizotumika ni kiwango kikubwa.

Kwa kweli hii haipendezi, na haiwezekani jengo linajengwa leo baada ya miaka miwili jengo lile lote limeharibika. Hili Mhe. Mwenyekiti, mimi nimekuwa na mashaka juu ya usimamizi wa mambo haya. Na kwa kuwa hatujawa na utamaduni, maana Baraza letu lishakuwa halina utamaduni wa kuchunguza jambo, hatutaki kuchunguza jambo hata jambo lenye mashaka.

Hili linahitaji kuchunguzwa na tujue kuna nini, kwa nini majengo haya ambayo yamejengwa pamoja na kwamba ni mikopo ya benki zetu, lakini ni fedha ambazo tumekopeshwa hatukugaiwa majengo yale yanayojengwa katika maskuli mbali mbali ambayo yamejengwa kwa gharama kubwa, kwa nini baada ya muda mfupi majengo yote yanaharibika.

Kwa vyovyote hapa inaonekana lipo jambo, haiwezekani. Sisi tunawajua wenzetu hawa wa China ni wajenzi wazuri sana, na majengo yao tumeyaona, China tunakwenda na kurudi kila wakati wanajenga majengo yaliyokuwa na *quality*, yenye viwango, na utashangaa kwa nini leo Machina wale wale wanaokuja kutujengea majengo hapa baada ya miaka miwili majengo yote tunaanza kufanya *repair* kwa pesa nyingi tu. Kwa nini inakuwa hivyo Mhe. Waziri? Majengo ambayo tungetegemea labda baada ya miezi kumi tuanze kuyafanyia *repair*, lakini majengo sasa hivi limejengwa jengo lina *consultant* lina kila kitu, baada ya siku mbili linavuja. Kwa nini na mafundi ndio hawa hawa?

Mhe. Mwenyekiti, kamati inayosimamia sekta hii mimi siwezi kusema kwamba labda tuunde kamati ikaangalie tatizo, lakini kamati inayosimamia sekta ya elimu lazima ilichunguze hili, tusiende tu kule kamati, Waheshimiwa Wawakilishi tuwe makini katika hili kwani majengo yale ni mabovu, mengine yanakwenda yanafunguliwa majengo ni mabovu, *tiles* zote zimeng'oka.

Hebu nendeni kule kwenye maskuli mukayaangalie, zile ni kodi za wananchi, haiwezekani jengo limejengwa leo baada ya mwaka mmoja au miaka miwili linahitaji *repair* pesa nyingi zaidi ya zile, hapa pana tatizo. Mhe. Mwenyekiti, nakwambia hapa pana tatizo na likichunguzwa litaonekana, sisi Wachina tunawajua sana. Sisi taarifa tuliyokuwa nayo Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba fedha zile ambazo wanapewa Machina kwa ajili ya ujenzi hazifiki zote, kuna sehemu ya fedha zinachukuliwa na wafanyakazi wa Wizara ya Elimu.

Mhe. Mwenyekiti, siku hizi Machina wanakwenda na wakati, zamani Mchina huwezi kumuendea kwa utaratibu huo, lakini siku hizi wanaenda na dunia, ukimwambia bwana pesa hizi za ujenzi huu chukua hiki, hiki ninazuia anakubali, lakini ukimzunguka ukimuuliza kwa nini inakuwa hivi, anasema pesa mumechukua wenyewe. Sisi tutajenga kwa kiwango kile cha fedha ambazo tumepewa, badala ya kuweka mifuko ya saruji 100 inawekwa 50 baada ya siku mbili tatu jengo limekufa. Ndio utaratibu tunaokwenda nao, hii nchi hii itafika wapi? Kwa utaratibu huu Mheshimiwa hatuwezi kwenda hata siku moja, na nchi hii haiwezi kupata maendeleo, kwamba tukiwa hatuna fedha matatizo, tukipewa fedha matatizo.

Leo majengo tunakuwa tunayafanyia matengenezo kila siku, jengo limejengwa juzi baada ya siku mbili unalikuta lote bovu, tutafika wapi, maendeleo yatapatikana wapi?

Kwa hivyo, Mhe. Waziri hili ulisimamie, kwa kweli hili ulisimamie na kamati ya sekta inayosimamia Wizara ya Elimu isimamie, na kama ingekuwa hatuna utaratibu wa kuunda kamati kwenda kuchunguza ningeliomba Baraza lako liunde kamati, lakini tukisema hapa mtakataa, kwa sababu wajibu wetu hatuujui, lakini kama tungekuwa tunajua wajibu wetu wa kuisimamia serikali hili tusingelikataa hata siku moja, kwa sababu huu ni udhaifu mkubwa sana katika nchi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, suala la kumalizia majengo ya skuli, Mhe. Waziri anakumbuka mwaka jana hapa aliniahidi kwamba atanimalizia jengo langu la skuli…

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naona mnatoka sana nje, tunaelekea ukingoni, wale waliokuweko nje naomba warudi ndani sasa. Mheshimiwa tuendelee umebakiwa na dakika nne.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aliniahidi kunimalizia jengo langu la skuli na nilieleza *concern* yangu na umuhimu wa kumaliziwa jengo lile, na akaniahidi na nilimualika akaja akaniwekea jiwe la msingi na akawaahidi wazee wa pale kwamba atalimalizia katika bajeti ile, lakini la kusikitisha sana Mheshimiwa pamoja na kufuatilia nilikuwa nikimfuatilia sana Mhe. Naibu Waziri kwa nini mwaka unamalizika hili jengo halijamalizwa, na mpaka leo halijamaliziwa na halikumalizwa pengine wenzetu wana ukosefu wa fedha, mimi sijui lakini ni ahadi ambayo imetolewa.

Kilichonisikitisha zaidi Mhe. Mwenyekiti, mbali ya kwamba lile jengo halijamaliziwa mbali na umuhimu wake, nimeangalia kitabu chake Mhe. Waziri hata katika ile orodha ya majengo ambayo yamewekwa kwa ajili ya kuezekwa hamna katika Wilaya ya Mjini.

Sasa hili limenitia mashaka, kwa sababu mwaka jana aliniahidi ataliezeka bahati mbaya limemshinda, basi hata orodha ya mabanda ambayo yapo katika Wilaya ya Mjini ambayo yanahitaji kuezekwa pia hamna kuna sifuri.

Kwa hivyo, nimeingiwa na mashaka, nataka Mhe. Waziri aje aniambie mbona hata orodha haimo mbali, na kwamba hakuwahi kunijengea mwaka jana pengine kutokana na ukosefu wa fedha lakini hata kwenye orodha basi majengo au mabanda ambayo yanasubiri kuezekwa pia katika orodha hayapo. Kwa kweli hii haipendezi hata kidogo, na imenitia mashaka. Kwa hivyo, Mhe. Waziri aje aniambie tena ahadi nyengine ya mwaka mwengine.

Je, katika mabanda yale najua kuna mabanda ambayo yamemalizika muda mkubwa, lakini kutokana na umuhimu Wilaya ya Mjini sasa hivi kuna jengo moja Wilaya nzima, hivi tunashindwa hili kulimalizia watoto wale wakapata nafasi ya kusoma, watoto wanasoma madarasani watoto 100, 120 lile Mhe. Waziri ukilimalizia angalau ile idadi katika madarasa itapungua na wale watoto watapata nafasi ya kusoma vizuri.

Kwa hivyo, nakuomba sana mwaka huu wa fedha pamoja na kwamba hukuweka hata kwenye madarasa ambayo yanasubiri kuezekwa katika Sekondari ya Nyerere hili nalo linahitaji limaliziwe ili watoto wetu waweze kusoma vizuri.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamelizungumzia sana suala la historia ya Zanzibar. Suala la historia ya Zanzibar ni muhimu, sisi sote humu tumesoma historia ya Zanzibar tulikuwa tunasoma, haidhuru sasa hivi historia ipo lakini siyo ile historia halisi.

Mhe. Mwenyekiti, watoto wetu hawajui historia ya Zanzibar na ndio maana unawakuta wanakwenda tu hawajui wanatoka wapi, tuko wapi, tunakwenda wapi.

Ni lazima suala la historia ya Zanzibar kama tulivyosoma sisi tunajua historia yetu ikoje, tunajua serikali hii ilikuwa inatawaliwa na Wakoloni, hivyo watoto wetu lazima wajue.

Leo mtoto ukimwambia kwamba nchi hii ilikuwa inatawaliwa na Sultani hajui, anakwambia aah hizo ni blaa blaa zenu wanasiasa, lakini kumbe nchi hii ilikuwa inatawaliwa zaidi ya miaka 300 watoto wetu wanatakiwa wajue, wajue nchi hii imefanya Mapinduzi mwaka 1964, Mzee Karume ndiye aliyeongoza Mapinduzi lazima wajue historia ya nchi yao, mtu yeyote asiyejua historia ya nchi yake ni mtumwa. Kwa nini somo hili la historia limeondoshwa na sasa hivi limetuletea athari kwa vizazi vyetu.

Jambo hili Mhe. Mwenyekiti, ni hatari Mhe. Waziri aje atwambie hapa ni lini wizara yake itarejesha somo la historia kama tulivyosoma sisi historia, ili watoto wetu wanaoanza chini wajue nchi yao inatoka wapi, iko wapi na inakwenda wapi, hapo ndio watakapokuwa na uchungu wa nchi yao, *otherwise* tutakapokwenda vyenginevyo vyovyote watakuwa hawana wanalolijua, kila kitu wanaona kiko hivi hivi kilivyo.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri uje utwambie ni lini Wizara ya Elimu itarejesha hili somo la historia, na siyo historia hii tunayoizungumza hivi sasa, hivi tunasoma mambo sijui ya nje lazima wajue historia ya nchi yao vijana wetu.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa muda wako mimi naiunga mkono hotuba hii na Mhe. Waziri atapata nafasi ya kuja kutoa ufafanuzi juu ya yale ambayo yote nimeyazungumza na hususan juu ya majengo haya mapya ambayo ni mabovu yanajengwa baada ya siku mbili, ma-*tiles* yanang'oka, yanavuja, yanahitaji tena ukarabati.

Serikali inahitaji tena kutumia pesa nyengine kwa ajili ya kufanyia ukarabati, na huku mikopo yenyewe ambayo tumekopa katika mabenki hatujaanza kuilipa ambayo ni mzigo mkubwa sana kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, hili linasikitisha sana. Ahsante nakushukuru sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia chochote katika bajeti hii ya mwaka 2014/2015 ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Moja kwa moja kwa kuanza Mheshimiwa naomba nianze na mradi wa uimarishaji wa elimu ya ufundi ni ukurasa wa 14 wa kitabu hiki na ni kifungu cha 20.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hiki Mhe. Waziri ameeleza kuwa mradi huu umetengewa jumla ya milioni mia tano (500,000,000) na unakusudia au ulilenga kufanya mambo yafuatayo:-

Moja ni kuanza ujenzi wa dakhalia mpya ya Skuli ya Sekondari ya Ufundi ya Kengeja. Vile vile kuipatia Skuli ya Sekondari ya Ufundi ya Kengeja vifaa vya karakana na kuendelea na ukarabati wa majengo, kununua vifaa vya kufundishia na vitabu kwa ajili ya taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia.

Mhe. Mwenyekiti, vyuo hivi viwili yaani Skuli ya Sekondari ya Ufundi ya Kengeja na Chuo cha Ufundi cha Karume cha Sayansi na Teknolojia ni skuli pekee zinazotoa mafunzo ambayo wanafunzi wanapomaliza mafunzo hayo kama hawakupata ajira katika serikali wanaweza kujitegemea.

Naamini serikali iliweka fedha hizi kwa madhumuni ya kuleta maendeleo kwa wanafunzi wa skuli zetu hizi mbili, lakini la kusikitisha mpaka kufika siku 18 zilizopita yaani tarehe 30 Mei, 2014 hakuna fedha zilizopatikana, na hivyo hakuna utekelezaji uliofanyika. Hili linasikitisha kweli kweli, na kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri anayehusika na utoaji wa hizi fedha atueleze ni sababu gani zilizomfanya mpaka hata angalau asilimia 50 ya fedha kuingizwa zile skuli zikatekeleza mambo yake yaliyokusudiwa, vyenginevyo nitaona serikali inasikitisha kuwa vyuo kama hivi muhimu kutovipa uzito wa juu.

Jengine nizungumze Idara ya Elimu ya Serikali ambayo iko katika kifungu cha 63 ukurasa wa 34. Idara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilikusudia kutoa mafunzo kwa walimu wapya na wasaidizi wao watakaoajiriwa. Vile vile kutoa mafunzo ya uongozi kwa Walimu Wakuu wapya na wasaidizi wao na kutoa mafunzo kwa walimu wa *panel* za masomo ya Kiingereza, Hisabati na Sayansi. Sio hivyo tu, imekusudia pia kutoa taaluma kwa walimu wa masomo ya sayansi kuhusu utumiaji na utunzaji wa vifaa vya maabara.

Mhe. Mwenyekiti, mafunzo kwa walimu ni jambo la lazima na naipongeza wizara kwa kuweka malengo hayo. Walimu wetu tunajua wanakabidhiwa watoto kutoka sehemu mbali mbali, wenye hulka, silka na tabia mbali mbali na wanataka kuendelezwa na kutumishwa katika itikadi ambayo wataweza kuyamudu masomo yao. Sasa kama walimu hawakuwa na mafunzo ya kutosha na wakajua nini wafanye kwa maslahi ya mtoto, ambapo walimu hao wanalipwa kwa makusudi kwa kuwaendeleza watoto hawa, kwa bahati mbaya huwa wanajisahau na huwa wanafanya mambo kinyume na utaratibu ambao unasababisha lile lengo la kumpatia elimu mtoto likakosekana.

Mhe. Mwenyekiti, sipendi kutaja skuli wala kumtaja mwalimu, lakini nimeshuhudia na mwalimu mwenyewe aliona labda hivi ndio sawa anavyofanya katika adhabu anazotoa, ama kumtoa mwanafunzi nje na mpaka kumtemea mate. Hii ni kwa sababu hawa walimu wanaona wanavyofanya ni sawa lakini pia ni kwa sababu ya kutopata mafunzo.

Kwa hivyo, naomba wizara ihakikishe kuwa hili lengo walililoliweka la mafunzo kwa walimu, mafunzo wakuu na wasaidizi wao na mafunzo kwa taaluma ya walimu wanaotumia vitu vya sayansi lipewe kipaumbele.

Vile vile nilitaka kujua huyu mwalimu anasomesha sayansi na yeye mwenyewe kasoma sayansi na halafu katumia vifaa vya sayansi, leo itakuwaje apewe mafunzo katika kusomesha masomo haya ya sayansi. Nafikiri mimi kama kuna kitu hicho basi inaonesha katika skuli zetu kuna walimu wamepewa masomo wafundishe na hawawezi kutumia zana za sayansi.

Jengine ukitizama kifungu cha 64 ukurasa huu huu wa 34 Mhe. Waziri ameeleza kuwa katika mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Sekondari itakusudia kuendelea kufuatilia shughuli za ufundishaji katika skuli na kuzipatia skuli vifaa mbali mbali vya kufundishia. Hilo ni jambo zuri, lakini pia itanunua vifaa vya maabara kwa ajili ya mazoezi katika masomo ya sayansi kwa skuli 100 za Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tukiangalia vifaa vya maabara ni vifaa ghali sana, skuli 100 za Unguja na Pemba ni nyingi sana. Mimi nataka nielewe Mhe. Waziri kajipanga vipi kupata pesa zote hizo za kuweza kununulia vifaa vya sayansi kwa skuli 100. Hilo ni moja.

Pili, kwa ninavyofahamu tunazo skuli nyingi tu za sekondari lakini hazina maabara, sasa vifaa hivyo vitawekwa wapi. Hilo ni la pili.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie basi kifungu cha 109 kwa sababu ya wakati kilioko katika ukurasa wa 48 na hii nakusudia ni Taasisi ya Elimu Zanzibar ambayo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 imejipangia kuendesha mambo yafuatayo:-

Kwanza, kuendesha mafunzo kwa walimu wa sekondari wa sayansi na namna ya kutumia vifaa katika kufundishia masomo hayo. Halafu itafuatilia na kusimamia matumizi ya vifaa katika ufundishaji na uendeshaji wa maabara katika skuli za sekondari na kufanya utafiti juu ya sababu za matokeo mabaya ya mitihani kwa masomo ya sayansi na hisabati kwa skuli za sekondari.

Mimi kwa sababu ya wakati nimalize kwa kuchangia kwamba, kuhusu kufeli watoto kwa hisabati na sayansi si suala la kufanyiwa utafiti. Hili suala liko wazi ni ukosefu wa walimu bora, ukosefu wa vifaa vya kufundishia na vile vile ni ukosefu wa mahala pa kuwekea vifaa hivyo vya kufundishia.

Kwa hivyo, kama wizara inakusudia kuwa wanafunzi wetu wapasi sayansi ni lazima itayarishe kwa namna ambayo vifaa vitakuwa vya kutosha, mahala pa kuviweka patakuwepo na walimu wenye uwezo wa kufundishia watakuwepo, vyenginevyo siku zote tutakuwa tunafanya mambo tu ya maneno lakini utekelezaji hakuna.

Mwisho ili tuendelee naomba sana kwa Mhe. Waziri walimu wetu wanafanya kazi kubwa sana, walimu wetu hawalali usiku na mchana, walimu wetu wana kazi kubwa ya kutoa taaluma kwa wanafunzi, lakini kwa ujumla mafao yao ni madogo sana. Naomba Mhe. Waziri ajitahidi kuangalia uwezekano wa kuwaongezea maslahi.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa nilitaka kujua kuhusu wanafunzi waliomaliza ualimu cheti mpaka leo wapo chungu nzima hawajaajiriwa. Je, serikali ina mpango gani? Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujamkaribisha Mhe. Waziri kwa ajili ya kuanza kutoa majibu na kufanya majumuisho tuna wageni kwa siku ya leo ambapo wageni wetu ni wanafunzi kutoka Skuli ya Sekondari ya Ben-bella, jumla yao ni wanafunzi 48 wakiwa pamoja na walimu wao wanne naomba wasimame ili waonekane. Ahsanteni. *(Makofi)*

Wale Wajumbe ambao hawamo humu ndani Mhe. Waziri atakapojibu masuala yao kwa maana ya kutoa majibu na endapo kama Mjumbe jawabu limetolewa hayupo, hatutoruhusu kupiga buti katika utaratibu kama huo. Ahsante Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ingawa ya haraka haraka bila ya matayarisho, lakini nitajitahidi kujibu yale nitakayoweza kujibu au kuyajibu yote na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atanisaidia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama hapa leo kutoa michango yangu. Mwenyekiti sijui kama nitapata nafasi ya kutoa majibu kama upigaji wa meza wenyewe namna hii, lakini nawaomba wanaogonga meza wagonge kwa pole pole ili wanipe nafasi nitoe hayo majibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri hao watu wamefurahika kuona kuna meza na viti vimekuja hapa juu, ndio maana wamefurahi, lakini Mhe. Waziri tuendelee.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo, afya njema na nguvu ya kuweza kusimama hapa na kujibu haya masuala.

Pili kama walivyotangulia wenzangu na mimi nampa pole sana Mhe. Naibu Waziri wangu, nampa pole kwa kufiliwa na mama yake, mama yake mpenzi tumeshamzika *Alhamdulillahi.* Mhe. Naibu Waziri alifanya safari ya Pemba kwenda kusoma hitma na siku ya kwanza tulipozungumza nilimsikia sauti yake nzuri kuwa kwamba ameanza kusahau, ameanza kuvumilia na amerudi katika hali ya kawaida.

Lakini kuanzia jana hali yake ni mbaya sana, hivi sasa yuko kwenye *drip* ana hamu ya kuja kunisaidia kujibu maswali lakini hawezi na nimemzuia. Kwa hivyo, tuendelee kumuombea Mwenyezi Mungu ampe maisha mazuri amrejeshe katika hali yake ya kawaida ili tuje tusaidiane katika kuendesha gurudumu hili.

La pili, namshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa michango yake aliyoitoa na ni mizuri kama kawaida ya Kamati hii inanishauri vizuri, nimepokea ushauri wake wote, na pale alipotoa michango yake ya kibinafsi amechangia mambo mazuri, ameelezea masuala ya kusamehewa skuli zetu matumizi ya nishati kama ni mchango wa kitabu hiki. Na wakaniomba nimuombe Waziri amwambie Mkurugenzi wa Nishati ili achukue hatua hii. Kuomba siku zote ni kitu kimoja lakini kupata unachoomba ni kitu cha pili.

Mimi Mhe. Waziri amenisikia na naendelea kumuomba ingawa idara hii inasema inaendesha kazi zake kitaalamu, kibiashara, wanasema wao wanadaiwa na *TANESCO* nakubali yote waliyoyasema, lakini naomba kilio changu kisikike, skuli zangu zote na hasa hizi 13 mpya tulizozijenga matumizi ya umeme ni lazima, lakini matumizi yanakuwa makubwa kila leo na umeme unakatwa mara kwa mara.

Namuunga mkono Mhe. Mohammed Mbwana Hamad walivyozungumza na wengine wengi wamezungumza suala hili namuomba Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati awe na moyo wa huruma, akisikie kilio chetu, kama hakutuondoshea kabisa basi atupunguzie kwa kiwango ambacho yeye mwenyewe anakijua. Mhe. Mwenyekiti naomba kusema hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Asha Bakari Makame kwa michango yake aliyochangia, kura zake alizotupa, pongezi ametupa ahsante sana alimradi jambo alilosisitiza ni kwamba historia tuirejeshe na tuirejeshe vile ilivyokuwa ikisomeshwa.

Namuunga mkono na namwambia kwamba somo la historia tumelirejesha miaka mitatu iliyopita na tunasomesha historia ya Mapinduzi, tunasomesha historia ya utawala wa nyuma wa kikoloni na hali halisi ilivyo hivi sasa.Tunajitahidi lakini tunamshukuru kutukumbusha na tutaendelea kufanya hivyo kila leo ili wanafunzi wetu wasisahau kwao walikotoka, walipo na wanakoelekea. Kauli hii ya historia imezungumzwa na Wajumbe wengi sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mussa Ali Hassan alizungumza suala hili, Mhe. Saleh Nassor Juma mkereketwa alizungumza suala hili na wote hao kwa pamoja nawaambia kwamba nimepokea mawazo yao, na tutarejesha au tumerejesha na tutaendelea kutia mkazo katika masuala hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mchangiaji wa pili aliyezungumza kwa bahati mbaya hapa hayupo, aah yupo ndugu Mohammedraza Hassanali Mohammedali.

Mheshimiwa alizungumza maelezo makubwa sana, kwa ukali mkubwa sana na hata akatishia bajeti hii isikubaliwe, isipitishwe, akataka tuunde ile tume Kamati ya Mkakati sijui kamati gani ile ili ichunguze suala hili kwa sababu alisema hapa pana rushwa. Hili nasema kwa unyenyekevu na upole mkubwa sana, mimi nakataa yale yote aliyoyasema, na nina ushahidi kamili. Lakini sikatai kwa ajili ya kushindana naye, hapana. Sikujenga tabia hiyo na hiyo sio tabia yangu, nimeachana kabisa na tabia hizo. Nakataa kufuta hilo kosa lililotiwa.

Lakini nasema mchango wa Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali uliungwa mkono kidogo na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, na Mheshimiwa wangu mkereketwa Mhe. Hamad Masoud Hamad aliunga mkono akasema kwamba hizi pesa tumezipata wapi, na akataka auone mkataba tuliotiliana naye huyu mtu wa Dar es Salaam aliyechonga hivi viti na meza.

Namshukuru sana Mheshimiwa mkereketwa hakuzungumza suala la kuzuia bajeti yangu, wala suala la kukataa vifungu, lakini alitaka kitu hichi akione.

Mhe. Mwenyekiti, nikijibu suala hili namjibu Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Hamad Masoud Hamad. Nasema hivi, hizi pesa ni za mradi wa *BADEA* wa kujenga chuo cha SUZA. Na kwa ufupi tulitoa tenda ya kuagizia au kununua hivi vifaa, ili atakayeshinda aje atufanyie kazi hii ya kututilia sio tu kununua viti, meza na vikalio hapana, kututilia vitu vyote vya chuo cha SUZA.

Kuna mchangiaji mmoja alizungumza jana kwamba kuanzisha chuo kikuu si kazi rahisi, ni kazi kubwa, ina hasara nyingi na gharama nyingi. Mimi nilimuunga mkono huyu. Chuo cha SUZA tulichokifungua mwaka mmoja uliopita kwa sababu ya kukamilisha vitu tulivyovitaka kwa kutoa tenda. Tukatoa tena, Mhe. Saleh Nassor Juma rafiki yangu. Wakamaliza kazi hii tukahamia na kazi yenyewe ni kazi ya kutia viti, meza chuo kizima, ofisi zote. Kutia viyoyozi chuo kizima. Kufanya shughuli zote za chuo hiki mpaka kikamalizika kikakamilika. Mambo ya umeme na kadhalika.

Tukasema tunatoa tenda ili atakayetafuta tenda hii na akapata atapewa hii kazi. Kwa bahati nzuri tulipotoa tenda hatukusema watu fulani wanaruhusiwa kuomba, watu fulani hawaruhusiwi kuomba. Tulitoa tenda iliyokuwa wazi kabisa. Kwa hivyo wa Unguja akaomba, wa Dar es Salaam akaomba, wa Bara akaomba, wa Visiwani akaomba, wote wakaomba.

Kwa bahati mbaya tena sana Mheshimiwa huyu sahibu yangu Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali alikuja ofisini akataka kutusaidia kuweka fanicha za hiki chuo, madarasa, ofisi. Lakini kwa hakika hakutaka kutusaidia alitaka kutukopesha. Bahati nzuri nimekuja na vitu hivi makusudi, narejea tena kusema sikusudii kushindana wala sikusudii kuwa jeuri, wala sikusudii kutoa maelezo marefu. Nakusudia kuweka mambo sawa, kwa sababu kilichozungumzwa jana kimeingia kwenye *hansard*, na ninachokizungumza mimi leo nataka kiingie kwenye *hansard*.

Mheshimiwa sahibu yangu katuletea vitu hivi ndivyo alivyokusudia kutuuzia kwa mkopo ili vitiwe skuli. Kweli jamani *by all means, with due respect.* Hizi ndio fanicha za kuzitumia kusomeshea watoto wetu? Sisi tulimwandikia barua tukamwambia kwamba ingia kwenye tenda ukipata nafasi, ukipita, utapata nafasi ya kuchonga hivi vitu na kutuuzia. Mheshimiwa sahibu yangu alikataa kuingia kwenye tenda, hakuingia kabisa!

Tukatangaza tenda, tukafanyia *evaluation*, tukaipasisha, na kwa bahati ya kawaida akapata tenda hii huyu mwenzetu wa Bara. Tukaulizwa pesa mmepata wapi, jibu tumeshatoa ni msaada wa *BADEA*. Hili deni lililobakia limebakia vipi la shilingi zaidi ya milioni mia moja na kitu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kujibu kwamba deni hili limebakia kwa sababu kazi ilikuwa haijamalizika, na tulizuia gharama nyengine ili kazi itakapomalizika tulipe pesa zake. Kwa bahati nzuri pesa zile zimetiwa katika *vote* yetu zipo. Na kwa bahati nzuri huyu mwenye tenda juzi amekuja ofisini kwetu akatwambia sasa ameshavipata vitu vyote yupo tayari kuvikamilisha. Mara atakapovikamilisha tutamlipa, pesa zake tunazo ili viweze kukamilika.

Sasa nimesikia fununu lakini sina haja ya kuzieleza, wala sina haja ya kuzitaja. Kwa nini Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali amesema yale. Kwa ufupi, kwa bahati mbaya sana hii tenda ameikosa hakuipata, na hii tenda ina pesa nyingi, lakini tunasema kama amekosa hili lipo jengine, almuradi aingie katika tenda katika utafutaji wa shughuli hizi kwa uwazi kabisa, lakini kuja kutwambia mimi nitakupeni shilingi kadhaa, nipeni mimi kazi hii na nitaifanya vizuri, akisha akasema ataifanya fundi wangu.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili barua ninayo na mimi nitakukabidhi barua hiyo kuweka ushahidi kamili. Nitakukopesheni msilipe hata pesa moja, lakini tukimaliza kazi mnipe pesa zangu zote, nitakupeni fundi wangu. Kazi kama hiyo na amri kama hiyo sisi si aghlabu kuweza kuifuata.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwaambie wale wenzangu waliomuunga mkono Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali shauri lake alilolitoa nimelijibu. Na kama mlitaka nijibu kwa uwazi na kwa ufasaha nimejitahidi. Nasikitika sana laitani Naibu Waziri wangu angekuwepo hapa na yeye kwa kuwa ni mchangiaji wa mwanzo katika suala hili, angelieleza kwa ufasaha mkubwa zaidi hata kuliko nilivyozungumza mimi, lakini bahati mbaya hayupo.

Sasa suala la mikopo sisi kama wizara hatukubali na haturuhusiwi kukopa kwa mtu binafsi, anayekopa ni Wizara ya Fedha. Sisi tumekwenda Wizara ya Fedha kuhusu suala hili. Wizara ya Fedha jamani amekuja mtu anataka kutukopesha pesa afanye kazi kadhaa wa kadhaa. Jawabu tulilolipata hamuwezi kufanya kazi hiyo kwa kumtegemea mtu mmoja, na kwa kuweka masharti kama hayo haiwezekani hilo. Tumezuiliwa tusikope kwa mtu binafsi.

Lakini kubwa zaidi tumesikia kadhia iliyompata Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Ukikopa pesa hizi au ukikopa kitu hichi kwa Mheshimiwa huyu anaita *Press Conference* kuelezea kwamba fulani aliyekopa amechukua pesa hizi hajalipa mpaka leo. Sisi tunaogopa kuingia katika mambo hayo ya kutangazwa katika redio na televisheni kwamba tulikopa.

Nimesema hili na nasema tena, si Mheshimiwa huyu tu. Mheshimiwa mwengine yeyote akitaka kunisaidia anisaidie kwa kutoa sio kwa kukopesha. Kama kukopeshwa mimi nitamfuata mwenyewe na nitaomba kibali cha Wizara ya Fedha, nikikipata tutafanya kazi hiyo. Mhe. Mwenyekiti, katika hili nakuomba kwa ufupi yachukue hayo na nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, mchangiaji wa pili alikuwa Mhe. Mussa Ali Hassan. Namshukuru aliomba tummalizie skuli zake. Katika hili naomba kulitolea ufafanuzi kwa wale wote walioniomba. Nawaomba radhi sana, kwamba Wizara kwa niaba ya Serikali iliahidi kuwa wananchi jengeni skuli zenu, zikifika pahala fulani tupeni sisi tutakumalizieni.

Mhe. Mwenyekiti, tumejitahidi sana kwa fedha kidogo tulizopewa kiasi ya shilingi milioni mia moja na kitu tumemaliza skuli nyingi sana, lakini bado zipo skuli nyingi sana hatukuzimaliza.

Na wale waliosema nilizitembelea skuli zao nikaona mazingira yalivyo na nikaahidi nitazimaliza, sikuzimaliza. Naahidi tena iwapo pesa hizi hizi nilizoomba ambazo ni kidogo sana zimepunguzwa, lakini hizi hizi nilizoomba namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha akinipatia nina hakika hii kazi nitaifanya.

Lakini zaidi ya hayo, suala la kuzimaliza skuli za Serikali zilizojengwa na wananchi, suala hili sasa lipo kwa Mhe. Rais. Mhe. Rais ametuagiza tumpelekee takwimu sahihi, hili tumefanya. Kimebakia nini, tunahitaji tufanye nini ili tutoshelezeke. Maelezo hayo yote tunayatayarisha, tunampelekea, *asaa* mkubwa akitaka suala kama hili ameshavumbua nyenzo za kukusaidia. Na Mhe. Rais hachoki kutusaidia, kwani akitusaidia sisi anaisaidia Serikali, anaisaidia jamii.

Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tuna tatizo la kutengeneza madawati na hili nitakuwa nalijibu lile suala lililoulizwa na wengi. Mmepata pesa ngapi katika hizi pesa zilizodhamiriwa kukatwa kwenye wale watu wanaokata tiketi. Mpango ni vipi, mmepanga ngapi na kadhalika. Nitakuwa najibu na hili pia.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais alituita akatwambia tumpe idadi ya vikalio tunavyovihitajia, tukampa, tunavyo vingapi, tukampa, mapungufu mangapi tukampa. Kimya kimya likaja hili suala kwamba wasafiri wote tuwakate shilingi mbili ili tupate kukusanya pesa za kutengeneza madawati. Tukakata pesa zikaingia *alhamdulillah.*

Kwa msaada aliotupa Mhe. Rais na pesa tulizotiliwa na Wizara ya Fedha baada ya kukamilisha madawati tumepata hatua kubwa. Na utaratibu tulionao sasa ni hivyo hivyo tumefanya awamu ya kwanza kazi hii, tumesambaza madawati mengi Unguja na Pemba.

Sasa awamu ya pili tunakwenda tumeshaitangaza tenda. Waheshimiwa wote wenye mafundi wao, wenye zana zao, wenye uwezo wao, waingie katika tenda hiyo ya shilingi bilioni mbili. Tukipitisha tenda hizi Mhe. Waziri wa Fedha atakuwa tayari kutupa hizo fedha tufanye hiyo kazi.

Mimi sio kwa sababu mwenyewe yupo hapa, hapana. Mimi najua serikali au nchi kwa jumla haina mapato, uchumi wake haukupanda bado tunasuasua hivyo hivyo, lakini Mhe. Waziri wangu ananisaidia sana. Nikienda na kilio changu hanirudishi, ananisaidia kwa kile kile alichonacho, kwa hivyo hizi bilioni mbili tutakapompelekea tenda na kumuelezea sasa watu hawa wapo tayari hii kazi tupe, nina hakika atatupa. Mara pesa zipo atatupa tufanye hiyo kazi, kwa hivyo Mhe. Rais alipokwambia niletee taarifa ya kitu kadhaa, kitu kadhaa, nina hakika Rais huwa ameshajiandaa kutusaidia.

Mhe. Mussa umesema mambo mengi, ninayapokea ninayakubali, lakini nakuomba sana hili moja la kujenga matuta karibu ya skuli barabarani; umenikabidhi lakini mbona si langu. Matuta hayajengwi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini kwa heshima na taadhima kubwa, nimelipokea hili tatizo lako na nitazungumzia na wizara zinazohusika na nitashirikiana nao tuhakikishe matuta yakilazimika. Maana yake ninajua kuna matuta mengine yanabomolewa, matuta mengine yanayojengwa yanabomolewa. Kwa hivyo ikilazimika, ikionekana ipo haja basi nitazungumza na wenzangu ili tuifanye kazi hii.

Ulizungumza tukumalizie skuli zako. Ninajua ni deni kubwa sana umeniachia. Na kila siku tukikutana mimi ninakwambia hili deni ninalikubali sina pingamizi. Ni muda mrefu na panapo uhai na uzima tukitiliwa fedha mwaka huu tulizoomba kwa kazi hii, kama si mradi wa tatu au wa nne basi utakuwa ni wa tano wa skuli yako kukujengea paa unalolitaka.

Mhe. Mohammed Haji Khalid umezungumza sentensi zako tumezisikia, michango yako tumeisikia. Tunachosema yale yote unayosema tuyafanye ambayo yanahitaji fedha siwezi kutoa ahadi asilimia mia juu ya mia kwamba nitayafanya, aah! Mimi niliituma Kamati yangu ya Baraza la Wawakilishi wanipigie debe Wizara ya Fedha inisaidie kunipatia fedha zangu zote ninazoomba. Mimi mwenyewe napiga debe hivi sasa, na ananisikia kwamba deni limekuwa kubwa na siwezi kulilipa. Deni la kuzimaliza skuli za wananchi.

Jamani hizi skuli ni muhimu kuzimaliza, ni muhimu sana. Wanafunzi wetu hawana pa kukaa, wanafunzi wetu wanatumia madarasa machache, darasa moja watu 100, 150 mpaka 200. Anayetaka nimpe ushahidi tupange siku twende Skuli ya Kijitoupele. Tukienda Skuli ya Kijitoupele ataona jinsi makaazi ya wanafunzi wetu walivyo.

Kwa hivyo wanaonidai skuli zao, wanaonipigia kelele nizimalize, nitawakubalia asilimia mia juu ya mia, maana hiyo shida ni yangu mimi vile vile. Kwa hivyo Mhe. Mohammed Haji Khalid ninakuomba sana nistahamilie, panapo uhai na uzima tukijaaliwa na Mwenyezi Mungu Mhe. Waziri wa Fedha akinitilia fedha zangu, na *inshaallah* atanitilia, basi nitafanya kazi hiyo kwa haraka sana.

Mchangiaji mwengine alikuwa ni Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Ninakubaliana na yote aliyosikitika kwamba skuli sizimalizi. Skuli ya Sharifu Msa ameitaja, Skuli za Bububu amezitaja kwamba baadhi ya skuli hizo zinavuja. Mhe. Mwakilishi kwa heshima na taadhima kubwa sana, nimepokea michango yako yote. Panapo uhai na uzima basi tutaijenga hiyo skuli ya Sharifu Msa pamoja na kuziba hayo mabanda yanayovuja.

Lakini tulikutana mimi na wewe na nikakupa habari kwamba unioneshe hicho kiwanja chako ulichonacho cha Bububu kinachofaa kujengwa skuli. Mhe. Mwenyekiti, katika ule msaada tuliopata wa skuli 10 za ghorofa kwa Unguja na Pemba, msaada huu ukitimia tutakaposaini mkataba, tutakapomaliza kutoa *go ahead*. Mjini Magharibi nimepanga kujenga skuli tatu.

Ukitaka kuona ushahidi kwa nini tumepanga kujenga skuli hizi Mjini Magharibi. Leo pita Skuli ya Bububu wakati watoto wanatoka skuli na pita skuli nyengine. Mimi juzi nilisimamisha gari makusudi nikaona umati wa wanafunzi hawa wanakwenda huku na hawa wanakwenda huku, skuli imepigwa kengele wanatoka skuli. Niliofuatana nao nikawaambia hapa pana haja ya kujengwa skuli hapa.

Sitoi ahadi hiyo, aah! Pana haja ya kujengwa skuli kutokana na umati uliopo. Nimesema Mjini Magharibi tutajenga skuli tatu. Nina hakika katika maeneo hayo, eneo la Fuoni kuna skuli na eneo la Bububu *asaa kheri* kuna skuli, lakini panapo uhai na uzima mradi wetu ukipita na huu utakuwa ni ukombozi mkubwa sana, tutazijenga hizi skuli kwa salama na amani. Tutatoa tenda, tutakaribisha *bid* watakaopata watabahatika kufanya kazi hiyo ya kuzijenga skuli hizo.

Sitorejea kufanya kosa lile alililolifanya Haji Mtule na kwengineko, tenda tatu kumpa mtu mmoja, hapana. Sasa kila mmoja ninampa kazi yake ili watu washindane kujenga hizi skuli. Kwa hivyo mtu asifikirie skuli 10 tenda moja nitampa mtu mmoja anijengee skuli 10, hapana. Nimejifunza, *kufanya kosa sio kosa kurejea kosa ndio kosa*. Nimejifunzo hizo. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, samahani sana nime-*take by surprise* na mimi sina msaidizi, utaniwia radhi sana, lakini hilo nimelijibu la Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mchangiaji mwengine alikuwa Mhe. Saleh Nassor Juma ambaye ni swahibu wangu. Lile suala la tenda nimeshalijibu lakini ninataka kumuahidi ule mkataba tuliotiliana saini na yule aliyetuchongea na kututengenezea vile vifaa vya skuli ya *SUZA* nimekuja nao, na ulitaka ukabidhiwe na nitakukabidhi. Ulisema usipouona utanizuilia fungu. Nakuomba kwa heshima na taadhima na kwa urafiki wote tulionao mimi na wewe, fungu langu niachie. Usinizuilie, nipewe ili nipate kutekeleza haya niliyoahidi.

Mhe. Bi Raya Suleiman Hamad nimekusikia kilio chako na nivumilie kwa kuahidi na nitaahidi mambo mengi sana, nivumilie. Umeniambia walimu wale waliopata elimu ya mjumuisho niliowapeleka Arusha, Bagamoyo na kwengineko, mpaka *University* ya Uganda tuliwapeleka. Hawa wameshareja; wamerejea na uwezo mkubwa *alhamdulillah*, wamerejea kazini na tunaendelea vizuri na somo hili la skuli mjumuisho.

Umeeleza kwamba wapo watoto wanaomaliza kufanyiwa mitihani yao kadhalika, wamepasi. Kuna watu umetwambia tunawafanya nini hawa kuwapa motisha ili elimu mjumuisho ipate hadhi yake na waongezeke. Nimelisikia wazo hilo, tutakaa na wenzangu tulifikirie namna ya kulitekeleza ili tufanikiwe na hayo mawazo yenu.

Umesikitika sana hatuwatendei haki wanafunzi mjumuisho wenye matatizo kwa sababu wana mapungufu hatuwatafutii vikalio maalum, hatukujenga sehemu ambazo wanazoweza kupita na vigari vyao wakaenda maskulini na kadhalika.

Hilo suala nimelisikia na ninakuahidi kwamba hiyo tunaifanya skuli zetu nyingi sana tunazozijenga sasa, tunajenga na *ramp*. Ingawa ile skuli ninadhani kwa bahati mbaya ile *ramp* imeharibika; imeanguka, kwa bahati mbaya ninasema, sio kwa dharau lakini ni kwa bahati mbaya, lakini skuli zetu zote tunazozijenga na watu wenye matatizo wanafika kila pahala wanapotaka kwenda *alhamdulillah*.

Mhe. Mwenyekiti, ila kuwachongea viti maalum watu hawa. Ninasema hiyo itakuwa kidogo ni vigumu, lakini nimepokea wazo na tutajitahidi kulifikisha pahala pazuri pole pole na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa ndugu yangu Mhe. Thomas samahani sana kama nimelisahau jina. Jina la mwanzo nimelisahau lakini hili jina la pili linaitwa Thomas. Ninakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Jina lake anaitwa Marina Joel Thomas.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Marina Joel Thomas ninakushukuru sana kwa michango yako.

Nimezipokea pongezi zako. Nina hakika pongezi hizi umezitoa kwa imani kubwa sana. Kwa kunionea huruma kwa kazi kubwa niliyopewa ambayo ninajitahidi kuitekeleza. Umeniambia wale wastaafu walioachishwa kazi au waliostaafishwa wamepata haki zao? Ninakujibu wamepata. Kama si wote basi ni wengi sana.

Umenishauri tunapojenga madawati, tujenge madawati yenye viwango, mazuri na madhubuti. Ninasema tunafanya kazi hiyo lakini bado tutaendelea kutoa tenda na watu watafute tenda hizo tutatangaza rasmi. Wasimamizi tunao ma-*carpenters* wetu na *engineers* wetu wapo. Ingawa mwaka huu wamezorota, lakini tutajitahidi.

Mhe. Mwenyekiti, samahani nirudie kwenye lile suala la Mhe. Ismail Jussa Ladhu la vitabu. Nisije nikamaliza kusema nikapigiwa buti nyengine ya bure. Ninasema hivi Mhe. Ismail Jussa Ladhu vitabu kweli vina makosa. (*Makofi*).

Na *English* iliyoandikwa kwenye kitabu kile ni mbovu sana, badala ya kusema mpira ulipoanzishwa yule *referee* alipuliza firimbi wakasema alipuliza tarumbeta, maana yake firimbi ukiipuliza inalia na tarumbeta ukilipuliza linapiga kelele. Kwa hivyo, kizungu chake firimbi maana yake ni tarumbeta, hayo makosa tumeyaona.

Mhe. Mjumbe, ulitaka nikueleze maelezo ya kina, sina maelezo zaidi kuliko hayo, ila hata kabla hujatoa hoja hii, hoja tuliiona zamani sana sisi. Tulikwisha kufanya kazi ya kukusanya vitu hivi ili tuvifanyie uchambuzi na kuviandika tena upya.

Najua litakuja swali la nyongeza hapa. Mkiandika upya si maana yake mtatumia fedha nyengine za serikali. Tutafanya nini? Tunakiri kosa lilitokea na kosa lilitokea hapa ilipaswa vitabu hivi vilipokuja tuvifanyie uchambuzi, ufafanuzi na kadhalika na tuvipitie vyote ukurasa kwa ukurasa ndipo tuvitie saini kuwa tumevipokea. Badala yake waliochaguliwa kufanya kazi hii tumepitia, hatukusema kuwa hatukupitia, tumepitia ukurasa kwa ukurasa, lakini waliochaguliwa kufanya kazi hii sio hawatoshi; hawafai.

Unampa mwalimu wa *primary school*, apitie kitabu cha Kiingereza ambacho ndicho utakachosomeshea, vipi? Kwa nini usimpe mwalimu wa Sekondari, kwa nini usimpe mwalimu mstaafu na kadhalika, ukampa mwalimu wa skuli ya *primary* apitie kitabu cha *primary school* kwa Kizungu cha *primary school* ni kinyume.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu tunakubali kosa limetendeka. Sasa hivi tutachukua hatua ya kuandika muongozo ili tuendelee kuwasomesha watoto wetu wa pale pale skuli, vitabu tumeweka pembeni tunavifanyia uchambuzi, tukishamaliza tutaviandika upya.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, vyovyote itakavyokuwa kosa limetendeka na mimi mwenyewe binafsi nakubali kosa limetendeka. Nimeshatoa agizo hilo kuagiza lifanyiwe kazi, tusiendelee kuwasomesha watoto wetu vitabu vya ajabu ajabu, tumesikia hilo.

Sasa ukinipigia buti ukiniambia nitoe maelezo ya ziada, baada ya maelezo hayo mimi sina mengine. Ila papite uungwana wa kusameheana, nilaumu utakavyopenda kunilaumu, niambie utakavyopenda kuniambia, lakini mwisho wa siku yetu ni kufanya marekebisho na kuhakikisha wanafunzi wetu wanapata kitu kinachofaa, na hatutorejea kosa hilo. Nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Mhe. Viwe Khamis Abdalla, ambaye ametushukuru, ametupongeza na ametulaumu panapostahiki kulaumiwa. Tumepokea lawama hizi, tunaahidi kwamba tutalirekebisha, tutafanya masahihisho na hatimaye tutakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, wachangiaji wengi na hasa Mhe. Ismail Jussa Ladhu alizungumza hili limemuhusu Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Subeit Khamis, Mhe. Nassor Salim Ali wote walizungumza suala hili la posho za kufanyia kazi. Maposho haya mliyapigia makelele Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sana, mwaka juzi na mwaka jana, tukawasikiliza sana. Mwaka huu wa 2013/2014 ndio tunaanza kuyatekeleza. Maposho hayajakamilika lakini tunajitahidi kama tuwezavyo kuyafanikisha.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim Ayoub ulizungumzia suala la mikopo. Nataka kusema suala la mikopo limezungumzwa na Wajumbe wengi sana na hoja ni moja ya msingi. Kwa nini mwaka jana mikopo iliongezeka na mwaka huu mikopo imepungua. Nataka kusema fungu la mikopo limeteremka kwa sababu ya mapato ya serikali. Mwaka jana tulipewa bilioni 9 na marupurupu tuwakopeshe wananchi, tukaongeza mikopo hadi 1,000 na marupurupu vile vile.

Mwaka huu nimepewa bilioni 8 kama tulivyopewa mwaka juzi. Sasa kama ulichopewa kimepunguzwa bila shaka na idadi ya mikopo utaipunguza. Ndio maana mikopo tutafanya safari hii wakopaji 1,000 ndio tutakaowakopesha, sio zaidi ya 1,400 kwa sababu fedha zetu zimepunguzwa. Sasa hilo hatuna namna wala hatuna njia ya kulirekebisha.

Ukiniambia tukate vifungu vyengine, vifungu gani. Ukiniambia tukate mshahara siwezi, tukate maposho siwezi, tukate vitabu siwezi na kadhalika, sijui tukate wapi hata turejeshe kwenye mikopo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa mwaka huu tuombe posho libakie hilo hilo tulilopewa la bilioni zaidi ya 8 na wakopeshwaji tuwaweke hao hao tuliowaweka 1,000, na kwa kiwango cha 1,000 Mhe. Jaku Hashim Ayoub sio kidogo jamani, ingawa kimeshuka, lakini ndio hali ilivyo hapa tustahamilie tutapigania tukipandishe tena mwakani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, uliangalia ile mikopo tu, lakini hukuangalia la kurudisha waliokopa, kurejesha zile pesa za waliokopa basi utakuta tumeongeza, idadi imeongezeka kubwa sana na tumeahidi tutaongeza kwa mwaka ujao na njia tutakazofanya ni hizi hizi za vitambulisho vya mkaazi vya kuwafuata watu makazini mwao, na kuwafuata Wakurugenzi na kadhalika. Na kwa bahati nzuri zile taasisi za Muungano kama Polisi, Jeshi na kadhalika tumeshafanya utaratibu, sasa wanatulipa moja kwa moja, wanawakata watu wao moja kwa moja wanatupatia pesa zao walizokopesha.

Kwa hivyo, na sisi tulikwishaamua kwamba Jeshi, Polisi na kadhalika hatuwapi mikopo. Tuliwaandikia barua wakubwa wao wakatujibu hivyo, na sasa *alhamdulillah* mambo yatakuwa mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salma Mohammed Ali wa viti maalum. Mama, mimi hukaa na Waziri mwenzangu hapa Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo tukakunong'ona kila unapochangia, tunasema sasa sikiliza vitu vinakuja hivyo. Mhe. Salma Mohammed Ali tunakupongeza sana kwa michango yako yote unayochangia, ni ya uhakika, umakini na ni michango bora sana, kwa hilo tunakupongeza sana.(*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Somo la Ujasiriamali ulilolizungumza hatulisomeshi peke yake, tunalisomesha kwa maana halisi ya somo la ujasiriamali; tunachanganya na masomo mengine, ili wanafunzi wetu wakimaliza wawe wamepata taaluma ya kutosha, wanaweza kujitegemea na kujiendesha. Kuna suala kama hilo lilikuja wajasiriamali hawa waliomaliza masomo yao kwa mara ya tatu mfululizo.

Mimi nasema hapana, wamemaliza mara moja tu miaka mitatu ya mwanzo imemalizika tumewatunuku, tumewapa mitihani wamefaulu, waliofaulu na sasa tumewakusanya pamoja tunawakopesha pesa. Karibu watapata pesa zao za kununua vifaa vya kuanzia kazi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri tujitahidi kuzingatia na muda pia.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Jaku Hashima Ayoub, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Salma Mohammed Ali, ndio yule yule niliyemtaja na Mhe. Salmin Awadh Salmin na wengine. Wote nyinyi mlizungumza kuhusu maslahi ya walimu na mkajenga hoja kwamba walimu wanastahiki kutunzwa na kuenziwa na kadhalika. Wala sina ubishi kabisa katika hilo. Mwalimu ni mtu mkubwa sana, na sisi kwa hakika hatuna cha kukilipa kwa mwalimu, atalipwa na Mwenyezi Mungu kwa kazi yake anayofanya ya kuwaongoza wanafunzi wetu; watoto wetu na wazee wetu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuahidi kwamba tumefanya mara tatu mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu kuongeza maposho, kuongeza mishahara, kuwaruzuku wale walimu wa zamani wanaokaribia kustaafu na kadhalika.

Tulifanya mengi kiasi, mtupongeze jamani, msitulaumu moja kwa moja, lakini tunaahidi tutaendelea na juhudi zetu hizo ili kuhakikisha hata Mhe. Rais wetu analizungumza hili kila leo, linamgusa kila leo kwamba walimu wetu tuwaenzi,tuwatukuze, tuwasaidie maposho yao, mishahara yao na kadhalika. Mhe. Mwenyekiti, laiti tungekuwa tuna bajeti nzuri, tuna pesa nzuri, madukhuli mazuri, basi tungeongeza maposho, tungeongeza mishahara na kadhalika. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa sana na kwa kuwa niko peke yangu, msaidizi leo amedharurika dharura ya ulimwengu, nimejitahidi nilipoweza, palipobakia kwa wale ambao sikuwataja mmoja mmoja, lakini michango yao ya jumla nimeijibu kwa pamoja wapokee majibu hayo. Kwa wale ambao sikuwajibu kabisa, sikuwagusia, nasema sikudhamiria kuwasahau. Kwa mfano, Suleiman Hemed Khamis na amechangia vizuri sana na kuniomba sana nisaidie skuli zake na kadhalika, kama vile Mhe. Ali Salum Haji nimemsikia na amechangia vizuri tokea kwenye kamati na hata hapa Baraza pia amechangia vizuri, ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Ussi Jecha Simai, tulisema ulipopata upashukuru na bado tunao wengi nyuma hatujawakamilishia. Lakini Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali asije akanihukumu na kunipigia buti jengine bure, tunasema skuli zako za Jimbo lako la Uzini kuna skuli 6 ambazo zimejengwa kikamilifu, tumetia vikalio na ile skuli nyengine nimeisahau jina ya madarasa mawili nimeijenga kikamilifu, na kama kuzishughulikia skuli ambazo zimejengwa na wananchi katika majimbo, *Alhamdulillah* Jimbo la Uzini limefaidika na tunashukuru tulipopapata. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ninamuahidi na sio kwamba nimemsaidia ndio nitafunga mikono. Ni wajibu wangu kama ulivyokuwa wajibu wako kunilaumu, lakini ni wajibu wangu vile vile kutekeleza lawama zako, ili kuhakikisha kwamba ninajirekebisha, kwamba ninatekeleza yale yote ambayo uliyoniagiza na ukiacha yale ambayo niliyoyataja mwanzo.

Mhe. Fatma Mbarouk Said, kwa kweli tumemsikia na mchango wake tunauthamini. Mhe. Mwenyekiti, amezizungumza skuli zao mbili zenye matatizo Mhe. Mjumbe, lakini napenda kusema kwamba matatizo tumeyamaliza kwa kuwaita watu wa Amani kwa Wazee na watu wa Kwamtipura. Tukawauliza kwamba kuna Amani wanataka jina hili na Kwamtipura wanataka jina hili tufanye nini, walikaa kwa pamoja na kukubaliana jina la Faraja na wala jina la Faraja halikutoka mifukoni mwetu.

Kwa hivyo, wakasema kama tumepata skuli kama hii nadhani hii ni faraja, sasa kwa nini hatuiti faraja, na sisi tukalichukua jina la faraja. Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru Mhe. Mjumbe kwa *comments* zake na ile skuli aliyoniahidi kwamba niitembelee nitaitembelea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kiasi naomba radhi sana kwa wale wote waliochangia nimeyasikia maneno yao, pia na kuyathamini malalamiko yao na wale waliokuwa wakali au wakakamavu sana na kusema hawapitishi bajeti yangu mpaka niseme hivi na vile. Kwa kweli, ninawaomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba wanistahamilie na warejeshe roho zao za kupitisha bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa sababu bajeti hii ni ya Serikali, ni ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Lakini nyote mliokuja hapa na kusema kwamba elimu ni sekta muhimu sana na wizara muhimu sana kama ilivyo Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu ni muhimu sana, nadhani vyema tukabakia na moyo huo huo, bila ya kuipitisha bajeti hii umuhimu utayayuka na kurudi *back step one*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba uyapokee maelezo yangu kama watakavyoyapokea Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi na wale waliohamaki na kukasirika ama walionuna. Kwa hivyo, nawaomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, warejeshe roho zao ndio mambo, kwa sababu siku zote ukweli unauma, na msema kweli ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Kwa kweli mnaponilaumu ninazipokea lawama zenu, tena ninaziheshimu sana lawama zenu, na ninakuogopeni sana, ninahakikisha kwamba ninakujibuni ipasavyo na pale nilipokosea Mhe. Mwenyekiti kwa niaba yako ninawaomba radhi wenzangu, wanisamehe na tuipitisheni bajeti hii, ili tuendelee mbele. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ahsante kwa majibu yako pamoja na ufafanuzi ambao umeutoa. Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja ambayo Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wanyooshe mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kukubali Hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Sasa naliomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 23 - WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Kifungu 0401	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	30,000,000/=
Jumla ya Fungu		**30,000,000/=**

Kifungu 0401

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia pumzi. Mhe. Mwenyekiti, nataka kuweka *hansard* sawa kwa sababu kama mzee wangu ninamuheshimu sana, husema siku zote ukweli ndio utabakia kuwa ukweli kwa jambo lolote ambapo Mwenyezi Mungu ameahidi.

Kwanza ni kuhusu suala la kuzungumza na waandishi. Ni jambo la uhuru wa kila binadamu, na mimi ninao uhuru wa kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, samahani tupe hoja moja kwa moja na wala hatuhitaji hotuba nyengine.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kwa sababu imeguswa hii hoja ambayo imenigusa mimi ni kuhusu suala la *tender* ya *State University of Zanzibar Campus* ya Tunguu. Biashara hii sikuanza mwaka 2012 nilikuwa sina duka wala sio mfanyabiashara wa *furniture*. Nataka niweke *hansard* sawa tu, kwamba hiyo haikuwa kweli, na wala sikuweka *tender* au mwaka 2012 sikuanza biashara hii na hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka juzi nilitoa maombi yangu hapa kwamba Skuli ya Pagali wakati Mhe. Rais wa Zanzibar alipokuja kuzindua Skuli ya Pagali tarehe 18 Julai, 2012.

Kwanza Mhe. Waziri naomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti athibitishe kwamba niliyosema ni ya kweli; kwamba siku ile Mhe. Rais alipokuja katika Jimbo la Uzini Skuli ya Pagali Mhe. Waziri hakuwepo alidharurika, Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu, na wala Naibu Katibu Mkuu wote hawakuwepo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tunaomba hoja.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, sawa. Kwa hivyo, naomba kupata maelezo tu, kwa kuwa Mhe. Rais aliahidi kwamba Skuli ya Pagali kuezekwa tokea mwaka 2012. Naomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, aniambie kwamba ahadi hii ya Mhe. Rais kwa nini haikuweza kutelekezwa na itatekelezwa lini hii ahadi ya kuezekwa hili banda.

Pili katika...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hoja ni moja tu.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kupata hoja hii ya Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali ya Skuli ya Pagali. Mhe. Mwenyekiti sitaki niyarudie yale uliyoyazuia yasizungumze, na mimi sitoyazungumza hivi sasa na niliyazungumza huko nyuma.

Mhe. Mjumbe, alitaka nitoe ahadi. Hizo ahadi alizotoa Mhe. Rais nitazitekeleza lini. Mhe. Mwenyekiti, tamko langu ni lile lile ambalo nimelitoa wakati nilipoelezea skuli nyengine zote. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niliomba radhi kwa zile skuli ambazo sikuzitekeleza, na nilitoa sababu na nikamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha safari hii anisaidie kunipa kama sio zote nyingi sana nilizoziomba, ili tumalize kujenga hizo skuli ambazo tumeziahidi.

Sasa kama Mhe. Mjumbe anataka nitoe ahadi kwa kutaja tarehe, siku na saa nitashindwa. Isipokuwa ninatoa ahadi kwamba tukizipata fedha hizi kwenye vifungu vyangu, na kwa kuwa Waziri wa Elimu nipo hapa na tumeshamsikia

Mhe. Mjumbe kwamba hili ni tamko la Mhe. Rais, nitakwenda kwa Mhe. Waziri wa Fedha kwa ajili ya kunipatia vifungu na wala sio hichi, isipokuwa anipatie vifungu vingi kwa ajili ya kuweza kuifanya kazi hii.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Mjumbe kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba anisamehe sana, kwa sababu siweze kutaja siku na tarehe, lakini tutatekeleza. *(Makofi)*

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu yake, lakini naona bado itakuwa ni kitendawili kwa sababu huu ni mwaka wa tatu tokea mwaka 2012, na wala hapakuwa na majibu ya barua ambazo zilizopelekwa zikafanyiwa kazi. Sasa ninasema lazima kuwepo na nia.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nataka Mhe. Waziri atoe tamko la serikali, je, haya majengo mengine tunayowaambia wananchi waendelee na wakati ikiwa haya bado hayajamalizika, sasa hawa wananchi tunaowaambia waendelee kwa nguvu zao, hivi majengo haya kweli yatakuja kumaliza?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kwa kweli Mhe. Waziri amejibu, na kama Mhe. Waziri wa Fedha atamuingizia fedha, suala hili amelisikia na atalitekeleza na tayari amekwisha kusema.

Sasa anachokiomba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ni kwamba Mhe.Waziri wa Fedha amtilie hizo fedha, labda unachokitaka ni uhakika wa Mhe. Waziri wa Fedha athibitishe kama atatia hizo fedha au vipi, nadhani tufanye hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa majibu yako mazuri, lakini Mhe. Mwenyekiti, hii ni ahadi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na wala sidhani hapa kama kuna suala au nini, kwa sababu ni ahadi ya Rais wa nchi chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, na huu ni mwaka wa tatu. Mhe. Mwenyekiti, huyu ni Rais na sio mtu wa kawaida, na kama Rais sidhani kama sisi wenyewe tukaanza kulichezea.

Hata hivyo, nataka Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, aniambie je, wananchi waendelee kudanganywa? Kwa sababu ikiwa majengo kama haya Mhe. Rais ametoa ahadi na wala haikuweza kutekelezwa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia vizuri Mhe. Raza, kuhusiana na Skuli ya Pagali na vile vile, nimemsikia vizuri Mhe. Waziri wa Elimu (Mhe. Ali Juma Shamhuna) kuhusu majibu yake, nataka nimhakikishie tu Mhe. Raza, kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, la kwanza, kupatikana kwa fedha tupitishe bajeti ya Wizara ya Elimu katika kikao hichi ili tumpe uwezo Mhe. Waziri wa Elimu kuweza kutumia hilo la kwanza, Mhe. Waziri wa Fedha hatoweza kutoa fedha kama bajeti haijapitishwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili, nataka nimhakikishie tu, Mhe. Raza kwa umoja wetu, kwa pamoja tuhakikishe kwamba tunakusanya kodi zetu vya kutosha kwa ukamilifu, kwa sababu nilisema kwamba bajeti yetu inategemea mapato tunayoyakusanya. Kwa hivyo, tuhakikishe kwamba tunakusanya na kila ambaye anadaiwa kodi alipe kwa ukamilifu pamoja na Mwenyekiti wa *ZAT* walipe kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, la tatu, nataka nimhakikishie tena Mhe. Raza, tukimaliza tutahakikisha kwamba tunaipatia Wizara ya Elimu fedha za kutosha ili waanze kuiezeka hizi shule ambazo zinapaswa kuezekwa.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, nimesema mambo mawili juu ya jambo hili hili, suala la ahadi ya Mhe. Rais, kama ni hali tunaendelea hivi ya miaka mitatu, kwa nini tusimshauri Mhe. Rais anapofanya ziara azuie kutoa kauli zake kwa sababu hii inawagusa wananchi na kama Mhe. Waziri wa fedha anasema ni lini, kwa sababu hili sio jambo la kwanza naomba Mwenyekiti ni-*repaid*, hili si jambo la kwanza mwaka jana Mhe. Waziri aliihakikishia Miundombinu.

Mhe. Mwenyekiti: Suala la ziara ya Mhe. Rais, hilo ni suala jengine, hapa tunataka kuthibitisha upatinaji wa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa hizi shule, Mhe. Waziri wa Fedha ameshatoa ahadi kwamba fedha atazituma baada ya harakati hizo kukamilika tusubiri sasa utekelezaji ndani ya Wizara inayohusika kwa ajili ya kukamilisha hizo ahadi za Mhe. Rais, nafikiri kwa hoja hii tumemaliza tuelekee katika hoja ya pili.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, hii ni ahadi ya serikali, sasa ningelimuomba kaka yangu namheshimu sana Mhe. Waziri wa Fedha anihakikishie kwamba katika kipindi hichi cha bajeti hii, skuli hii kwa ahadi ya Mhe. Rais itafanyika, halafu vile vile sijapewa majibu katika skuli tunazoendelea kwa nguvu za wananchi kwa kuwa nyuma hayajamalizika, hatuoni sababu kwamba serikali ingelisema kwamba sasa hivi wananchi tuwazuie wasiendelee na hili ili hizi skuli zilizokuwa miaka mitano au kumi ziendelee kuliko kuwadanganya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti: Hiyo hoja nyengine Mhe. Waziri, Mjibu hoja yake ya mwanzo ili tuweze kuendelea.

Mhe. Waziri wa Elimu, na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana sana Mhe. Waziri wa Fedha, nimshukuru sana kwa tamko lake kwamba atajitahidi awezavyo kunipatia fedha tunazoziomba pindi bajeti yangu ikipitishwa,lakini pia, Mhe. Waziri wa Fedha, aliwataja watu kuwaomba na kuwahimiza walipe kodi wasikae nazo walipe na akamtaja Mwenyekiti wa *ZAT* kwamba mmoja ni yeye aliyechelewa kulipa kodi alipe, ili fedha hizi zikipatikana na bajeti yangu ikipita, Mheshimiwa atakuwa tayari kunisaidia, mimi sina la kuongeza kuliko ahadi aliyoitoa Mhe. Waziri wa Fedha, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, hakusema Mhe. Waziri wa Fedha kwamba kama anachelewa au halipi isipokuwa ni ucherewaji tu. Kwa hivyo, hizo fedha ziharakishwe na ziweze kulipwa kwa mapema kama ambavyo sheria yetu tumeipitisha katika malipo yanayostahiki, ahsante sana.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuwa na mimi niweke sawa kwenye *Hansard*, nataka kuihakikishie Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mhe. Waziri wa Fedha, *ZAT* hatudaiwi hata senti tano, ni suala la mahesabu. Kwa hivyo, nataka kuweka *Hansard* sawa tu.

Mhe. Mwenyekiti: Hiyo siyo hoja yetu Mhe. Mjumbe, ahsante, tunaendelea.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, naweka *Hansard* sawa tu, bado sijapata tamko la serikali, nataka tamko la serikali kuhusu wananchi kuendelea kujenga kwa nguvu zao ili serikali ije kuezeka, kwa ushauri wangu nasema hapa tulipofika kuna vitu hivi vya serikali kuendelea kuviweka kwa miaka mitano haijamalizika, sioni sababu serikali itoe tamko kwa sababu kama alivyosema serikali hali yetu hai hoi, tuna uchumi mgumu tunataka kukusanya kodi na kukubaliana na kulipa kodi, ni jambo la lazima, ndio maana tumekuja huku, lakini serikali itoe tamko kwamba huku tusiendelee mpaka tuje tumalize huku nataka tamko la serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, Mhe. Mjumbe, anaomba tamko lako je?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Elimu: Mhe. Mwenyekiti, suala la kutoa tamko la serikali kama uwezo huo ninao, basi mimi sitotoa tamko la serikali kuwaambia wananchi wasijenge, huwezi kusema hivyo, kwa nini? Suala hili tumeshalizungumza kwenye Baraza la Mapinduzi, tumelijadili vya kutosha na tukaamua wananchi waendelee kujenga skuli na sisi tusaidie skuli, tusaidie kwa uwezo wetu utakavyoturuhusu, nasema kutoa tamko la serikali kwamba wananchi tuwazuie wasijenge skuli siwezi na sina mamlaka hayo, ahsante sana.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri, kwamba anasema haya ni maamuzi ya Baraza la Mapinduzi, lakini kama ni maamuzi ya Baraza la Mapinduzi, naheshimu sana kwa sababu Mhe. Rais wangu ndio Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, sasa kama haya ya nyuma hatukuweza kuyamaliza zaidi ya miaka mitano, halafu tunaendelea kuwapa mzigo wananchi ambao tunajua na tuna hakika hatuwezi kuyamaliza huoni, huu ni usumbufu kwa wananchi kwenye majimbo yetu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hoja yetu ilikuwa ni kutiliwa fedha na Mhe. Waziri, ameshakubali. Kwa hivyo, hoja yetu hiyo, ndio inamalizika, hilo suala la pili, ilikuwa ni Mhe. Waziri, kusaidia na tayari ameshatoa ufafanuzi, naomba tuishie hapo, tuelekee kwa mtu mwengine mwenye hoja ili tuweze kuendelea na taratibu zetu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri, kwa majibu yake fasaha katika baadhi ya hoja ambazo tumezitoa hoja ninayoisimamia katika Idara ya Mipango Sera na Utafiti, ni hoja niliyoitoa kuhusu kuwepo kwa fungu la posho la kufundisha, ambayo ipo katika sehemu ya kwanza kijifungu

211100, Mishahara ya Fedha taslim kuna kijifungu kidogo pale 211115, Posho la kufundisha *seating allowance* milioni 63,590,000.

Mhe. Mwenyekiti, ili Mhe. Waziri, anifahamu na kwa sababu leo kama alivyosema mwenyewe yuko peke yake hana msaidizi, nadhani ni muhimu kulifahamu sisi hilo, naomba niliseme taratibu kwa nini nasimamia hoja hii? Majibu yake Mhe. Waziri, kachanganya vitu viwili; kuna waliozungumzia kuhusu maslahi ya walimu na mimi nakubali kwamba ni miongoni mwa tuliokuwa tukisema siku zote kwamba posho hili wapewe walimu, lakini hoja yangu binafsi, ilikuwa ni kwamba posho hili limetengwa katika kila Idara ambayo inashughulika na walimu na ili kumsaidia Mhe. Waziri na wasaidizi wake haraka haraka, naomba niseme ukenda katika Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi ukurasa wa 142 wa buku hili la mahisabu kuna 220,000,000/= posho la kufundishal.

Mhe. Mwenyekiti, ukenda ukurasa wa 144, Idara ya Elimu ya Watu Wazima Posho la kufundisha ni 144 milioni, ukinda Idara ya Mafunzo ya Ualimu ukurasa wa 149, Posho la kufundisha 80 milioni, ukenda ukurasa wa 152, Idara ya Elimu ya Sekondari posho la kufundisha 180 milioni, ukenda Idara ya Elimu ya Watu Wazima Pemba ukurasa 161, Posho la kufundisha limetengwa 63 milioni, ukenda Idara ya Mafunzo ya Ualimu Pemba ukurasa wa 163, posho la kufundisha limetengwa milioni 33,500,000/=, ukenda ukurasa wa 164, Idara ya Elimu ya Sekondari Pemba, posho la kufundisha limetengwa milioni 200 na unamalizia Idara ya Technolojie habari Unguja ukurasa wa 166, zimetengwa milioni 48 na Pemba zimetengwa 32 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu kama kila Idara imetengewa fungu lake kwa walimu katika Idara hizi mbili, nimeanza hapa nitakuja hapa nitakuja hii hoja hii hii katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji, hili posho la kufundisha lililotengwa katika Idara zinazosimamia utawala katika Wizara linafanya kazi gani? Nataka majibu, halafu na hoja yangu kwamba fedha hizi zing'olewe katika Idara ya Mipango Sera na Utafiti na katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji fedha za posho la kufundisha wao hawafundishi wao wanasimamia *Management* waliofundisha wameshatengewa na wameziorodhesha zote hapa. Naomba maelezo hizi hapa zinafanya nini katika Makao Makuu ya Utawala wa Wizara?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Elimu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwa hoja yake sahihi kabisa, posho la kufundisha zilitiwa katika maidara haya kwa sababu zilichanganywa na mishahara na matumizi mengineyo vitabu na kadhalika. Kwa hivyo, sio posho peke yake la kufundisha jumla ya matumizi mengine katika Idara hizi, kwa mfano mishahara kama nilivyotangulia kusema. Kwa hivyo, hatukuweza kulibagua hili la kufundisha hili la kusomesha, hili la kufanya nini, hili limechanganywa kwa pamoja na mishahara.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, hakunielewa suala langu au hoja yangu. Naomba nirejee, sihoji kwa nini posho la kufundisha limewekwa katika jumla ya mishahara ya fedha taslimu, naheshimu maelezo yake nakubali linapaswa likae hapa, lakini kwa zile Idara ambazo nimezisoma, hoja yangu na naomba nisikilizwe vizuri hoja yangu, ni kwamba anayelipwa posho la kufundisha ni mwenye kufundisha mwenye kufundisha ametengewa fungu hulo katika kila Idara yao, elimu maandalizi, msingi, sekondari, mafunzo ya walimu, technolojia ya habari, elimu ya watu wazima, kote huko katika kila fungu la mishahara liko fungu lao wanaosomesha posho la kufundisha ninachohoji.

Mhe. Mwenyekiti, katika Idara ambazo wafanyakazi wake hawafundishi ni watawala ni *Management* ya Wizara, naanzia na hapo Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kuna milioni 63,590,000/=, lakini hoja kama hii ninayo katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji ana milioni 460 zimetengwa posho la kulipa nilikuwa nahoji hizi hapa zinafanya nini? Wanalipwaje watu wa wanaoshughulika na *Management* ya Wizara, fedha za kufundishwa wakati wao hawafundishi wanaofundisha wako kule na limeshatengwa fungu lao.Nataka maelezo na kama hayapo, nitaomba fedha hizi za posho la kufundisha zilizomo katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na zilizomo katika Idara ya Utumisi ya Uendeshaji, zihamishe ziende katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu zikasomeshe watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu naomba nimalizie, utajua kwamba fedha hizi sio za posho la kufundisha, kwa sababu posho la kufundisha katika Idara zote tulizosoma tumeona, ziko Unguja na ziko Pemba, lakini ajabu posho la kufundisha Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Idara ya Utumishi ya Uendeshaji ziko Unguja tu, Pemba katika mafungu haya hazionekani.Nataka maelezo, kama hayapo zihamishwe hizi hizi kwa ujumla wake, mafungu haya mawili ni 523,590,000/= ukenda ukizijumlisha katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu tutarudi kule kule kwenye bilioni tisa alizotaka Mhe. Waziri wa Elimu, watu wetu wasome ipasavyo, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya ziada kuliko niliyoyatoa, sinayo tena na kama fedha hizi zinahamishwa kupelekwa kwenye mafunzo ya amali, Mikopo ya Mafunzo ya Elimu ya Juu, mimi sina pingamizi, yote ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa hivyo, sina jawabu. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na nisisitize kwamba Wawakilishi wa wananchi tutaendelea kusimamia matumizi bora ya fedha za walipa kodi na kama alivyosema mwenyewe Mhe. Waziri wa Elimu, nikitumia Kanuni ya 98 6(C), niliomba kupunguza kwa sababu zinakataza kuengeza, hazikatazi kupunguza na madam zimo ndani ya Wizara ya Elimu kama sijamuondoshea kama mwengine nikasema ziende Hazina, nimependekeza.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba tuwe wasikivu ili tuweze kwenda vizuri, kuna hoja za msingi zinazungumzwa, tusikilize sote ili tufanye kazi yetu kwa ufanisi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, nimependekeza zibakie hapo hapo kwa Mhe. Waziri wa Elimu, ziende kwenye bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kwa hivyo, nashukuru kwamba tumekubaliana 523,590,000 ambazo hazihusiki na mambo ya utawala wa posho la kufundisha, ziende kule namshukuru Mhe. Waziri, kanikubalia na naamini baada ya hayo, Wizara yake naamini zitampa ufanisi yeye, nafikiri tuendelee.

Mhe. Jaku Hasshim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa kujibu baadhi ya hoja, kuna hoja yangu moja ambayo hakuwahi kujibu Mhe. Waziri, nayo iliahidiwa katika kikao hichi hichi cha Baraza la Wawakilishi ya Skuli yangu ya *primary* ya Muyuni, kutokana na uchakavu wake na hali yake ya mazingira Naibu Waziri, alikwenda namshukuru sana na akaiona hali ile ilivyo, na serikali ikakiri katika chombo hichi hichi na wananchi wenyewe wa Muyuni wanajua hivyo, nikaambiwa katika bajeti hii, *Hansard* hapa ninazo, mimi naomba nimkumbushe tu Mhe. Waziri, anipe jawabu ili tuendelee.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba arejee kidogo hoja ya Mhe. Jaku, kidogo kama itawezekana. Naomba ruhusa kutoa ufafanuzi mdogo tu kipindi tulizungumza kama ndio imeshamalizika basi.

Mhe. Mwenyekiti: Ile hoja ya kwanza ya Mhe. Jaku.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Jaku, sijaisikia, hebu anieleze tena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, nilipokuwa nikichangia, nilikaribia kulia kutokana na skuli yangu uchakavu wake wa Muyuni, hali yake hairidhishi na chombo hiki hiki cha Baraza la Wawakilishi imekiri kupitia kwa Naibu Waziri (msaidizi wako) ambaye bahati mbaya leo hakuja, kakiri kuwa katika bajeti ya mwaka huu skuli ile itaingizwa, lakini kitabu nikipekua na miwani, nimetafuta sikupata kuona kifungu hicho. Kwa hivyo, ile skuli ni chakavu, pamoja na nyumba za walimu za Jambiani, walimu pale wanakaa katika mazingira mazito na wanachangishwa shs. 7000/=, kodi zile, sijui umeshanifahamu Mhe. Waziri? Uchakafu wa banda la Skuli ya Muyuni la *primary* na nyumba za walimu Jambiani.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, wale Makatibu maana ya kuwaleta ndani, ina maana inapotokezea hoja muwe wepesi wa kumsaidia Mhe. Waziri, mukichelewa inakuwa ni mtihani.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa Skuli yake ya Muyuni, nilimtuma Mhe. Naibu Waziri, ende Skuli ya Muyuni akenda akaiona na tunakubali tuliahidi, ninamuomba Mhe. Jaku, awe mstahamilivu zaidi kwamba kwa mwaka huu iwe itakavyokuwa, tutairekebisha. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, anasema katika mwaka iwe itakavyokuwa, kwa maana mwaka huu haumalizi panapo majaaliwa itamalizika. Hoja ya pili, hakuwahi kuimaliza kuhusu mabanda ya walimu pale, hali yao hairidhishi nayo na wanachangishwa shilingi elfu saba kulipa kodi zile nyumba za walimu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, mabanda ya walimu ya Skuli na kadhalika, Skuli ya Muyuni eneo la Muyuni kwenye Jimbo la Mhe. Jaku, nitayafanyia kazi, ndivyo nilivyosema.

Mhe. Jaku Hashim Ismail: Mhe. Mwenyekiti, ujuwe Mhe. Waziri, akishakuwa mbele vyovyote anaweza kukubali, anataka lake liwe, sasa mimi anipe muda lini ili wananchi walioniajiri kule wananisikia hivi, sasa wapate kujua. Unajua mtu akishakuwa mbele yuko tayari kujibu lolote atakwambia kesho, keshokutwa. Nisha wahi kupata kauli kwa Mhe. Mohammed Aboud kama hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, Mhe. Waziri, amekwisha kutamka kwamba ni mwaka huu nini zaidi unataka au unataka tamko lipi la ziada.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tatizo mimi anambie Disemba, Oktoba au Novemba anieleze hapo tu hapana makubwa kitu kidogo tu, hicho anijibu hapo tu, nijiwe nini cha kuja kukifanya, maana yake haya maneno si yangu, hii *Hansard* ipo hapa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana na taadhima namuomba Mhe. Jaku, nimemwamia muda wa mwaka huu wa fedha nitalishughulikia suala hili. Sasa kama anataka nimwambie muda kesho au halafu kidogo, nitakwenda na kadhalika hilo haliwezekani. Bajeti ya Serikali ni mwaka mzima, kuanzia sasa hivi tukimaliza bajeti ikishapitishwa mpaka mwakani kipindi hicho chote, tutaifanya hiyo kazi, sasa anataka nimdanganye, mimi sikuzoea kudanganya watu. Ahsante sana.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti pamoja na marekebisho yake- 2,664,590
Kifungu 0701 Idara ya Utumishi na Uendeshaji-

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, sina dhamira ya kukwamisha katika majawabu ambayo Mhe. Waziri, sikumsikia kunijibu, ni suala la mafunzo ya madereva. Sasa naomba anijibu na anijibu kwa ufasaha, kwa sababu haya mambo sisi huwa tunayafatilia, nimepata taarifa kwamba walipewa laki nane madereva kwenda kufundishwa, lakini mwezi mzima mtu akakae Dar-es-salaam kwa kupata mafunzo kwa pesa hizi. Sasa anijibu vizuri, maana hapa kuna hamsini na ngapi milioni nilizisema jana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, anijibu na hili nitalifatilia.Tukishampitishia bajeti yake hapa, nihakikishiwe kwamba madereva na hasa dereva wake yeye na Naibu Waziri na hao wengine, maana hata hao hawajapelekwa kwenye mafunzo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na namshukuru sana Mhe. Asha Bakari Makame, kwa hoja yake. Ni kweli sikumjibu vya kutosha, lakini ni kwamba *course* ya madereva inaendelea, mwaka jana tumepeleka madereva sita, nadhani kama sikosei dereva wa Naibu Waziri alikuwemo, lakini ninachotaka kusema na mwaka huu na huyo dereva wangu anayempigania, nakushukuru sana Mhe. Asha, kwa kumtetea dereva wangu yumo katika orodha ya mwaka huu katika madereva 6 tutaopeleka kusomesha mwaka huu.Tulizuia kidogo, kwa sababu iliamuliwa madereva hawa tuwasomeshe hapa hapa Zanzibar, tutafungua *course* hapa Zanzibar, lakini kwa bahati mbaya tumechelewa na haikufunguliwa. Kwa hivyo, mwaka huu tutawapeleka madereva sita. Ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, napokea kwa shingo upande, lakini namuomba sana Mhe. Waziri, mimi nitalifuatilia hili na kwa kweli posho la laki nane mnampeleka Dar-es-salaam kukaa kule kutwa ukiigawa utapata elfu thalathini, Dar-es-salaam, ipi hiyo elfu thalathini mtu akodi hoteli, apate chakula, apate matumizi? Namuomba Mhe. Waziri na hivi ninahakikisha nitalifuatilia.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, hapa sikusudii kuzuia kifungu, lakini nilipochangia Mhe. Waziri, nilimuuliza, lakini hakunipa maelezo sasa, kwa sababu nimekosa kifungu cha mipango sera, naona nizuie hapa ili nipate maelezo. Nilizungumza kwamba kule Jambiani kuna nyumba za walimu ambazo ni mbovu sana na wanakaa walimu na wanalipa kodi, lakini sasa zile nyumba, kwa sababu ni mbovu wanalipa pesa, halafu wanaambiwa watengeneze wao na hizi nyumba ni za Wizara ya Elimu. Sasa nilitaka Wizara ya Elimu, Mhe. Waziri, anipe majibu kama zile watawatengezea wale watu waendelee kulipa kodi au wasamehewe kulipa kodi watengeneze nyumba. Sasa hakunipa majibu. Kwa hivyo, naomba anipe majibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Subeit, anipe muda kidogo baada ya bajeti hii, nikutane na wenzangu tulijadili suala hili ili tuamue kusamehe kulipa kodi au tusisamehe tupunguze au tusipunguze, hili suala kulitolea ufafanuzi, sasa hivi kidogo ni gumu, lakini mimi na wafanyakazi

wenzangu Katibu Mkuu, Naibu Waziri na kadhalika, tutakaa *emergently* tulizungumze na halafu nitampelekea jibu ikiwa kwa maandishi au kwa kuzungumza nae mwenyewe na kadhalika, lakini nitamjibu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, sikusudii kuwa nimuhangaishe Mhe. Waziri, lakini kwa sababu unajua tatizo ni moja, tukishapitisha bajeti hapa sasa, itakuwa kule kumpata tukakaa pamoja, inakuwa ni kazi kubwa, lakini hapa ni sawa sawa na mtu kama ng'ombe ana ndama wake ukamkamata atakuja mwilini. Kwa hivyo, hapa ninajua atakuja mwilini. Kwa hivyo, madam watendaji wake wapo, basi ningeomba washaurizane, lakini anipe jibu kama watawasamehe wale watengeneze nyumba au zitengenezwe nyumba waendelee kulipa kodi, lakini sasa tusiwabebeshe mizigo miwili, yaani kodi wanalipa na nyumba watengeneze. Kwa hivyo, ninaomba anisaidie majibu Mhe. Waziri, sina nia ya kuwa nimuhangaishe sana mzee wangu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Subeit, Mhe. Waziri, amejibu kwamba hilo kulitolea maamuzi hapa si jambo rahisi, anachokiomba itakapomalizika bajeti yake, yeye akae na watendaji wake, halafu aweze kukujibu, kwa sababu suala lako linahusu kuhusu kusamehe kodi kama sijapotea. Kwa utaratibu huo, anaomba umuachie ili atakapomaliza bajeti, akae na watendaji wake, ndipo atoe maamuzi, yeye yuko mbele na watendaji wako nyuma, haya maamuzi yatatoka vipi ndugu yangu Subeit.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, bajeti *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu leo tunaipitisha, sasa naomba anambie bwana ee, tukipitisha bajeti, muwatilie wiki ngapi au muwatilie siku ngapi? Lakini hajanambia hivyo, kwa sababu tukimaliza tu pengine tukishapitisha bajeti, je, akija akinambia mwezi wa kumi na moja.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, mjibu Mhe,Subeit muda gani baada ya kupitishwa hiyo bajeti yako.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, sidhani kama utachukua muda wa miezi mitatu, sidhani, lakini sote tuko hapa hapa Unguja tukimaliza bajeti tu, tutakaa tutazungumza tutajibu.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilimtaka Mhe. Waziri, aje anambie katika kipindi hiki cha mwaka 2014/15 wamejipanga kuajiri walimu wangapi wa masomo ya Sayansi na masomo ya *Art*? Lakini jawabu hili sikulisikia kwenye majumuisho yake.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kweli sikumjibu na jibu ninalo si katika moyo wangu, lakini ninamuahidi hata siku mbili hazipiti nitampelekea kwa maandishi walimu wangapi tumeajiri, wa sayansi wangapi na wa *Art* wangapi.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa vijana wapo wananisikiliza naomba Mhe. Waziri, anipe jibu hapa ili vijana wasikie.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, suala lako ambalo umeliuliza linahitaji jawabu la kitakwimu na Mhe. Waziri, amesema hana takwimu sahihi kuweza kukupatia hapa. Ameomba umpe muda ili aweze kujibu kwa maandishi.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, basi naomba iwe hivyo alivyosema, lakini isifike siku mbili tatu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, siku mbili hazizidi nitampa jibu.

Kifungu 0701	Idara ya Utumishi na Uendeshaji Pamoja na marekebisho yake-	2,713,800,000
Kifungu 0702	Baraza la Elimu-	50,000,000
Kifungu 0703	Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar-	380,000,000
Kifungu 0801		

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilisema walimu wanakazi kubwa na mchango wao ni mkubwa katika kutoa elimu. Kuna posho za nauli shilingi 1700, baadae wanalipwa shilingi elfu moja na walimu wao wengine kudai uhamisho wakabaki huku mjini. Serikali inatoa kauli gani kuhusu posho hilo shilingi 1700, baada ya shilingi elfu moja walizokuwa wakiwapa mashamba.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kauli ni kwamba tutatoa posho lote kamilifu lililokubaliwa na serikali na kama wanapata posho dogo tutarekebisha.

Mhe. Jaku Hashim Ismail: Mhe. Mwenyekiti, ninarudia tena vile vile, msemo wangu ukishakuwepo mbele unakuwa rahisi kukubali lolote, anambie lini hao watu, mimi nimletee Ofisini kwake ili kuja kuwalipa hizo posho zao.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu anataka lini, nimwambie narejea tena kusema jamani, bajeti ni mwaka mzima tutafanya marekebisho ya walimu wote kuhusu posho la nauli. Tutawapitia mwalim mmoja mmoja, Skuli moja moja ambapo pana kasoro tutazirekebisha katika kipindi hiki cha bajeti. Lini nimwambie kama nimwambie kesho, kama keshokutwa nitadanganya, siwezi kudanganya, lakini tutalifanya suala hilo. Kama ameridhika aridhike hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, narejea tena, wala hapana jazba, walimu wanakazi ngumu, mwenyewe kakiri Mhe. Waziri na hiyo bajeti sio mwaka huu na huko miaka ya nyuma, ndio hivyo hivyo wanapewa shilingi elfu moja. Tunawajali vipi walimu?

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee, walimu wenyewe wameshasikia huko.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika hoja za mchango wangu ambazo bahati mbaya kwa sababu ya muda Mhe. Waziri, hakuwahi kuzitolea ufafanuzi nilipokuwa nikichangia pale suala la vitabu, ule wakati wake haujafika, nilitaka kuzungumzia suala ambalo nililitaja la idadi ya masomo katika Skuli za Msingi na nikatoa mfano, kwamba kwa mfumo wetu wa elimu unapokuwa na masomo 13 kwa mwanafunzi wa darasa la tano, kwa hakika humsaidii na ni kinyume na taratibu za nchi nyengine za ulimwengu, tunaendelea kuongeza tu idadi ya masomo bila ya kuzingatia umri na uwezo wa wanafunzi wa kuweza kusimamia masomo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hili Mhe. Waziri, hakuwahi kulitolea kauli kama atalifanyia kazi kama wanao mpango wa kuyapitia tena kupunguza bei ya masomo, kwa sababu sisi pia tumesoma, *primary* hatukuwa na masomo mengi kama hivi. Nilikuwa naomba maelezo ya Mhe. Waziri, masomo 13 katika skuli moja na hii sina hakika kama ni Skuli zangu tu Mji Mkongwe baadhi ya Skuli ambazo ndio nimewahi kuwauliza walimu wake ama ndio ilivyo Zanzibar nzima, lakini labda ataweza kunisaidia wana mpango gani juu ya hilo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa na namuomba radhi Mhe. Jussa, sikuwahi kulijibu swali hili kwamba masomo ni mengi na ameyataja masomo, ninafikiri kumi na mbili, kumi na tatu ni mengi sana. Ninamuahidi Mhe. Jussa, kwa sababu hili somo moja la Sayansi Kimu limeondolewa, badala yake linasomeshwa kuna vifungu vitatu vya Sayansi Kimu vilivyochanganyishwa. Sasa ndio maana yakaongezeka. Sasa suala la kuirejesha tena Sayansi Kimu kama ilivyokuwa zamani au kuzungumza vyengine kuyapunguza, hilo nakubali kwamba kweli sikumjibu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kulitoa jawabu hilo kwamba tutakaa mapema iwezekanavyo kulijadili ili kuona tunaweza kulirejesha kama zamani au kuliacha libakie hivi hivi lilivyo, lakini tuamue masomo ni mengi au si mengi, lakini hoja hii ya masomo mengi tunayoyatoa ni hoja madhubuti, ni hoja ambayo imetoka sana katika Baraza hili. Kwa hivyo, ni wajibu wetu Wizara kulifanyia kazi. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na ili tuendelee katika hili sina haja ya kuvutana na Mhe. Waziri, kwa sababu kakubali *in principle*, mimi nitoe pendekezo dogo tu kwake na kwa uongozi wa Wizara. Nadhani kama tutakuwa na *consultant* katika mambo mengine mengi, basi elimu ndio roho ya Taifa lolote. Kwa hivyo, nadhani tusione tabu kama wataalamu tuliokuwa nao haya wanashindwa kuyamudu tutafute pia *consultant* kutoka nje. Bora kugharamika kupata *consultant,* maana Kamati tumeshaunda nyingi, mimi ninazikumbuka tangu miaka ya nyuma, waangalie kama kunahitajika, pengine tunaweza tukapata *consultant* mmoja tu akauangalia mfumo wetu wa elimu ulivyo, mahitaji ya dunia ya leo yanavyokwenda na akatusaidia kutupendekeza mgawiko wenyewe wa miaka, masomo yanayotakiwa katika elimu ya *primary* na *secondary* na vitu vyengine kama hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, nasema *in principle* kalikubali kwamba atakwenda kulifanyia kazi ili kulipatia ufumbuzi nampa hoja hiyo tu kwamba katika kulifanyia kazi azigatie na ushauri kama wataalamu kidogo wanatushinda tupate *consultant* walitazame. Mimi naamini kuna baadhi ya nchi washirika tukiwaomba kwa suala

kubwa kama hili na elimu ni sekta moja ambayo imesaidiwa sana, basi kuna uwezekano mkubwa sana kupata *consultant* pengine hata tusimlipie sisi, akaja akaangalia mfumo wetu wa elimu, masomo yanavyosomeshwa, uwezo wa wanafunzi wetu na kusaidia katika hili. Baada ya hayo, naomba tuendelee.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kupata fursa hii, jana nilipochangia kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na kama kawaida yangu nilisema kwamba naunga mkono mia kwa mia, lakini kulikuwa kuna mambo matatu ambayo niliyachangia, moja ni kuhusu jina la skuli hilo, sina wasi wasi nimekubaliana nae, lakini kuna mambo matatu mengine ambayo niliyaeleza na hili moja nitalipandishia tu kwa sasa hivi kwa sababu jibu hakunipa kuhusu Skuli ya Sebleni, nimejenga vyoo vinne na sasa hivi kuna tatizo la maji. Kwa hivyo, nilitaka aniahidi kwenye bajeti hii Mhe. Waziri, atanisaidia nini?

Mhe. Mwenyekiti, jengine vile vile, kuna madarasa matatu Kilimahewa "A"…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hoja yako iwe moja, sio mbili, naomba ajibu hiyo Mhe. Waziri, ambayo umeitoa sasa hivi.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka nimpe yote mawili na hilo…

Mhe. Mwenyekiti: Unao uhuru wa kutoa hoja moja, moja katoa Mhe. Jaku, moja Mhe. Jussa na wewe moja.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu maji…

Mhe. Mwenyekiti: Sawa atakujibu Mhe. Waziri. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nasikitika asije akaniambia nitayapeleka lini kama kesho, keshokutwa au mtondogoo, hilo nitashindwa kulijibu, lakini kama kumpelekea maji kwa sababu ya vyoo ameshajenga, hilo nalichukua na namuahidi kwamba nitalifanya. Nitazungumza na wenyewe wahusika wa Idara ya Maji ili wakatusaidie kutupelekea maji na Mhe. Waziri muhusika ananisikia nasema hivi, lakini kutoa ahadi kwamba nitapeleka maji kesho, kesho kutwa, mtondogoo siwezi, lakini nitalifanya.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, nimemsikia Mhe. Waziri na mimi wala sitegemei kwamba kwa leo na kesho, lakini kwa sababu ni haki yangu na wizara hii nimesema tokea mwanzo kwamba naunga mkono bajeti yake, lakini hata hiyo kwamba nimfuate sitaki, kwa sababu ataniambia ni yale yale kama alivyokwishakusema mwanzo kuwa hatoniambia ni lini, lakini angalau anipe moyo kuwa atatusaidia kwa sote, kwa sababu hili jambo la elimu ni jambo la jamii la wote na kama wizara ni lazima iwajibike. Kwa hivyo, naunga mkono nakubaliana na yeye na naomba tuendelee.

Kifungu 0801 Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi- 23,880,000,000
Kifungu 1201 Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala- 671,000,000
Kifungu 1402 Chuo cha Kiislamu-

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilionesha hofu yangu kuhusu kuuliwa kwa Vyuo vya Kiislamu na nilimueleza Mhe. Waziri, vyuo hivi vya Kiislamu ikiwezo Chuo cha Mazizini kilivyotoa watu wazuri wa kutusaidia na nilimueleza kama kwa kuwa watoto wetu mara nyingi muda wao ni mdogo wa kwenda vyuo vya Kurani, tulitegemea Chuo cha Kiislamu kitoe watu ambao watawasaidia watoto wetu kule maskuli kupata hii elimu ya Kiislamu, lakini kwa bahati mbaya sana sikumsikia Mhe. Waziri, kunipa jawabu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, samahani sana hebu anieleze tena.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, rejea tena Mhe. Waziri, hajakusikia vizuri.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nilisema wakati nachangia nilionesha hofu yangu kuhusu wizara kuua kwa Vyuo vya Kiislamu ikiwemo Chuo cha Mazizini na nilieleza Mhe. Waziri, vyuo hivi vya Kiislamu ikiwezo Chuo cha Mazizini kilivyotoa watu wazuri kwa umuhimu wa chuo kile na nilimuomba Mhe. Waziri, anieleze, ni kwa nini kwani chuo kile kilitoa watu wengi na sisi wa Zanzibar tulikitegemea kama tutapata watu

makini wakuwasomesha watoto wetu elimu ya dini, hasa ukizingatia muda wao ni mdogo wa kwenda kusoma katika vyuo vya Kurani, lakini hapa Mhe. Waziri, sikusikia kusema lolote kuhusu hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, jibu hoja ya Mjumbe, lakini sasa hivi tuko katika Chuo cha Kiislamu Pemba, yeye suala lake liko Mazizini Unguja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ndio ninalotaka kulijibu hilo la Mazizini…

Mhe. Mwenyekiti: Endelea kujibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: *Inshaallah*. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salma Mohammed Ali, ulipochangia niligusia kwamba wewe ni mchangiaji mmoja ambaye uko makini sana, mimi na mwenzangu Waziri wa Habari kila tukikaa hapa ukichangia, tunakuhusudu namna ya michango yako na mimi nitahakikisha nakupa jibu la Mazizini utosheke na ufurahike, hatukusudii kuua Uislamu, tunakusudia kuujenga Uislamu vizuri zaidi. Kwa taarifa yako Mhe. Salma, pengine ni mapema kutaja, lakini tuna nia yakuifanya Mazizini Chuo cha Kiislamu kwamba ni chuo kikuu, tuna nia hiyo. Pengine ni mapema sana kutaja, lakini tuna nia hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa nilizungumza wakati nachangia kwamba tumetia mkataba na wa Oman kujenga Chuo cha Kiislamu Mazizini, kujenga Msikiti mpya. Kwa bahati nzuri sasa hivi wako kwenye *site* wameshafika wanajenga, wameshakusanya vifaa. Nikasema katika ujenzi huo tutajenga msikiti mkubwa sana, una vyumba vya madarasa 6, una *laboratory* ya kompyuta, una maabara na kadhalika. Kwa hivyo, kama tunakwenda huko na tunaelekea huko Mhe. Waziri, huwezi kusema kwamba tunaiua dini ya Kiislamu, hatuuwi, tunaikuza na tunafanya juhudi zetu zote, mwaka huu tunamaliza hapo na tunakwenda Pemba Micheweni kumaliza ujenzi wa ukuta. Ahsante sana.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini vile vile, naomba niweke sawa, sikusema kama wataua Uislamu, nilisema kama wanaviua vyuo vya Kiislamu hii tofauti, lakini kwa sababu Mhe. Waziri, amenieleza dhamira yao waliyonayo na lengo lao. Kwa hiyo, mimi naunga mkono na naamini kile ambacho wa Zanzibar tulikitegemea kitokee pale Mhe. Waziri, ameshatuahidi kama bado ana lengo hilo na wataendelea kulifanyia kazi. Nashukuru.

Kifungu 1402 Chuo cha Kiislamu Pemba-	30,000,000
Kifungu 14003 Chuo cha Kiislamu Unguja-	30,000,000
Kifungu 1404 Taasisi ya Karume-	

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, wala sina nia katika kuzuia kifungu Mhe. Waziri, hapa ni ombi tu hiki chuo kutokana na hali yake ningekuomba ukafanya siku ukenda ukakiangalia kutokana na uchakavu wak, maabara na vifaa vya kufanyia kazi. Sina nia, huo ni ushauri kukuomba tu kwa heshima ya hali ya juu, ufanye siku ukakitembelee hiki chuo na kina upungufu wa walimu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naukubali ushauri wake.

Kifungu 1404 Taasisi ya Karume, Sayansi na Teknojia-	1,056,600,000
Kifungu 1405 Chuo cha Ualimu Benjamin Mkapa-	30,000,000
Kifungu 1406 Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar-	5,050,000,000
Kifungu 1407	

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, sina dhamira kwa sababu nimeshaiunga mkono, lakini sikupata ufafanuzi sasa nitamuomba Mhe. Waziri, anifafanulie katika kuchangia kwangu nilisema kwamba kulikuwa Chuo cha Amali kujengwa, lakini nikakosea nikasema Bwagamoyo kumbe Daya. Sasa naomba Mhe. Waziri, anielezee kitaanza lini au kitu gani kimekwama kwa sababu siku zimeshakuwa nyingi, ili nataka wananchi wa huko Mtambwe Daya wanisikie ili waweze kuwa na tamaa. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, nasema Chuo cha Mafunzo ya Amali Pemba, mchoro unakamilika mwezi wa August mwaka huu na michoro ikishakamilika tu, tukishaipasisha na tukishajadiliana, tutaikubali na tutaanza kazi ya ujenzi, lakini alipokuwa akichangia alisema mwanzo tuliamua

kukijenga Bwagamoyo, lakini mimi na Mwakilishi na wasaidizi wangu tulikwenda Pemba tukaiangalia Bwagamoyo na hilo eneo lilochaguliwa, tukagundua kwamba Bwagamoyo kuna mikarafuu mingi sana. Hivyo, itakuwa ni vigumu kukata mikarafuu tukajenga skuli wakati maeneo mengine yapo. Kwa hivyo, ndio maana tukenda katika eneo hilo tulilokusudia ambalo sasa michoro yake inamalizika mwezi wa August na halan ikimalizika michoro, tutaanza shughuli za ujenzi. Ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi kwa majawabu, kwa kweli yakutosheleza na mimi nitalifuatilia kama kawaida yangu, tuendelee.

Kifungu 1407 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar- 1,750,000,000
Kifungu 1408

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri tuko wawili, hoja yangu moja ni ya kukumbusha tu, si hoja kubwa, kwamba fungu hili ndio nililopendekeza zile fedha ambazo zilikatwa kule ambazo ni milioni 63,590,000 kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na 460,000,000 kwenye Idara ya Utumishi na Uendeshaji ambayo jumla itakuwa 523,590,000 posho la kufundisha nije hapa na hiyo maana yake itatupa jumla ya bilioni 9,315,990,000 ukiziongezea hapa, nadhani Mhe. Waziri, sasa atapata *target* yake alikuwa anataka kusomesha wanafunzi wote waliokuwa wanataka kuwasomesha.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hasa niliyoisimamia ni kwamba nilipochangia nilizungumzia pia suala kucheleweshwa kuingiziwa fedha wanafunzi wetu wanaosoma na nikasema sisi wenyewe tumepitia huko katika jambo ambalo mwanafunzi akiwa katika elimu ya juu halihitaji ni kuanza kushughulika atalipa vipi, atasimamishwa lini na haya yanatokezea. Hata Chuo Kikuu cha Taifa kinawafanyia hivyo wanafunzi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, nilikuwa nasema kwamba nilikuwa nataka kauli ya serikali, kuna wanafunzi kwa mfano *University of Zanzibar* ya Tunguu, mpaka hivi tunavyozungumza walikuwa hawajaingiziwa fedha ya posho ya huduma za kimasomo na huduma za kimasomo zinaweza kufanya wao wakaweza kusoma vizuri na wakatafuta vifaa wanavyohitaji. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kauli ya serikali suala hili litamalizwa lini? Kwamba fedha tunaidhinisha na tunaambiwa katika *first priority* za bajeti hizi ni masuala ya elimu na afya, kwa nini kunakuwa na ucheleweshaji mkubwa wa kuwaingizia fedha wanafunzi wetu wanaosoma katika elimu ya juu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kama tulikuwa tunachelewesha, ni bahati mbaya sana, si dhamira yetu. Tunawaheshimu na tunawapenda sana wanafunzi wetu. Jana tulilizungumza suala hili na tukakubaliana, nikathibitishiwa kabisa kwamba hiyo ilikuwa ni bahati mbaya na suala hili litarekebishwa na kama halikurekebishwa ili kuanzia mwaka huu kusiwe na ucheleweshaji wa kulipa maposho ya mkopo wa wanafunzi. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naamini *Inshaallah* kwa mwaka huu baada ya kuwaongezea fungu hilo nililowaongezea itakuwa mambo mazuri, lakini naomba kwa mwaka huu tunaomaliza nao ambao uko mwishoni, tumebakisha siku kadhaa kabla ya kufika mwisho wa June ambao ndio mwisho wa mwaka wa fedha, nilikuwa naomba kauli ya waziri au kauli ya serikali kwamba kwa wale ambao bado hawajamaliziwa sehemu zao za mikopo, anihakikishie kwamba watamaliziwa kabla ya mwisho wa June ili waweze kuendelea na masomo yao vizuri na mitihani yao wanayoendelea nayo ili waweze kufanya vizuri.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama ni kutoa kauli kwamba tutawakamilishia malipo yao kabla ya mwezi wa June kumalizika na-*hesitate* kidogo, lakini ninalokuwa na ithibati nalo ni lile tulilolizungumza jana, na leo asubuhi saa mbili tumelizungumza tena na tumelikamilisha. Kama kulikuwa kuna ucheleweshaji ni bahati mbaya, sasa hivi tutawarekebishiwa na mahitaji yao yote tutayakamilisha, lakini kama hali itaruhusu kulipa kabla ya mwezi wa June tutafanya hivyo, kama haitaruhusu, basi nasema achukue ahadi yangu kwamba tutarekebisha, lakini si mwezi wa June.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, Mhe. Mjumbe anaulizia kwa haya yalikuwemo. Kwa hiyo, hizi siku chache zilizopita kwa mwaka huu tunaomaliza nao kama kuna madeni anataka kupata ithibati yatakamilika kabla ya kuingia kwa mwaka mpya, hicho ndicho alichokiomba Mhe. Mjumbe.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Jussa, asinibane kiasi hicho, yeye akubali kwamba nitakamilisha, hivyo anavyotaka na ilivyotaka serikali na ilivyotaka Jumuiya ya watu na walivyotaka wananchi na kadhalika. Nimethibitisha nitafanya marekebisho, lakini tena kusema ikiwezekana kabla ya June nitafanya, haikuwezekana, Mhe. Waziri wa Fedha kanyamaza kimya, maana yake haiwezekani hiyo. Ingekuwa inawezekana kulipa kabla ya June, Mhe. Waziri, angekuwa ameshasimama, lakini haiwezekani hivyo, lakini tutafanya na tutalipa. Namuomba Mhe. Jussa, anikubalie.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida katika masuala haya na serikali, mawaziri wote ni mashahidi, naweza kuwa mkaidi katika baadhi ya maeneo mengine, si katika maeneo haya, lakini katika hili nilichokuwa nasema alivyokuwa akinijibu Mhe. Waziri, kasema kwamba ni kwa bahati mbaya kama imetokezea hivyo, sasa mimi ufahamu wangu ukisema kwa bahati mbaya ni kwamba fedha hizi zitakuwa zipo, lakini pengine kumetokezea matatizo katika kuziingiza na ukishachukua *commitment* ya mwanafunzi kumpa mkopo, maana yake anakitegemea kitu kile aweze kusoma, aweze kufanya mitihani yake vizuri na hawa ndio keshokutwa hizo nafasi watakuja kukaa wao huko, tunahitaji kuwatengezea mazingira mazuri na huku vile vile watakuja kukaa wengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, nilikuwa nasema, ndio maana nilikuwa nataka *commitment* ya kurekebisha kwa jumla kama ni sera sina tatizo, nilichokuwa nakitaka mimi kwa mwaka huu unaomalizika, wale ambao bado wana bakaa zao hawajaingiziwa na wengine wako katika mitihani wanazihitaji fedha hizo, kwa nini serikali ione tabu kunihakikishia kwamba hawa ichukue *commitment* itawaingizia pesa zao ili waweze kumaliza masomo yao vizuri kwa mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, naliuliza hili, kwa sababu ya hoja yangu kwamba nahofia kwa utaratibu wa Wizara ya Fedha au wa serikali ikifika mwisho wa Juni, kama fedha hazikutumika, zinarejeshwa Hazina, ndio maana nikataka hii kauli ya serikali katika hili.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemfahamu vizuri sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu na nimemfahamu vizuri sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Nataka niseme kwamba namuomba sana Mhe. Ismail Jussa, atuachie Wizara ya Fedha na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tutakaa tuweze kuangalia, kama kuna fedha ambayo imeshatoka, nasema tena narudia, kama kuna fedha ambayo imeshatoka kwa ajili ya mikopo na kama kuna wanafunzi ambao wanastahiki kupewa mikopo yao katika kipindi hiki, basi tutalisimamia hilo ili waweze kupata fedha hizo, lakini kama kuna fedha ambayo haijatoka na wapo wanafunzi ambao wanastahiki kupata mikopo yao katika kipindi hiki, tutaangalia tutakachokuwanacho na tuweze kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe Ismail Jussa, kama alivyosema Mhe. Waziri, *commitment* ya moja kwa moja itakuwa ngumu mpaka tuweze kuiangalia hasa mtiririko mzima wa pesa na idadi ya wanafunzi ambao wanadai na kiwango ambacho kimesalia na uwezo wetu wa ndani, lakini kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa, mimi nakubaliana naye kabisa kama mwanafunzi amekopa kiwango fulani ana tamaa kwamba kiwango kile atakipata katika kipindi fulani.

Mimi namuomba sana atuachie tutakaa na wenzetu hapa tutamtafuta Katibu Mkuu wangu na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Mkurugenzi wa mikopo, nadhani kati ya siku mbili hizi, kesho na keshokutwa niweze kukaa nao pamoja na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali tuweze kuona tunafanye katika huu muda ambao umetajwa, atuachie kidogo tulifanyie kazi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru, nataka niamini kwamba serikali italifanyia kazi suala hili, naomba tu katika huko kufuatilia alikosema Mhe. Waziri wa Fedha, kwa sababu walionileta lalamiko *specifically* hasa ni wanafunzi wa *Zanzibar University* ya Tunguu, inawezekana wako wengine, lakini wao hawakuweza kutufikia. Nataka niombe anapofuatilia aangalie *specifically* wanafunzi ambao waliidhinishiwa mikopo ambao ni wa *Zanzibar University*. Baada ya kusema hayo, nasema tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza katika kujenga hoja yangu, nataka nimshukuru Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe kwa wizara hii au kitengo hiki kuongeza fungu la shilingi 523 milioni. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Waziri, hoja yangu sasa hivi itakuwa rahisi kwake kama maji yanateremka tu. Serikali yoyote duniani haiwezi kupiga hatua yoyote, bila ya kuwa na elimu, mwaka jana wanafunzi 1,410 wa elimu ya juu, mwaka huu wamechukua wanafunzi 1,000, naona hakuna sababu tena ya kuzuwia fungu hili. Kwa kweli nikuombe sana Mhe. Waziri, ili tuendelee hapa kidogo nitakuwa mkaidi maana hakuna sababu tena ya kuja kunizuia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, njoo kwenye hoja, sasa hakuna tena maelezo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu wanafunzi 1,000 ni kidogo, mwaka jana 1,410 na mwaka huu unaokuja wataongezeka tu wanafunzi, ndio nikasema serikali inafanya masihara au mzaha na pesa zishaingizwa hivi sasa, nataka wanafunzi baada ya 1,410 waliokuwa mwaka jana, tufike angalau 1,500, hoja yangu iko hapo hakuna sababu ya msingi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nalikataa tamko lake Mhe. Jaku Hashim Ayoub, moja kwa moja la kwamba serikali inafanya mzaha, serikali iko *serious* na waziri wa serikali yuko *serious* na ndio maana nikakubali kukata pua kuunga wajihi. Sasa hili tamko la serikali linafanya mzaha, lakini naona suala hili kama tushalimaliza kwa sababu nimekubali kuwa pesa zitolewe zitiwe katika mikopo na tumerudi pale pale, sasa hivi kwenye shilingi milioni tisa na kitu kidogo badala ya shilingi milioni nane. Sasa mimi sikumfahamu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, labda anieleze tena.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, tayari Mhe. Waziri, ameridhia hoja ambayo ameitoa Mhe. Ismail Jussa Ladhu na tayari hizo pesa zimekubalika zirudi katika sehemu ya mikopo. Vile vile, serikali iko *serious* katika masuala yake, kama una la ziada.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka atoe kauli mwaka jana walikuwa wanafunzi 1,410, kitabu hiki, mwaka huu 1,000 na pesa zishaongezeka, wanafunzi wangapi wataongezeka? Kiswahili chepesi tu hicho, ndio nikasema tunafanya mzaha hatutaki wanafunzi wasome, ikiwa mwaka jana 1,410, mwaka huu 1,000, mwakani wataongezeka tu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sikuyafahamu kwa hicho alichokitaka cha papo kwa papo, nimtolee sasa hivi *figure* ya wanafunzi, kwa sababu pesa zimeongezeka badala ya wanafunzi 1,000, tutatoa wanafunzi wangapi? Hilo kama yeye anaweza kufanya hesabu haraka haraka akanipa idadi tutaweza kufanya, lakini si tumeongeza na tumerudia kwenye shilingi milioni tisa, sasa tatizo liko wapi? Mimi naona hakuna haja hapa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu mimi pesa zimeongezeka *total* ya wanafunzi inabidi iongezeke, ndio hoja yangu, shilingi 523 milioni si pesa kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo mazuri ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, naomba nielezee kidogo maelezo ya ziada kutokana na maelezo ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Kwa kuwa kuna ongezeko la fedha, maana yake kutakuwa na ongezeko la wanafunzi na mambo haya yana utaratibu wake, watarudi wizarani na watayapanga vizuri kutokana na hicho kilichoongezeka na kwa sababu lishawekwa sharti kwamba zitumike kwa sababu kadhaa.

Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub, akubaliae na maelezo ya waziri ili tuendelee, kwa sababu kwa vyovyote vile, si rahisi kwa Mhe. Waziri sasa kufanya mahesabu hapa, kupanga kuna taratibu zake katika kupanga. Tukubaliane kwamba wataongezeka wanafunzi kutokana na ongezeko la fedha ambazo wamekubaliana kuongeza. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri mwakani tutaripotiwa wanafunzi waliyoongezeka tuendelee.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza shughuli iliyo mbele yetu na kwa kuwa tuna bajeti muhimu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kwa kuamini kwamba Waheshimiwa Wajumbe, watajitahidi tuweze kumaliza shughuli hii katika nusu saa ama zaidi. Hivyo, niliombe Baraza lako tukufu liruhusu kuweka Kanuni ya muda kando ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tuwahoji wanaokubaliana na hoja ya kuongeza muda wanyooshe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Kifungu 1408 Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu-	Pamoja na marekebisho yake	8,792,400,000
Kifungu 1409 Baraza la Mitihani Zanzibar-		1,590,000,000
Kifungu 1410 Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu-		86,000,000
Kifungu 1411		

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba serikali inisikilize kwa umakini sana, kote nimeridhia tumefanya marekebisho na tumepita. Taasisi ya Elimu ndio inayohusika pamoja na mambo mengine na kusimamia utungaji wa vitabu.

Mhe. Mwenyekiti, nilitoa hoja nashukuru Mhe. Waziri, kakubaliana na mimi kayathibitisha niliyoyasema kwamba sikuzua kuwa vitabu hivi ni uoza mtupu na hivi ndivyo vinavyotumika kuwatayarisha wanafunzi wetu kwenda mbele, halafu baadae tunalalamika matokeo ya mitihani wakati Kiengereza kinachosomeshwa ndio hiki kwamba; "*get ready to a game, a man kick the ball very nice where goalkeeper jumps different sizes"*.Hiki ndio Kiengereza wanachosomeshwa wanafunzi wetu, hiki ni *Book Four* na mifano mingine.

Mhe. Mwenyekiti, hiki kimoja kina makosa hayapungui 200 na hivyo hivyo vyegine. Kama nilivyosema hahitaji mwandishi makini, hasa hawezi kujiandika hata jina lake akaandika Edi's, mwandishi makini anajua *standard* ya uandishi pamoja na kuandika jina lake kama lilivyo. Huo ndio msingi uliotufikisha hapa, tunalalamikia kuhusu mitihani inaturejesha nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri nimesema peke yangu, nataka maelezo mawili kutoka kwa Mhe. Waziri. Moja kasema tusamehe, lakini hii kusamehe kila mwaka, ndio inatufikisha hapa, ningelisamehe ingekuwa hoja hii nimeileta leo, lakini hoja hii niliileta mwaka juzi, bila ya vitabu nikasema tu, nikamwambia Mhe. Waziri, akitizame kitengo chao kinachosimamia haya, kuna harufu ya ufisadi, kwamba upitishwaji wa nani atunge kitabu na nani apewe *tender* ya kuchapisha, unakwenda kwa misingi ya watu kupata *commission* zao, sio katika misingi ya uadilifu matokeo ndio haya. Nilisema siku moja katika mchango wangu nilipotaja kitabu cha Kenya *"It is our time to eat*" ukiruhusu ufisadi ukaenea kila sekta ya maisha itaathirika, hapa roho ya Taifa ni elimu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, katoa hoja mbili; moja kasema tusamehe, pili anasema vitaandikwa upya. Najiuliza vitaandikwa upya kwa bajeti ipi? Ndio suala langu la kwanza hilo. Kwa sababu katika hotuba yake Mhe. Waziri, kwenye ukurasa wa 47 na 48, ukurasa wa 47, taasisi ya elimu inaripoti kuchapishwa vitabu hivi, ukurasa wa 48, unasema kuwa mwaka huu vitachapishwa vitabu vyengine. Sasa kwa madarasa ya tano na sita, hivi *book one to four* vishamaliza, sasa hii fedha ya kuchapishwa upya inatoka wapi?

Mhe. Mwenyekiti, pili, hawa waliotutia hasara hii na hasara sio fedha tu, hasara kubwa zaidi kuwapotosha watoto wetu na kuwajengea msingi mbovu, hawa tuwaache tu? Ndio maana nikasema serikali isikilize kwa makini, hili nitadinda hapa mpaka nipate kauli ya serikali, kwamba hawa wote waliohusika na kuvipitisha hivi na Mkuu wa Taasisi hii, wawajibike, wajiuzulu na wapatikane watu wapya kufanya kazi hii. Kama hakuna kuchukua dhamana kwa makosa wanayoyafanya, kila siku makosa yataendelea kufanyika. Kwa hivyo, niambiwe kwanza hivyo vipya pesa zitatoka wapi? Lakini na waliotusababishia hasara ya fedha na hasara ya kuwatayarisha wanafunzi wetu katika msingi mbovu wawajibike. Hapa tupate kauli ya serikali, ndio tupitishe taasisi ya elimu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nimeiona *concern* ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu, na ninafurahi alinitaja kwamba nimeitolea ufafanuzi wa kutosha, inaonekana hakuridhika. Ombi langu la kusema tusameheane, amelikataa na sasa hivi anakuja na jipya kwamba wanaohusika wawajibike. Mimi nasema kama atakubali usemi wangu huu kwamba "kufanya kosa sio kosa, kurejea kosa ni kosa" na nime-*admit* kwamba kosa limefanywa na nikataja njia moja iliyosababisha kufanya kosa, ni kutumia walimu wa *primary school* kufanya

review ya vitabu hivi, lakini kama haitoshi vitabu hivi, vimepelekwa TAKUKURU kuiangalia ile *element* ya rushwa iliyotajwa huo mwaka juzi anayozungumza.Tunasubiri majibu ya TAKUKURU, tumepeleka zamani hatujapata majibu bado.

Mhe. Mwenyekiti, inaonekana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, hakuridhika na niliyomwambia, hakuyakubali sawa, amefika pahala kusema kwamba waliohusika wawajibike, basi Mhe. Rais, amemsikia na Katibu Mkuu Kiongozi anasikia watu hawa wapo wanatusaidia sana, wametutungia vitabu vingi vizuri, kwa bahati mbaya hivi vina makosa na wamevisaini kwa kukubali kwamba vitabu vizuri, lakini vina makosa, nakubali. Basi kama ni kuwajibisha kwanza tungojee ripoti ya TAKUKURU ije, halafu tutamshauri Mhe. Rais, kama anawawajibisha hawa walioandika vitabu hivi, waliopokea na wakatia saini, kama anamuwajibisha Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, tutasubiri matokeo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe, kama ni binadamu anatakiwa ayafikirie niliyoyasema, nilichukua *effort* maalum, kwanza nilisahau kulitaja suala hili, nikisha nikakumbuka nikachukua *effort* maalum kulirejea na nikalielezea vizuri vya kutosha kwa kiasi ya uwezo wangu nilionao. Sasa mimi namuachie mwenyewe aamue, lakini pia, namuachia Mwenyezi Mungu atuhukumu licha ya hukumu tutayoipata TAKUKURU, lakini na Mwenyezi Mungu namuachia atutolee ufafanuzi na tumalizie suala hili, lakini tunasema tunajiandaa kuandika vitabu vyengine, kuandika miongozo mingine ili wanafunzi wasikae bure na suala kama pesa tutazipata wapi? Sisi tunao wahisani wetu. Kama tulivyozoea kuombaomba tutaendelea kuombaomba. Mwenyezi Mungu atatujaalia tutazipata hizi pesa, tutafanya marekebisho, lakini suala la kusimamisha la kutaka watu wawajibike, namuomba sana arudishe kauli yake. Tumekubali makosa na tumekubali tutafanya marekebisho. Sina zaidi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimtoe wasiwasi Mhe. Waziri, sahibu yangu sana na yeye anajua hilo na katika hili ningeweza kusema kwamba Waziri awajibike, lakini sikusema hivyo na pengine katika nidhamu za uongozi inakubalika kubeba dhamana, lakini sikusema hivyo. Mimi nimesema *specifically* kwa hatua hii kwanza Wakuu wa Taasisi ya Elimu ambao ndio wenye dhamana hii na hawa wanaosimamia Kitengo cha Uandishi wa Vitabu wawajibishwe.Inawezekana pengine katika hawa mimi siwajui nani, lakini pengine mwalimu wangu. Sasa hapa hatuzungumzi mambo ya binafsi. Ukipewa dhamana, unatumikia Taifa na kama nilivyosema mambo haya tukiyaachia, ndio inakuja ile aliyosema Mhe. Rais "*business as usual"*. Kwamba ikiwa mtu anafanya makosa, halafu hachukuliwi hatua, kwa nini mwengine ajirekebishe?

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi ninachosema hatuwezi kulea uoza kama huu na kama alivyosema, kasema ni suala la binadamu. Ingelikuwa nimelianza leo, lakini suala hili kama nilivyosema na leo nimekuwa mkali kwa sababu nataka tutoe fundisho. Miaka minne tumestahamili, huu mwaka wa tano wa mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, tunachotarajia Wawakilishi si kazi ndogo kwenda kufanya utafiti wa mambo haya ukaja nayo hapa, wangeweza kuwa wanakuja wanarudi tu, sisi wengine tunaumisha vichwa kuja na mambo haya hapa kusaidia kufanya kazi tulizokuwa tumetumwa.Yule anayechukua mshahara mwisho wa mwezi autumikie. Kuna wengine wanatumika zaidi kuliko sisi, hawapati hata robo ya tunachokipata sisi. Sasa unapofanya kazi hii, unataka uone tija yake. Kwa hivyo, tunachotegemea kutoka serikali ni kwamba tunapotoa hoja nataka kutoa fundisho leo, kwamba serikali izichukue izifanyie kazi. Sasa mimi nilitegemea maadam mwaka juzi nimelileta na nikaanza kutoa indhari ningetegemea haya yasitokezee, lakini kwa sababu hayafanyiwi kazi tunakuwa wepesi wa kutoa kauli tunapotaka bajeti ipitishwe, ikishapitishwa bajeti yote tunayasahau na yanakuja haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, nikasema kwa hatua hii na namtoa wasiwasi kabisa sahibu yangu Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, sisemi Mhe. Waziri, awajibike, nasema Mkuu wa Taasisi ya Elimu Zanzibar na Kitengo kinachohusika na upitishaji wa vitabu hivi, hawa wawajibike. Sasa mimi kazi yangu kufikisha ujumbe, serikali ipo bahati mbaya, lakini Kiongozi wa Shughuli za Serikali hayupo hapa.Kanuni nataka kama sikuridhika nimeondosha shilingi Kiongozi wa Shughuli za Serikali anipe kauli hapa simuoni, lakini pengine kwa utaratibu wake atasimama mwengine mwenye kauli yake.Ninachotaka nipewe kauli kwamba hili litachukuliwa kama alivyosema Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mamlaka ya uteuzi pengine kwa Mkuu wa Taasisi, lakini naamini kwa wale wenye uongozi wa kitengo hichi, hawa hawateuliwi na Mhe. Rais. Kitengo ni dhamana yake mwenyewe Mhe. Waziri na *Management* yake na ninaisema tena na nimelisimamia hili kwa sababu sitaki kutaja skuli hapa, lakini kuna skuli ina Mwalimu Mkuu makini, nilimwambia Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (Ndugu

Abdalla Mzee) kwamba vitabu vina matatizo akavikataa katika skuli yake. Kuna skuli zimepiga marufuku vitabu hivi visiingie kwa sababu havina kiwango. Kwa hivyo, ninachosema mteule wa Mhe. Rais Mkuu wa Taasisi, sawa tumuachie Mhe. Rais, lakini wale ambao ni Wakuu wa Kitengo ambacho wapo chini ya dhamana yake Mhe. Waziri na watendaji wake, hawa anihakikishie kwamba wanachukuliwa hatua. Akinambia wamemsaidia sana, mimi nashangaa, kama kumsaidia ndio huku sijui wakiwa hawamsaidii wanafanya kazi gani? Nataka kauli ya serikali katika hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niendelee tena kumshukuru Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa maelezo yake ya kina na majibu yake mbali mbali ambayo yamesaidia sana hapa katika kuendeleza kuifikisha shughuli hii ya bajeti ya Wizara ya Elimu. Aidha, nimshukuru sana ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kweli amesema jambo kubwa na hata Mhe. Waziri, mwenyewe amelikubali kwamba ni jambo kubwa na la msingi. Nimpongeze kwa kazi kubwa anayoifanya Taasisi ambazo zinasaidia sana kuendesha shughuli zetu za serikali hasa hasa katika eneo hili la elimu ambalo ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwamba tumeliona tatizo, lipo tatizo na ni wajibu wetu tulirekebishe na ushauri wa Mhe. Ismail Jussa Ladhu ni mzuri sana, anataka tuchukue hatua ya msingi wenzetu watendaji na wengine wenye dhamana na sote wenye dhamana. Pale linapotokea kosa tuweze kurekebisha kwa wakati ili kuepuka makosa makubwa. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Jussa, akubaliane nae tulichukue jambo hili ili tukalifanyie kazi kwa upana wake, ili tutoe majibu sahihi yanayoendana na ushauri wake, jambo kama hili lisiweze kutokea. Ni kweli limeshatokea na limeshaweka athari, lakini namuomba tukubaliane tupitishe bajeti, Serikali itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba tunarekebisha kama alivyokwishaeleza Mhe. Waziri na hayo mengine baada ya kuyafanyia kazi kwa kina na kujua taathira na yote yaliyotokea ili hatua zinazofaa ziweze kuchukuliwa. Naomba sana tukubaliane nae tuendelee. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema lengo langu ni kufanya kazi niliyopewa na dhamana ya watu waliokwenda kukaa foleni tangu alfajiri kunipigia kura, naamini wamefanya hivyo kwa kila mtu hapa. Nimeipokea kwa heshima kauli ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na pia kauli ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Ninachokiomba kwamba serikali inapochukua ahadi ikazifanyie kazi ahadi zake inazotupa hapa chombo hiki kikubwa.Ni bahati mbaya tu kwamba sisi hatujaamua kuwa *serious* tu humu. Katika Mabaraza mengine, sasa hivi pangeruka kivumbi humu ndani, lakini tunaoneshana kistaarabu, huu ustaarabu mara nyengine ukizidi wanaoumia ni wananchi.Kama nilivyosema hawa wameshaharibiwa *future* yao. Kwa hivyo, ninachosema kwamba nakubali kama nilivyosema, kuna mamlaka ya uwajibishaji kwa maana ya Mhe. Rais aliyemteua, lakini kuna kitengo ambacho kipo chini ya Mhe. Waziri. Ni matumaini yangu kwamba yote yanataka kufanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niombe tena kama nilivyosema kule mwanzo na napendekeza tena. Kama tunajihisi hatujakuwa na watu hivi sasa, mimi naamini watu wapo, tunao watu kina Mwalim Mohammed Mgeni Ali, hapa wamepasi kwa Kiengereza.Wote wanamjua, Mhe. Ali Juma Shamhuna, anamjua. Hawa wangeweza kuazimwa wamestaafu kufanya kazi ya *editing* ya vitabu kama hivi kwamba kila kitu mpaka kikang'ang'aniwe na watu wao wenyewe kwa sababu tu kuna rizki mtu atapata. Kwa hivyo, mimi ninachosema wapo watu wanaweza kutafutwa ndani, la hatutaki hao nasema tena *British Council* wanaweza kuombwa kwa vitu kama hivi. *British Council* pia wakasaidia waandishi na hata kusaidia kuvipitia, lakini nasema hili ni suala *serious*. Kwa hivyo, naomba moja lifanywe liwekwe hili hili na hivi vitabu naomba viondolewe, kwa sababu mpaka hivi sasa ninavyozungumza vinauzwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hivi nimenunua *bookshop*, vimeandikwa *not for sale*, lakini vinauzwa, tunajua sote hali ilivyo.Mimi nimevinunua *bookshop* hivi, nikampa mtu aliyekuwa na dhamana yake alikuwa anavipitia, akavipitia. Kwa hiyo, kazi ambayo nimekuja kuisema hapa. Kwa hivyo, naomba viondolewe, lakini la pili, kama nilivyosema tuone hatua zinachukuliwa. La tatu kwamba watafutwe watu wa maana ndani ya nchi wapo hapa, lakini hata ikiwezekana kuomba msaada mimi nina hakika Ubalozi wa Uingereza, *British Council* wanaweza kutusaidia sana katika masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee kwa sasa.

Kifungu 1411 - Taasisi ya Elimu- 14,000,000

Kifungu 1601 - Idara ya Mafunzo ya Ualimu- 1,158,160,000
Kifungu 1701 - Idara ya Elimu Sekondari -

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, niligusia Skuli ya Sekondari ya Kiboje na niliwasilisha picha mbele yako Mhe. Mwenyekiti, hali ya skuli hii ambayo inaitwa sekondari, lakini skuli hiyo vile vile, madarasa haya yamepewa jina la Mhe. Rais Mstaafu *Alhaj* Dkt. Salmin Amour Juma.

Mhe. Mwenyekiti, nataka anihakikishie tu, kwa kuwa jina hili lipo la kiongozi na mabanda haya hata yule ng'ombe au mbuzi huwezi kumuweka ndani. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, anihakikishie mabanda haya lini ataweza kuyamaliza na kama anasema hawezi kuyamaliza, basi lile jina la Dkt. Salmin Amour Juma lililokuwepo katika banda lile ambalo mimi na wenzangu Wazanzibari kwa mchango mkubwa wa Mhe. Rais wetu Dkt. Salmin Amour akalitoe pale ili lisiwekwe jina lake au anihakikishie kwamba madarasa yale yatakuwa yametengenezwa kwa heshima ya Mhe. Rais Mstaafu Dkt. Salmin Amour.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine kauli za sahibu yangu zinanitisha kusema kwamba mabanda yale hayafai kulala hata mbuzi. Kuna banda la skuli jamani halifai kulaza hata mbuzi. Jana alisema halifai kulala hata mende, leo kidogo amelipa *promotion*, halifai kulala hata mbuzi. Tunakosa lugha nyengine ya kuzungumza kuliko kuzungumza hivi. Dkt. Salmin Amour ni mzee wetu, ni mlezi wetu, ni Mhe. Rais wetu tunamuamini. Tulisema tumezijenga skuli za jimbo lake nyingi sita na mbili nane. Tumezitia vikalio vyote. Tumemjengea katika jimbo lake skuli ya kileo ya mkopo wa Benki ya Dunia. Katika skuli 13 tumezijenga.Basi ni sawa tuwe hatuna shukrani ya kushukuriwa, potelea mbali, lakini basi ndio lugha yenyewe ya kutumia hii kwamba tunajenga mabanda hata mbuzi kulala hafai na hata mende kukaa hafai.

Mhe. Mwenyekiti, jamani kwanza lugha hii ungeikataa na wewe umenyamaza kimya na inazungumzwa upo, mara mbili, mara tatu imezungumzwa lugha hii. Kwenye Baraza hili imezungumzwa lugha hii ya kejeli.

Mhe. Mwenyekiti, tukiacha hapo, ndivyo tulivyozoea na tulivyofundishwa, silaumu, tutaendelea kusikiliza lugha hii. Tumepewa kazi ya kufanya ni pamoja na kustahamili maudhi. Mwenyezi Mungu ametupa moyo huo na ametupa umri huo na mimi nasema ahsante nakubali tumejenga banda la kulala mbuzi na *Inshaallah* penye uhai na uzima hatutofika kwenda kupachua hilo jina la Dkt. Salmin Amour, hilo silifanyi. Badala yake nitaijenga hii skuli kwa hadhi hiyo hiyo ya Dkt. Salmin. Halafu tutaamua tunapeleka watoto wanafunzi au tunapeleka ng'ombe na punda, lakini ahadi ninaitoa mwaka huu huu wa fedha na mimi nimepewa ari ati, nitafanya ari kubwa na nitakwenda juu chini kwa Mhe. Waziri wa Fedha. anitilie fedha tumalize skuli hii tuijenge kwa hadhi ya Dkt. Salmin ili tuwaweke hao wanafunzi wetu. Ahsante sana.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, unajua wakati mwengine unakuwa una uchungu na nchi na uchungu wa wananchi wenzangu wa jimbo langu na uchungu usiopingika, huo ndio ukweli na utabakia kuwa ukweli mabanda yale nasema tena hata njiwa mimi siwezi kumuweka. Kwa hivyo, nashukuru Mhe. Waziri, kwa majibu yake mazuri na anasema heshima ya Mhe. Rais Mstaafu Dkt. Salmin Amour ataiweka, ataitunza na ataitengeneza. Mimi namshukuru kwamba huyu Komandoo ni Mhe. Rais wetu, mpendwa wetu. Naomba tuendelee.

Kifungu 1701 - Idara ya Elimu Sekondari- 18,160,000,000
Kifungu 2001 - Idara ya Mipango na Sera Pemba-

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, mimi langu ni dogo sana. Nataka nianze kwa ule msemo wa Kiswahili, sijauzoea kuwa "kufanya kosa si kosa, kosa ni kurudia kosa". Kufanya kosa ni kosa, kurudia kosa ni kosa jengine.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia juu ya umalizwaji wa banda la Skuli ya Mahuduthi ambalo mwaka jana lilikuwepo kwenye mpango wa kuezekwa bahati mbaya halikuulizwa. Mara hii Mhe. Waziri, katika kujibu kasema hawezi akaweka ahadi, lakini mwaka jana lilikuwa lina ahadi, mara hii limetiwa kuwa litaezekwa, lakini Mhe. Waziri, kashindwa kusema kuwa litaezekwa au haliezekwi. Ningependa kujua kwa nini anashindwa kuweka ahadi wakati ambapo limetiwa katika mpango wa kuezekwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ahadi yangu iko pale pale mara tu bajeti hii ikishapita, tukishaomba na tukitiliwa pesa, pamoja na skuli nyengine, skuli hii tutaisaidia.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki nirudi mara kwa mara kunyanyuka, kukaa, kunyanyuka, kukaa, lakini Mhe. Waziri, asitumie neno "kusaidia". Kwa kuwa limo katika mpango, aseme tutafanya wajibu wetu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia niliona bado sijamaliza michangio yangu, nikamuandikia Mhe. Waziri, mchango mwengine kwa maandishi na nikamuomba Mhe. Waziri na nikamwambia kama hapa naomba majibu kwa sababu nitakuwa mkaidi sana. Sasa naomba Mhe. Waziri, aniambie kwa sababu hili nitakalolizungumza, hii inafika bajeti ya nne nalizungumza suala hili hili, lakini utekelezaji wake sijui unakwama wapi?

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Kiislam Micheweni kinahitaji kuwa na msikiti madhubuti. Chuo ni cha Kiislam, lakini miaka yote nazungumza kujengwa kwa msikiti Chuo cha Kiislam. Ameligusia Mhe. Waziri, kama kitajengwa Chuo cha Kiislam Mazizini, ikisha tutakwenda Micheweni, lakini kama kuna mtu asiyestahamili na anayezungumza suala lake likawa bado halijatekelezwa, basi mmoja ni mimi.Nimeanza na Mhe. Haroun Ali Suleiman, wakati ni Mhe. Waziri wa Elimu, suala hili la Chuo cha Kiislam Micheweni kujengwa msikiti. Nikaja na swahiba wangu Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban. Naomba anieleze Mhe. Waziri, huu msikiti hasa Chuo cha Kiislam Micheweni lini utajengwa? Maana nimeshaambiwa kila siku utajengwa, utajengwa, lini?

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nadhani suala la kujenga Misikiti haliingii katika bajeti yetu. Suala la kujenga Misikiti halimo katika bajeti yetu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.Nilimuahidi na naendelea kumuahidi tutashirikiana pamoja mimi na yeye na wengine wote wanaotaka fadhila za Kiislamu kuzungumza na Masheikhe na Maulamaa, kuwaambiwa kwamba kuna tatizo hili na hili, tusaidieni.

Mhe. Mwenyekiti, tuombe dua, basi Mwenyezi Mungu atujaalie tukizungumza na Masheikhe hawa, maneno yetu yawe *makubul*. Nina hakika tutaujenga Msikiti na watu wa Micheweni wataendelea kunikumbuka kwamba nilisema neno hili siku moja kwamba tutaujenga Msikiti. Hivi sasa tuna tatizo la kujenga uzio wa matofali Chuo cha Kiislamu, hicho hicho anachokizungumza cha Micheweni. Tuna tatizo la kurekebisha matatizo madogo madogo ya Chuo hicho hicho cha Micheweni. Tutaifanya kazi hiyo kadiri ya Mwenyezi Mungu atakavyoturuhusu na tukizipata pesa hizi. Kwa hivyo, siwezi kutoa ahadi ya kitu ambacho hakipo ndani ya mikono yangu na hakipo katika uwezo wangu wa kwenda kwa Mhe. Waziri wa Fedha, anipe pesa, hanipi pesa za kujenga Misikiti. Ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Waziri, kwa kusema ukweli, lakini tunapokuja humu Barazani tukitoa ahadi zetu, basi ninawaomba Waheshimiwa Mawaziri, watupe zile ahadi ambazo zina uhakika kwamba zitatekelezeka, kwa sababu kipindi nilichopita niliambiwa kwamba tayari wameshapata mfadhili kutoka Saud Arabia kuwa kitakwenda kujengwa Chuo cha Kiislamu Micheweni, utajengwa Msikiti. *Wallahi* nendani mukawatizame watoto wanasali ndani ya yale madarasa na pale pana wanafunzi wasiopungua zaidi ya watu mia sita na wote ni watoto wa Kiislamu. Pale hapana Msikiti, wanasali ndani ya darasa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti,....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba nikusaidie. Mhe. Waziri, alichokisema kitu ambacho hakikupaswa kuzungumzwa sasa hivi, alisema tayari kuna masuala anazungumzia ambayo wakati wake bado. Kuna ujenzi katika suala la Mhe. Salma wa Chuo cha Kiislamu cha Mazizini kitakapojengwa kitakuwa na Msikiti na madarasa manne au sita, amesema sita. Hapo hapo mambo kama hayo baadae yatafanyika Micheweni Pemba, lakini masuala haya wakati huu bado hayajatimia. Ndivyo nilivyomfahamu Mhe. Waziri, katika mazungumzo yake alipokuwa akijibu suala la Mhe. Salma. Sasa suala la ujenzi wa Misikiti ya kawaida ya kujengwa kwa ajili ya maeneo yetu ya kusalia. Suala hili halimo katika Wizara ya Elimu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza nieleweke mimi sizungumzi kuwajengea watu wa Micheweni vijijini mwao Misikiti, nazungumzia Chuo cha Kiislamu Micheweni, sizungumzii kujengewa Misikiti watu vijijini mwao. Nazungumzia Chuo cha Kiislamu na sasa hivi lile analolizungumza kisha kabadilisha, ananiambia wanazungumza na Masheikhe kwenda kujengwa. Kwa hivyo, bado jibu langu linalouliza, linauliza Chuo Kikuu cha Kiislamu Micheweni, sizungumzii vijijini.

Mhe. Mwenyekiti: Basi subiri upewe jawabu Chuo cha Kiislamu cha Micheweni kama kuna mpango huo wa serikali au laa. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo na Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kubwa sana.Ninapenda kumwambia Mhe. Subeit Khamis Faki, kwamba katika bajeti yangu ya mwaka huu wa fedha 2014/2015, tumetenga fedha za kumalizia ukuta wa uzio wa Chuo cha Kiislamu Micheweni na tumetenga fedha za kufanya marekebisho madogo madogo ya Chuo cha Kiislamu Micheweni. Akiniuliza lini tutafanya kazi hiyo, nitashindwa, lakini katika kipindi cha bajeti hii cha mwaka 2014/2015, tutafanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: *Inshaallah.* Mhe. Subeit Khamis Faki.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nasemaje bado ninarudia tena, mimi nimeshaahidiwa zaidi ya bajeti tatu hapa, kama Chuo cha Kiislamu Micheweni utajengwa Msikiti, lakini kila nikija nikiahidiwa, naahidiwa kama yule mtoto wa kuku, utanyonya kesho, utanyonya kesho. Sasa naomba nijibiwe kwa sababu anasema hayupo. hasa huo mpango wa kujengwa. Kwa mujibu wa maelezo yake anasema haupo hasa. Kwanza alisema kama wakimaliza Mazizini watakwenda Pemba. Sasa anasema haupo hasa ujenzi wa Msikiti pale Micheweni kwenye Chuo cha Kiislamu. Kwa hivyo, bado hajanipa jibu. Naomba anipe jibu la ujenzi wa Chuo cha Kiislamu Micheweni Msikiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Mawaziri, kuna yeyote anayetaka kusaidia kwenye hili. Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri hoja ya Mhe. Subeit Khamis Faki na nimesikiliza majibu aliyotolewa na Mhe. Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mimi ninataka niseme tu na hili sio kwa Mhe. Subeit Khamis Faki tu, kwa sisi sote tuliomo humu ndani na tulioko nje. Kupanga ni kuchagua na kulingana na hali yetu ya mapato hatuwezi tukafanya kila kitu kwa wakati mmoja.Kama alivyosema Mhe. Waziri na mimi ninataka niongezee. Kama nia ya kujenga ipo, basi fedha zitakapopatikana Mhe. Subeit, avute subra. Hali yetu kwa sasa kama alivyosema Mhe. Waziri wa Elimu, hataweza kutekeleza hayo, lakini kama nia ipo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inayoongozwa na Jemadari Mhe. Ali Juma Shamuhuna, basi fedha zikipatikana tutatekeleza hilo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka nimuombe tu avute subra. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Subeit Khamis Faki, unatakiwa na Mhe. Waziri wa Fedha, uvute subra katika hili.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia sana Mhe. Waziri wa Fedha, swahibu wangu, lakini serikali haina dini, lakini wafuasi wake wana dini. Unajua kama pale pahali pana watu mia sita na kile chuo kinaitwa Chuo cha Kiislamu, sikiliza hilo jina kwanza. Kwa maana hiyo Waislamu pale wanatakiwa wafanye ibada zao. Hivyo, kama kuna mambo yanayofanywa muhimu, hili ni moja la kupewa kipaumbele. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri wa Fedha, anipe ahadi tu ni lini watashughulikia suala hilo muhimu, kwa sababu ni jambo muhimu kweli kweli.Keshokutwa tunaingia kwenye mwezi wa Ramadhani, watu wapo pale wanataka kuabudu, wanakwenda kuabudu ndani ya madarasa.
Mhe. Mwenyekiti, ninasema hivi, kwa sababu nimeshapewa ahadi zaidi ya bajeti nne na kila bajeti inakuwa ahadi nzuri tu, huwa naridhika. Sasa leo imeshageuzwa kibao, hakuna hasa hiyo nia ya kutekelezewa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, una lolote la ziada.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Subeit Khamis Faki, ni rafiki yangu sana.Nilimuahidi nitamjengea kituo cha habari pale na hakuamini na nikamjengea kipo. Nilimuahidi nitamjengea skuli ya kisasa anipe eneo na nitamjengea. Katika skuli nne tutakazozipeleka Pemba, sita Unguja na nne Pemba. Skuli moja ni Micheweni kwa Mhe. Subeit.

Mhe. Mwenyekiti, hili la kujengewa Msikiti, mimi naona si tatizo kubwa. Aliyeahidi si mimi, maana hakuna pesa za bajeti za serikali unazoweza kuzitenga kujenga Msikiti. Ninakubali ni Chuo cha Kiislamu, kuna wanafunzi pale wa Kiislamu na sisi sote ni Waislamu.Hao wanafunzi waliopo na walimu na nyinyi wametenga sehemu ya kusalia na wanasali. Ninachoweza kukisema Mwenyezi Mungu akipenda na mimi sasa ninaahidi, nitajitahidi kuzungumza na wafadhili na wakubwa wote ninaowajua kutujengea huu Msikiti.Kama Msikiti wa Chuo cha Kiislamu Mazizini tena

wa kileo kabisa Mwenyezi Mungu atujaalie tubakie mpaka Msikiti huu umalize, tunaweza kuujenga au kujengewa, maana ninasema kujenga maana sisi tunachangia.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa nini utushinde wa Micheweni. Kama kuna jimbo nalipenda sana mimi ni Kaskazini Pemba, ni Jimbo la Micheweni. Kilio hichi nakisikiliza kwa makini sana. Mwenyezi Mungu akipenda nitakitekeleza, lakini Mhe. Subeit, ukiniuliza lini, sijui, mimi kwamba nilikupa ahadi kwamba nitakujengea Msikiti Micheweni, sijui. Mimi ninakumbuka ahadi iliyoitoa Chuo cha Habari, skuli na kadhalika, hizo ndizo ahadi nilizozitoa.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti,lakini ninatoa ahadi sasa nitawatafuta wafadhili kwa nguvu zangu zote wa Oman, Saud Arabia, Misri na kadhalika watujengee huu Msikiti. Hilo ndilo ninaloweza kulisema.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri. Mhe. Subeit, sasa naomba ukisaidie kiti na tukubaliane katika hili.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, naona nimuachie Mhe. Waziri, tuendelee kwa sababu jibu hasa la ahadi sijapata. Kwa sababu yeye atatafuta wafadhili, kuna kupata na kukosa, lakini serikali wenyewe ingetoa tamko ya kwamba tutajenga Msikiti ijapokuwa kama ni mdogo, basi ningejua kuwa kuna ahadi ya kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, basi tuendelee.

Kifungu 2001 Idara ya Mipango na Sera Pemba-	503,626,000.00
Kifungu 22001 Idara ya Utumishi na Uendeshaji Pemba-	1,469,958,000.00
Kifungu 2301 Idara ya Elimu Pemba-	6,622,694,000.00
Kifungu 2501 Idara ya Elimu ya Watu wa Wazima na Elimu Mbadala Pemba-	185,501,000.00
Kifungu 2801 Idara ya Mafunzo ya Ualimu Pemba-	761,790,000.00
Kifungu 2901 Idara ya Elimu Sekondari Pemba-	7,805,270,000.00
Kifungu 2902 Idara ya Teknolojia ya Habari-	350,600,000.00
Kifungu 3001 Idara ya Teknolojia ya Habari-	115,511,000.00
Jumla ya Fungu-	**86,201,500,000.00**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 23 - WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera, Mipango na Utafiti-	400,911,006,000.00
Kifungu 0801 Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi-	13,662,128,000.00
Kifungu 1201 Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala-	8,859,316,000.00
Jumla ya Fungu-	**27,432,450,000.00**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu pamoja na mabadiliko kidogo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja ilikubaliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa namna ambavyo mumenipa mashirikiano ya hali ya juu kabisa hadi kuiwezesha kupitisha bajeti hii ya makadirio na mapato kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kumuachia Mhe. Waziri, sasa akafanye kazi ya kutuendelezea elimu

katika nchi yetu, lakini kabla sijaahirisha Baraza hili wakati huu, naomba kutoa matangazo mawili ambayo yapo hapa. Tangazo la kwanza, tumepata wageni ambao wameingia si muda mrefu, wageni hawa ni jumla yao ni wawili, wanatoka Kampuni ya *Super House Limited* ya India, Jimbo la Utrapradesh.Wajumbe hao ni Mohamed Vishan ambaye ni meneja, naomba asimame na Ajay Kumar. Tunaomba wageni hao tuwatambue uwepo wao.

Waheshimiwa Wajumbe, lakini pia, kuna tangazo kwa Waheshimiwa Wajumbe, wote wa Baraza la Wawakilishi munatangaziwa kuwa kutakuwa na zoezi la upigaji picha kwa ajili ya *website* yetu ya Baraza. Zoezi hilo litafanyika kuanzia kesho tarehe 18/06/2014 hadi tarehe 23/06/2014, saa tatu za asubuhi. Kuanzia saa tatu asubuhi mpaka saa sita mchana katika Afisi za Huduma ya Baraza la Wawakilishi.Wajumbe wote munatakiwa kufika kwa ajili ya upatikanaji wa picha hizo. Ni suala muhimu sana tunasisitizwa. Baada ya hapo, ninachukua fursa hii kusitisha Baraza hili hadi saa 11.00 jioni ya leo. Ahsanteni.

(Saa 7:40 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2014/2015
Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu muumba mbingu na ardhi na mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima na uwezo kutukutanisha tena hapa leo hii, ili kujadili mambo muhimu ya maendeleo ya nchi. Tunamuomba atuongoze ili tuweze kutekeleza kazi hii kwa hekima na busara na atuwezeshe kufanikisha malengo yetu kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako lipokee, lijadili na hatimaye likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kama ilivyo kwenye vitabu vya bajeti vya wizara yangu na viambatanisho vyake vinavyogaiwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, ambayo vyote naomba viingie kwenye kumbukumbu za *Hansard.*

Mhe. Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein), kwa kuiongoza vyema nchi yetu.Uongozi wake uliojaa hekima na busara umesaidia sana kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na katika ustawi wa jamii wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kuchukua fursa hii pia ya kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais (Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad) na Makamu wa Pili wa Rais(Mhe. Balozi Seif Ali Iddi) kwa kutekeleza majukumu yao na kumshauri ipasavyo Mhe. Rais. Aidha, napenda kuwapongeza kutokana na juhudi wanazofanya katika kuyapatia ufumbuzi matatizo mbali mbali ya wananchi pamoja na kutetea haki zao.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, napenda kukupongeza wewe kwa umakini wako katika kuliongoza vyema Baraza la Wawakilishi. Pia, pongezi hizi ziende kwa Mhe.Spika mwenyewe na Wenyeviti wa Baraza lako kwa namna wanavyokusaidia katika kazi zako. Aidha, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari (Mhe. Mlinde Mabrouk Juma) pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii, kwa kutusaidia na kutushauri ipasavyo na kurahisisha utekelezaji wa majukumu yangu.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Gando kwa mashirikiano mazuri wanayonipa katika kutekeleza utumishi wangu kwao.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, ilikadiria kupata shilingi 10,215,458,134/= kwa kazi za kawaida na shilingi 510,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

Aidha, wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,522,580,000/= zinazokwenda Mfuko Mkuu wa serikali na shilingi 2,111,250,000/= zinazokusanywa na kutumiwa na taasisi husika.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya shilingi 6,841,986,973/= zilipatikana kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 67 na shilingi 267,400,207/= kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia. Aidha, wizara ilikusanya shilingi 1,487,410,284/= sawa na asilimia 98 zilizoingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 1,897,218,111/= sawa na asilimia 90 ambazo zimekusanywa na kutumiwa na taasisi za Wizara, (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1a hadi 1(d)).

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2013/2014

Utekelezaji Halisi wa Miradi kwa mwaka 2013/2014:

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara imetekeleza Miradi minne (4) ifuatayo:-

(i) Utengenezaji wa njia za kukimbilia za Uwanja wa Gombani

Mhe. Naibu Spika, lengo la mradi ni kuufanya Uwanja wa Gombani kuweza kukidhi viwango vya Kimataifa kwa kujenga "*base*" itakayotumika kuweka mpira wa kukimbilia (*tartan*).

Mhe. Naibu Spika, mradi huu ulipangiwa shilingi 100,000,000/= ambazo zingeweza kuweka msingi "*base*" utakaotumiwa kuweka mpira wa kukimbilia. Hadi kufikia Mei 2014 jumla ya shilingi 90,000,000/= zimepatikana katika mradi huu sawa na asilimia 90. Kazi zinazoendelea kufanyika ni pamoja na utoaji wa matangazo ya zabuni, tathmini ya kumpata mshauri mwelekezi, utayarishaji wa michoro, kutoa zabuni ya mjenzi wa msingi na kuanza kazi hiyo.

(ii) Uhifadhi wa sehemu za kihistoria na mambo ya kale:

Mhe. Naibu Spika, lengo la mradi ni kuwa na maeneo ya kihistoria yaliyo endelevu kwa maendeleo ya Utamaduni na Utalii. Hatua mahsusi ni kuweza kuyapima na kuweka mipaka baadhi ya maeneo ya uhifadhi na kuyapatia hati miliki, kutangaza na kuendeleza maeneno ya kihistoria, kuhifadhi mambo ya kale na sehemu za kihistoria, kukusanya, kusambaza na kuweka mabango ya maelezo katika maeneo ya kihistoria, kushajihisha jamii na kutangaza sehemu za kihistoria, kuanzisha maeneo mapya ya kihistoria na makumbusho mpya, kuwepo kwa maeneo bora ya kihistoria na mambo ya kale.

Mhe. Naibu Spika, mradi huu ulitengewa shilingi 230,000,000/= ambapo hadi kufikia Mei 2014 jumla ya shilingi 67,400,207/= ziliingizwa sawa na asilimia 29. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa choo katika chemba ya watumwa Mangapwani, utengenezaji wa kisima cha chini kwa chini Mangapwani, uungaji wa umeme katika chemba ya Watumwa Mangapwani, uwekaji wa nguzo za mipaka katika maeneo ya kihistoria ya Pete, Bungi, Unguja Ukuu, Chuini, Dunga na Shakani. Vile vile, maeneo saba (7) ya kihistoria ya Mangapwani, Mnarani, Kisima cha Chini kwa Chini, Chemba ya watumwa, Bi Khole, Kuumbi na Mwana Mpambe yamepiwa na kupatiwa hati miliki.Aidha, maeneo ya kihistoria ya Mkamandume na Msikiti Chooko yameendelezwa ili kuyaweka katika hali nzuri na kutumika kwa miaka mingi zaidi.

(iii) Uimarishaji wa Studio ya kurikodia Filamu na Muziki kwa kuipatia vifaa:

Mhe. Naibu Spika, lengo la mradi huu ni kununua vifaa vya kurikodia muziki na filamu kwa ajili ya Studio ya Rahaleo.Mradi huu katika hatua ya kwanza ulitengewa jumla ya shilingi 80,000,000/= na hadi kufikia Mei 2014 shilingi 80,000,000/= zimeingizwa sawa na asilimia100. Kazi inayoendelea ni ununuzi wa vifaa vilivyokusudiwa baada ya kufuata taratibu zote za manunuzi, vifaa hivyo ni *Sony xdcamex, Camera tripods na Track dolly, Camera cran, Lens fish eye, Digital video mixer, Digital audio mixer na Power amplifier* kwa ukamilishaji wa Studio. Hata hivyo, Wizara imeamua mradi huu kuumaliza kwa hatua zote mbili ndani ya kipindi hiki cha mwaka wa fedha.

(iv) Mradi wa ujenzi wa vituo vya kutoa taarifa za usalama:

Mhe. Naibu Spika, lengo la mradi huu ni kutoa msaada wa taarifa za utalii na kusimamia masuala ya usalama yanayohusiana na utalii. Hatua mahususi ya mradi ni kujenga kituo kimoja kwa awamu ya kwanza pamoja na kufanya ununuzi wa vifaa kwa kituo hicho.Fedha zilizotengwa kwa hatua ya kwanza ni shilingi 100,000,000/= ambazo hadi kufikia Mei 2014 shilingi 30,000,000/= zimeingizwa sawa na asilimia 30.Kazi iliyofanyika hadi sasa ni uchoraji wa ramani ya kituo pamoja na kuandaa gharama za mradi, kazi inayoendelea ni uandaaji wa "*software*" itakayounganisha taarifa za kiusalama za utalii.

MAENEO YA VIPAUMBELE VYA KISEKTA KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, wizara imeweza kujipangia maeneo muhimu ya utekelezaji kisekta na kuwa ni vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2014/2015, vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo:-

SEKTA YA HABARI

Mhe. Naibu Spika, mambo muhimu ambayo imejipangia katika Sekta ya Habari kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ni kama yafuatayo:-

i. Kuanzisha mitandao ya kijamii kwa ajili ya wananchi kupata habari kwa urahisi popote walipo kupitia simu na *internet*;

ii. Kutoa taaluma ya kutumia vifaa vya Teknolojia ya Utangazaji wa dijitali;

iii. Kuwapatia wananchi huduma bora za habari na kwa wakati kwa njia ya magazeti, redio na televisheni; na

iv. Kuimarisha huduma za habari na mawasiliano kwa kuipatia Sekta hii vitendea kazi vikiwemo gari na mapazia ya sinema.

SEKTA YA UTAMADUNI

Mhe. Naibu Spika, maeneo muhimu ambayo tumejiwekea kipaumbele katika Sekta ya Utamaduni kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ni kama yafuatayo:-

i. Kuhifadhi na kuimarisha maeneo ya kihistoria pamoja na kuyatangaza ndani na nje ya nchi;
ii. Kutangaza na kuendeleza Lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na usahihi wake ndani na nje ya Zanzibar;
iii. Kukuza kazi za sanaa pamoja na kuendeleza matamasha na maonesho ya filamu na muziki; na
iv. Kuwashajihisha wasanii kuitumia Studio ya Rahaleo kurekodia kazi zao ili waweze kunufaika na sanaa zao.

SEKTA YA UTALII

Mhe. Naibu Spika, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika sekta ya Utalii mwaka wa fedha 2014/2015 ni kama yafuatayo:-

i. Kubadilisha muelekeo wa sekta ya utalii Zanzibar ili iweze kuleta tija zaidi katika uchumi wa nchi;

ii. Kukijengea uwezo wa kitaalamu na kitaaluma Chuo cha Maendeleo ya Utalii (*ZIToD*) ili kutoa rasilimali watu kulingana na mahitaji ya soko la utalii; na

iii. Kujenga mazingira bora ya Hoteli ya Bwawani ili kukidhi kiwango cha Kimataifa na kuwavutia wageni wengi wa ndani na nje ya nchi.

SEKTA YA MICHEZO

Mhe. Naibu Spika, maeneo muhimu yaliyopewa kipaumbele katika Sekta ya Michezo mwaka wa fedha 2014/2015 ni kama yafuatayo:-

i. Kuimarisha miundombinu ya michezo iliyopo na kujenga njia ya kukimbilia katika Uwanja wa Gombani - Pemba;
ii. Kukamilisha mapitio ya Sera ya Michezo;na
iii. Kuviimarisha vilabu vya michezo kwa kuvipatia mafunzo na fursa za michezo ya majaribio ili kuviwezesha kushindana katika mashindano ya Kimataifa.

MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo imetengewa jumla ya shilingi 15,336,575,000/=. Fedha hizo ni pamoja na miradi iliyoibuliwa kwenye maabara ya utalii (*Tourism Laboratory*). Kati ya hizo shilingi 9,371,200,000/= kwa kazi za kawaida (Tafadhali angalia kiambatisho namba 2) na shilingi 400,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Katika kukuza Sekta ya Utalii nchini, Serikali imeanzisha Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Utalii (*Tourism Development Program*) ambayo imetokana na matokeo ya Maabara ya Utalii (*Tourism Lab*) yenye jumla ya shilingi 5,595,375,000/= inayohusisha Taasisi mbali mbali za Serikali na Sekta binafsi.

Mhe. Spika, aidha, wizara inakadiria kukusanya mapato ya shilingi 1,718,658,000/= fedha ambazo zitaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia, makusanyo ya shilingi 2,236,250,000/= ambazo taasisi za wizara hukusanya na zimeruhusiwa kutumia kwa ajili ya uendeshaji wa taasisi hizo.

MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, mbali na miradi iliyoibuliwa na Maabara ya Utalii, ipo miradi mengine itakayotekelezwa na wizara katika mwaka wa fedha 2014/2015. Miradi hiyo ni kama ifuatayo:

(i)Mradi wa ujenzi wa vituo vya kutoa taarifa za usalama:

Mhe. Naibu Spika, lengo la mradi huu ni kutoa msaada wa taarifa za utalii na kusimamia masuala ya usalama yanayohusu utalii. Hatua mahsusi ya mradi huu ni kuendelea kujenga vituo vya kutoa taarifa za usalama kwa watalii. Mradi huu umetengewa shilingi 250,000,000/=

(ii)Uhifadhi wa sehemu za kihistoria na mambo ya kale:

Mhe. Naibu Spika, lengo la mradi huu ni kuwa na maeneo ya kihistoria yaliyo endelevu kwa vizazi vya leo na vijavyo kwa maendeleo ya nchi. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na uhifadhi wa mambo ya kale na sehemu za kihistoria, kukusanya na kusambaza taarifa za kiakiolojia katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba, kuweka mabango yenye taarifa katika maeneo ya kihistoria, kuwepo maeneo bora ya kihistoria na mambo ya kale. Mradi huu unategemewa kuingiziwa jumla ya shilingi 150,000,000/=

TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 NA MALENGO YA MWAKA 2014/2015 KWA KILA TAASISI

Mhe. Naibu Spika, malengo tuliyotekeleza kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na tuliyopanga kutekeleza kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kiidara na taasisi zilizo chini ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi ni kusimamia shughuli zote za utawala, utumishi (rasilimali watu), maendeleo, wajibu na maslahi ya wafanyakazi wa Wizara pamoja na kusimamia udhibiti wa bajeti ya wizara. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kujenga mazingira bora ya kazi yatakayowezesha Wizara kufanya kazi kwa ufanisi;
ii. Kuwaongezea ujuzi na utaalamu watendaji kwa maendeleo ya Wizara; na
iii. Kuhakikisha kuwepo kwa mashirikiano ya uendeshaji na utawala ya Wizara.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, Idara hii imefanikiwa kutekeleza malengo yake ya mwaka wa fedha 2013/14 kama ifuatavyo:-

i. Katika kujenga mazingira bora ya kazi, Idara imesimamia na kuimarisha upatikanaji wa huduma mbali mbali za Ofisi ikiwemo mawasiliano ya *internet*, *fax* na simu za ndani za ofisini, ulipaji gharama za maji, umeme, ununuzi wa mafuta na vilainishaji pamoja na vitendea kazi. Vile vile, Idara imefanya matengenezo madogo madogo ya gari, kununua samani za Ofisi pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao.

ii. Katika kuwaongezea wafanyakazi ujuzi, utaalamu na maarifa, Idara imegharamia masomo kwa wafanyakazi 14, wanawake (8) na wanaume (6) kati ya hao wafanyakazi watatu (3) ni wa ngazi ya Shahada ya Pili (*Master*), watano (5) ni wa ngazi ya Shahada ya Kwanza na wanne (5) ni ngazi ya Stashahada (Diploma) na mmoja ngazi ya Astashada. Lengo ni kuwaongezea ujuzi, maarifa na ubunifu ambao utapelekea kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Mafunzo pia yametolewa kwa watendaji wa taasisi nyengine zilizomo katika wizara.(Tafadhali angalia kiambataniisho namba 3).

iii. Katika kujenga mashirikiano ya uendeshaji na utawala, Idara imefanya tathimini ya utendaji kazi kwa Taasisi, Idara na Vitengo vilivyomo kwenye Wizara Unguja na Pemba kwa lengo la kujua mafanikio na changamoto zilizomo na kubuniwa mbinu za kukabiliana nazo ili kuimarisha ufanisi katika kazi.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014. Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,099,322,218/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Mei 2014 imefanikiwa kupata shilingi 831,219,802/= sawa na asilimia 76.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imejipangia kutekeleza malengo makuu matatu ambayo ni;

Kuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi wenye ujuzi na utaalamu kwa kuwapatia wafanyakazi nafasi za masomo ndani na nje ya nchi ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika Wizara. Kuwa na mazingira bora ya kazi kwa kuipatia Wizara vitendea kazi vyenye ubora vitakayowezesha Wizara kufanya kazi kwa ufanisi.

Kuwa na mashirikiano mazuri na endelevu ya Uendeshaji na Utawala kwa kutembelea taasisi zilizo chini ya Wizara, kushiriki katika semina na mikutano ya Kitaifa na Kimataifa. Katika kutekeleza malengo hayo Idara imepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kuendelea kuwalipia masomo yao wafanyakazi sita (6) waliopo vyuoni pamoja na kuwapatia mafunzo wafanyakazi wengine watano (5) ambao wanatarajiwa kujiunga katika viwango tafauti vya masomo kama ifutavyo:- Shahada ya Kwanza fani ya Ugavi na Ununuzi mmoja (1), Shahada ya Kwanza ya *Computer Science* mmoja (1), Stashahada ya *Material Management* (1), Rasilimali Watu mmoja (1) na (1) Cheti katika Utunzaji Kumbukumbu;

ii. Kuwawezesha wafanyakazi sita (6) kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi katika nchi za nje;

iii. Kuwafanyia semina wafanyakazi wa Idara ili kupata uelewa zaidi juu ya masuala jinsia, njia za kujikinga na maambukizi mapya ya *VVU* na UKIMWI, afya na usalama kazini;

iv. Kuandaa mafunzo kwa wafanyakazi wa Wizara kuhusiana na matoleo mapya ya Sheria, Kanuni na Miongozo ya Utumishi Serikalini;na

v. Kuipatia Ofisi vitendea kazi bora na vya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, naomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,127,035,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kupanga, kutayarisha, kukagua, kuratibu na kutathmini mipango ya maendeleo ya Wizara, kupitia Sera, kufanya tafiti mbali mbali na kusimamia utekelezaji wake. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuwa na Sera na Mipango bora ya kisekta ya Wizara kwa maendeleo ya Wizara;
ii. Kuimarisha maendeleo ya Wizara kupitia matokeo sahihi ya tafiti;na
iii. Kuimarisha uwezo wa watendaji na utendaji kazi wa pamoja wa kisekta kwa maendeleo ya Wizara.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara hii imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Idara imeweza kuratibu mapitio ya Sera ya Michezo, Utalii na Mambo ya Kale ambazo hivi sasa matayarisho ya kukamilika kwake yanaendelea;

ii. Idara imewalipia wafanyakazi wake wawili mafunzo ya muda mrefu mmoja katika Shahada ya Kwanza ya Takwimu na mwengine Shahada ya Pili ya Usimamizi wa Miradi.Vile vile, Idara imewalipia wafanyakazi wawili waliohudhuria mafunzo ya muda mfupi nchini China;

iii. Idara imefuatilia na kutathmini Mipango na shughuli mbali mbali zinazotekelezwa ndani ya Wizara ikiwa ni pamoja na kuratibu, kutayarisha na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwa Kamati ya Baraza la Wawakilishi, pamoja na taarifa za utekelezaji wa malengo kwenye vikao vya pamoja vya Uongozi wa Wizara na Mh.Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

iv. Hatua ya pili ya utafiti wa maeneo ya kihistoria inaendelea kwa uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa zinazohusu maeneo maarufu ya kihistoria kama vile Msikiti wa Kizimkazi, Chwaka Tumbe na Kuumbi yanayotembelewa na watalii. Katika kufanya utafiti wa maendeleo ya sanaa takwimu za utafiti zilizokusanywa katika Mikoa miwili ya Unguja zimekusanywa na zimeanza kufanyiwa kufanyiwa uchambuzi; na

v. Idara imeratibu tafiti zilizofanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara kama vile utafiti wa utamaduni usioshikika na tayari umekamilika na kitabu kimeshachapishwa.Vile vile, Idara imeratibu utafiti wa majina ya viumbe vya baharini na mazingira yao na kazi hii bado inaendelea.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 157,800,000/= kwa matumizi Mengineyoyo na hadi kufikia Mei 2014 imefanikiwa kupata shilingi 30,479,600/= sawa na asilimia 19.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutekeleza malengo makuu matatu nayo ni:- Kuwa na Mipango bora ya kisekta na Sera kwa kutayarisha na kuzipitia Sera za Wizara. Kuwa na *"Data base"* ya takwimu sahihi ya taarifa zinazokusanywa na Wizara. Kuwa na wafanyakazi

wenye ujuzi na utaalamu katika fani ya Takwimu na Teknolojia ya Habari. Katika kutekeleza malengo hayo, Idara imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kusimamia matayarisho na mapitio ya Sera na Mipango ya kisekta kwa maendeleo ya Wizara,
ii. Kuimarisha maendeleo ya Wizara kupitia matokeo ya takwimu za tafiti zinazofanywa;
iii. Kufuatilia na kutathmini Mipango na shughuli mbali mbali zinazotekelezwa katika Wizara; na
iv. Kuendelea kuwalipia wafanyakazi wawili (2) waliopo masomoni pamoja na kumpatia mafunzo mfanyakazi mwengine mmoja (1) ambae anatarajiwa kujiunga na masomo katika kiwango cha Shahada ya Pili.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kufanikisha malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 kwa ufanisi, ninaiombea jumla ya shilingi 120,305,000/= kwa matumizi Mengineyo.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Ofisi Kuu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Pemba ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Wizara Kisiwani Pemba. Ofisi hii ni kiunganishi katika kuhakikisha majukumu, malengo na shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa upande wa Pemba. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Ofisi hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuhakikisha kuwa taasisi za Wizara zinashirikiana na kutoa huduma bora kwa jamii kwa maendeleo ya Wizara kwa upande wa Pemba; na
ii. Kujenga mazingira bora yatakayoiwezesha Ofisi Kuu Pemba kufanya kazi kwa ufanisi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, Ofisi Kuu imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

i. Ofisi imeratibu utayarishaji wa vipindi 36 ambavyo vilihusisha hatua za maendeleo kisiwani Pemba ambapo wananchi walishiriki kutoa maoni yao juu ya maendeleo makubwa yaliyofikiwa;
ii. Ofisi Kuu imeratibu shughuli za uendelezaji wa maeneo ya kihistoria ya Mkamandume na Msikiti Chooko ili kuyaweka katika hali nzuri na kutumika kwa miaka mingi zaidi;
iii. Ofisi Kuu imeratibu shughuli za uendelezaji wa Sekta ya Utalii kwa lengo la kuhimiza dhana ya utalii kwa wote ambapo Kamati za utalii za Wilaya zimeanzishwa ili kuhakikisha utalii unaendelezwa kwa maendeleo ya nchi;
iv. Ofisi Kuu imeratibu matengenezo ya Uwanja wa Michezo Gombani kwa kuezua na kuezeka paa pamoja na kuendelea kuupaka rangi ili kuuweka katika hali nzuri; na
v. Ofisi Kuu Pemba imeratibu ujenzi wa Jengo la Judo katika Uwanja wa Gombani Pemba kwa kushirikiana na Ubalozi wa Japan na Chama cha Judo Zanzibar, ambalo tayari limekamilika na kufunguliwa rasmi.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi Kuu Pemba iliidhinishiwa jumla ya shilingi 672,624,750/= kwa kazi za kawaida na shilingi 100,000,000/= kwa kazi za maendeleo na hadi kufikia Mei 2014 imefanikiwa kupata shilingi 468,645,750/= sawa na asilimia 70 kwa kazi za kawaida na shilingi 90,000,000/= sawa na asilimia 90 kwa kazi za maendeleo.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Ofisi hii imepanga kutekeleza malengo matatu nayo ni:- Kuwa na wafanyakazi wenye ujuzi na utaalamu kwa kuwapatia wafanyakazi nafasi za masomo ndani na nje ya nchi. Kuwa na Mipango bora ya kisekta na Sera kwa kutayarisha na kupitia Sera za Wizara, kuwa na "*Data base*" ya takwimu sahihi ya taarifa zinazokusanywa na Wizara. Kuwa na mashirikiano mazuri na taasisi za Wizara za Pemba kwa kutoa huduma bora na kujenga mazingira bora yatakayoiwezesha Ofisi Kuu Pemba kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Katika kutekeleza malengo Ofisi Kuu imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi (6) katika kada mbali mbali na kuimarisha mazingira bora ya wafanyakazi; na

ii. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na taasisi za Wizara zilizo chini ya Ofisi Kuu Pemba zikiwemo za uwekaji wa njia ya kukimbilia (*Running Track*) katika Uwanja wa Gombani na kufanya matengenezo madogo madogo ya Ofisi Kuu na Uwanja wa Gombani.

Mhe. Naibu Spika, ili Ofisi Kuu ya Wizara ya Habari,Utamaduni, Utalii na Michezo Pemba iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, naomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,278,161,000/= kwa kazi za kawaida.

SEKTA YA HABARI

Mhe. Naibu Spika, Sekta ya Habari imeundwa na taasisi tano ambazo ni Shirika la Utangazaji Zanzibar, Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti ya Serikali, Tume ya Utangazaji, Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui (*ZMUX*) na Chuo cha Uandishi wa Habari. Majukumu ya msingi ya taasisi hizi ni kuarifu, kuelimisha na kuburudisha jamii, kuratibu uchapishaji wa magazeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kusimamia vyombo vya utangazaji vya Serikali na vya binafsi na kutoa taaluma kwa waandishi wa habari.

SHIRIKA LA UTANGAZAJI

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Shirika ni kutoa habari, kuelimisha, kuburudisha na kuhamasisha jamii juu ya masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Shirika hili lilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kutayarisha vipindi vyenye kuvutia wasikilizaji na watazamaji wengi wa ndani na nje ya Zanzibar; na
ii. Kujenga mazingira bora ya kazi ili kuliwezesha Shirika kutoa huduma bora na zenye ufanisi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Utangazaji limefanikiwa kutekeleza malengo hayo kama ifuatavyo:-

i. Shirika limesimamia shughuli zake za kila siku za uendeshaji kwa kuipatia Studio vifaa vikiwemo kamera, dv *recoder*, kompyuta za *lap top* pamoja na matengenezo ya Studio kwa Unguja na Pemba;

ii. Katika kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Shirika limeandaa na kurusha hewani vipindi 450 vinavyoelezea maendeleo na mafanikio yaliyofikiwa tokea kuasisiwa kwa Mapinduzi ya Zanzibar. Vile vile, vipindi maalumu 20 vya kupinga unyanyasaji, vipindi 119 vya kutangaza dhana ya utalii kwa wote na vipindi 101 vyevye kuelezea mafanikio ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika kuleta maendeleo;

iii. Shirika limewapatia mafunzo wafanyakazi wake wanne (4) ngazi ya Shahada ya Pili na mafunzo ya muda mfupi ya Habari wafanyakazi 10 nchini China;

iv. Shirika limewapatia watendaji wake mafunzo ya utayarishaji wa vipindi vya redio na televisheni vinavyolingana na nadharia vya vyombo vya habari vya umma yaliyoendeshwa na Shirika la Utangazaji la Ujerumani (*DW).* Vile vile, Shirika la Utangazaji la Ujerumani (*DW*) limetoa mafunzo ya Uongozi wa Shirika kwa watendaji mbali mbali wa *ZBC;* na

v. Shirika limeanza kazi ya ujenzi wa Studio mbili za dijitali, moja *Karume House* na nyengine Mkoroshoni Pemba.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Shirika la Utangazaji liliidhinishiwa jumla ya shilingi 2,050,000,000 /= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Mei 2014 imefanikiwa kupata shilingi 1,607,749,741/= sawa na asilimia 78. Shirika lilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 280,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 227,101,390/= sawa na asilimia 81.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Shirika la Utangazaji limepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni:- Kuwa na mazingira bora ya upatikanaji wa habari kwa jamii kwa kuongeza ujuzi na utaalamu kwa watendaji wa vyombo vya habari na kuwapatia huduma muhimu wafanyakazi pamoja na kuwapatia vitendea kazi. Kuhakikisha vyombo vya habari vinatoa taarifa zilizo bora kwa kuandaa vipindi vitakavyovutia jamii na kujenga uhusiano mzuri wa Kitaifa na Kimataifa kuhusiana na masuala ya habari. Katika kutekeleza malengo hayo Shirika limejipangia shughuli zifuatazo:-

(i) Kuwapatia mafunzo watendaji 10 wa vyombo vya habari katika kuwaongezea ujuzi na utaalamu katika fani ya Ufundi, Utayarishaji Habari na Teknolojia ya Habari;
(ii) Kuandaa vipindi vipya na kuviimarisha vilivyopo ili kuwa na matangazo bora kwa wasikilizaji na watazamaji;
(iii) Kutoa taarifa sahihi na kwa wakati pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa vitendea kazi vilivyo bora kwa ajili ya kuondoa matatizo ya upokeaji habari;
(iv) Kuendeleza mahusiano na wadau mbali mbali wa sekta ya habari;
(v) Kuanzisha mitandao ya kijamii na kukamilisha muundo wa Shirika;
(vi) Kuweka utaratibu wa vipindi vya redio kupitia kwa msambazaji wa maudhui (*ZMUX*); na
(vii) Kumalizia ujenzi wa studio mbili za dijitali Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, ili Shirika la Utangazaji liweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2014/2015, naliombea liidhinishiwe jumla ya shilingi 1,814,536,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na kukusanya shilingi 300,000,000/=.

IDARA YA HABARI MAELEZO

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Idara ya Habari Maelezo ni kutoa elimu kwa maendeleo mijini na vijijini, kuimarisha uhusiano mzuri kati ya Serikali na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi, kutayarisha na kutoa vielelezo katika mfumo wa picha, sinema na majarida kuhusu shughuli za Serikali na kusimamia Sheria ya Habari Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuandaa na kuratibu mikutano ya waandishi wa habari kuhusiana na matukio mbali mbali Unguja na Pemba;
ii. Kuonesha sinema katika vijiji 18 Unguja na 12 Pemba;
iii. Kuweka picha za matukio muhimu kwenye mabango (*Display Boards*);
iv. Kufanya machapisho na ununuzi wa picha za viongozi wa kitaifa-Rais Kikwete 300 na Marehemu Mwalimu Nyerere 54; na
v. Kuifanyia marekebisho ya Sheria namba 5 ya Usajili wa Magazeti na Vijarida ya mwaka 1988.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kutekeleza malengo hayo kama ifuatavyo:-

i. Idara imefanya mikutano 40 ya waandishi wa habari ikiwemo inayohusiana na maendeleo yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Sheria za umiliki wa ardhi na elimu juu ya maambukizi ya ukimwi;

ii. Maonesho ya sinema yamefanyika katika vijiji 50 kuhusu elimu juu ya maradhi yasioambukiza yakiwemo kisukari, kansa na sindikizo la damu;
iii. Aidha Idara imeweka picha katika mabango yake yaliyopo Unguja na Pemba, pamoja na kusambaza taarifa na matukio muhimu katika Blog na ofisi za mabalozi wa Tanzania zilizopo nje ya nchi; na
iv. Idara imekamilisha kuifanyia marekebisho Sheria Na 5 ya Usajili wa Magazeti na Vijarida ya mwaka 1988 baada ya kufanya mikutano kadhaa na wadau wa habari kwa kutoa maoni yao juu ya marekebisho ya Sheria hiyo. Marekebisho hayo sasa yanaandaliwa kuwa mswada wa sheria ambao utawasilishwa katika ngazi zinazohusika.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014. Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 378,912,301/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Mei 2014 imefanikiwa kupata shilingi 216,317,830/= sawa na asilimia 57. Idara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 18,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 5,645,000/= sawa na asilimia 31.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Habari Maelezo imepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni:- Kuhakikisha wananchi wanapata taarifa muhimu kupitia njia za habari na mawasiliano, kusambaza taarifa katika ofisi za kibalozi, *Blog* na vyombo vya habari vya Serikali na binafsi na kuonesha sinema katika vijiji vya Unguja na Pemba. Kuwa na mazingira bora ya kazi kwa kuipatia ofisi vifaa vya kisasa vya kuhifadhia kumbukumbu, kufanya matengenezo ya jengo la ofisi na kuongeza ujuzi na utaalamu kwa wafanyakazi. Katika kutekeleza malengo hayo Idara imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kutoa taarifa katika ofisi za kibalozi, *Blog* na Vyombo vya Habari;
ii. Kuonesha sinema katika vijiji 100 vya Unguja na Pemba;
iii. Kuweka mapazia matatu ya kieletroniki katika maeneo yenye mkusanyiko wa watu kwa ajili ya kuonesha picha za maendeleo. Mapazia hayo mawili kwa Unguja na moja Pemba;
iv. Kuimarisha Idara kwa kuipatia vifaa vya kisasa ikiwa ni pamoja kununua mapazia ya kuoneshea sinema mjini na vijijini;
v. Kuwapatia mafunzo watendaji wa vyombo vya habari katika kuwaongezea ujuzi na utaalamu; na
vi. Kuwasilisha Rasimu ya marekebisho ya Sheria namba 5 ya vijarida na magazeti ya mwaka 1988 katika ngazi husika na baadae katika baraza lako Tukufu.

Mhe. Naibu Spika, ili kukamilisha vyema malengo ya Idara ya Habari Maelezo katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, naomba kuidhinishwa jumla ya shilingi 380,828,000/= kwa kazi za kawaida na kukusanya shillingi 19,000,000/=.

SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Shirika la Magazeti ya Serikali ni kusimamia uchapishaji wa magazeti ya Serikali ya Zanzibar, kuelimisha wananchi ili kukuza uelewa wao wa mambo, kutoa habari zenye kuhamasisha jamii na kushiriki kwenye harakati za maendeleo ya nchi.

Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Shirika la Magazeti ya Serikali lilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuchapisha magazeti ya kila siku;
ii. Kuchapisha magazeti ya kila wiki;
iii. Kusafirisha na kusambaza magazeti ndani na nje ya Zanzibar;
iv. Kufuatilia upatikanaji wa habari ndani na nje ya nchi pamoja na masoko mapya; na
v. Kufanya malipo ya '*hosting'* ya tovuti (*website*).

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, napenda kuliarifu Baraza lako kuwa, Shirika limeweza kutekeleza kwa kiasi kikubwa shughuli zake kwa mwaka 2013/2014 kama ifuatavyo:-

i. Shirika limekamilisha michoro ya ujenzi wa ofisi mpya na lipo katika hatua ya kukamilisha BoQ na "*Tender document*" kwa ajili ya ujenzi huo, ambao unategemewa kuanza mara zitakapopatikana fedha. Shirika la Magazeti ya Serikali linategemea kufanya ujenzi huo katika kiwanja chake kilichopo Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja;
ii. Katika kuwajengea uwezo wafanyakazi ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kuongeza uzalishaji, Shirika limeweza kuwasomesha wafanyakazi wake sita (6) katika ngazi mbali mbali ndani na nje ya nchi. Wafanyakazi hao wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi na wengine wanaendelea na masomo;
iii. Shirika limewapatia stahiki za likizo wafanyakazi wake. Pia Shirika lilimsaidia mfanyakazi wake mmoja gharama za matibabu nchini India;
iv. Shirika lilisambaza magazeti katika Mikoa ya Unguja, Pemba na Tanzania Bara; na
v. Malipo ya tovuti yamefanyika na tovuti imefunguliwa na inaitwa *www.magazetismz.com*.

Mhe. Naibu Spika, Shirika linapenda kuliarifu Baraza lako kuwa, Gazeti la Zanzibar Leo limeweza kuwafikia wasomaji wengi zaidi kwa kuongeza maeneo ya usambazaji katika baadhi ya mikoa ya Tanzania bara.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014. Shirika liliidhinishiwa jumla ya shilingi 816,000,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Mei 2014 limefanikiwa kupata shilingi 504,459,728/= sawa na asilimia 62. Shirika lilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 500,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 379,677,521/= sawa na asilimia 76.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Shirika la Magazeti ya Serikali limepanga kutekeleza malengo yake makuu mawili kama yafuatayo: Kuwa na magazeti yenye makala na habari za kielimu ambazo zinalenga kuondosha umasikini nchini na kuishajiisha jamii kushiriki katika mipango ya maendeleo ya nchi kwa kuchapisha na kusambaza magazeti ya kila siku na kila wiki. Kuwa na miundombinu bora ya ofisi na vitendea kazi na kuwaongezea ujuzi na uwezo wafanyakazi wa Shirika. Katika kutekeleza malengo hayo Shirika limejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kufuatilia upatikanaji wa habari ndani na nje ya nchi pamoja na kufanya utafiti wa kutafuta masoko mapya ya habari;
ii. Kuchapisha magazeti ya kila siku na kila wiki pamoja na kusafirisha na kusambaza ndani na nje ya Zanzibar;
iii. Kuongeza ujuzi na utaalamu kwa watendaji wa Shirika la Magazeti ya Serikali; na
iv. Kulipatia Shirika vitendea kazi bora na vya kisasa.

Mhe. Naibu Spika, ili Shirika la Magazeti ya Serikali liweze kutekeleza malengo hayo, naliombea kuidhinishiwa shilingi 592,726,000/= kwa kazi za kawaida na kukusanya shilingi 500,000,000/=.

TUME YA UTANGAZAJI

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Tume ya Utangazaji ni kusimamia vyombo vya utangazaji vya serikali na vya binafsi vinavyoanzishwa nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Tume ya Utangazaji ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kufuatilia ugawaji wa mawimbi na udhibiti wa utendaji wa vyombo vya utangazaji nchini;
ii. Kuhudhuria kongamano la kitaifa la matumizi ya mfumo wa utangazaji wa dijitali; na
iii. Kugharamia vikao vya bodi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Tume ya Utangazaji imeweza kufanya mambo yafuatayo:-

i. Tume imegawa mawimbi kwa redio jamii za Tumbatu na Mkoani pamoja na kuwasaidia gharama za uanzishwaji wake. Pia imegawa mawimbi kwa Redio Wananchi FM;
ii. Tume imeweza kusimamia upatikanaji wa nafasi za masomo ya muda mrefu kwa watendaji wake wawili, mmoja (1) Stashahada katika fani ya Uhasibu na mwengine Stashahada ya Manunuzi;
iii. Imetoa mafunzo kwa wamiliki wa vyombo vya utangazaji kuhusu hatua mpya ya mfumo wa ugawaji wa mawimbi ya dijitali; na
iv. Vikao vya Bodi vimefanyika na kupitia maombi ya kuanzisha vyombo vya utangazaji.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Tume iliidhinishiwa jumla ya shilingi 187,537,951/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Mei 2014 imefanikiwa kupata shilingi 159,869,401/= sawa na asilimia 85. Tume imepangiwa kukusanya jumla ya shilingi 44,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 46,862,960/= sawa na asilimia 107.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Tume ya Utangazaji imepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni:- Kuwa na maendeleo katika Sekta ya Utangazaji inayokwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya kisasa kwa kushiriki mikutano kuhusu matangazo ya teknolojia ya dijitali, kuratibu na kusimamia taratibu za utangazaji nchini kwa mujibu wa Sheria ya Utangazaji. Kuwa na mazingira bora ya kazi yatakayoiwezesha Tume kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwa kuipatia huduma, vifaa na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

Katika kutekeleza malengo hayo Tume imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kufanya utafiti wa watazamaji kuhusu mfumo mpya wa utangazaji wa dijitali;
ii. Kuanzisha mfumo wa kufuatilia na kurikodi vipindi vinavyorushwa na redio nchini (*monitoring system*), ili kufahamu maudhui yanayorushwa na vyombo vya utangazaji vya redio ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa matakwa ya sheria Na 5 ya Tume ya Utangazaji;
iii. Kufuatilia mabadiliko ya teknolojia ya dijitali ili kuviweka vyombo vya utangazaji katika hali ya kuwa tayari katika mabadiliko yanayotokea kila mara; na
iv. Kuwapatia mafunzo watendaji na kuipatia ofisi huduma na vitendea kazi.

Mhe. Naibu Spika, ili kukamilisha vyema malengo iliyojipangia Tume ya Utangazaji katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, naomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 201,499,000/= kwa kazi za kawaida na kukusanya shilingi 52,000,000/=.

KAMPUNI YA UUNGANISHAJI MAUDHUI (ZMUX)

Mhe. Naibu Spika, itakumbukwa katika bajeti iliyopita ya mwaka wa fedha 2013/2014 Kampuni hii ilieleza majukumu yake ya msingi yakiwemo. Kuendesha kwa ufanisi na kujitegemea kwa shughuli za kuunganisha maudhui kwa kutumia miundombinu ya dijitali na kuhakikisha Zanzibar inakwenda sambamba na mageuzi ya utangazaji yanayotokea duniani kila mara.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Kampuni ya Uunganishaji Maudhui ilipanga kutekeleza mambo yafuatayo kwa fedha ambazo imekusanya:-

i. Kuunganisha vipindi vinavyopendwa na watazamaji kupitia dijitali;
ii. Kusimamia zana na vifaa vilivyomo katika miundombinu ya dijitali;
iii. Kuwapatia wafanyakazi stahiki zao; na
iv. Kuipatia ofisi vitendea kazi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Kampuni ya ZMUX imetekeleza shughuli zufuatazo:-

i. Kampuni imeimarisha huduma zake kwa kununua vifaa vya kukamatia matangazo kama vile *SDI – converter, satellite dish* moja (1) na *decoders* mbili (2) pamoja na kufanya matangazo (*promotion*);
ii. Kampuni imefanya utafiti mdogo ili kujua mahitaji ya wateja kwa lengo la kuimarisha huduma zake kwa Unguja na Pemba. Utafiti huo umebaini kwamba wateja wengi wanapendelea kuongeza chanali nyingi zaidi zikiwemo za mipira na maisha ya wanyama. Aidha, watazamaji wa Pemba wametaka kuondolewa kukatika kwa matangazo; na
iii. Ili kuwa na mazingira bora ya kazi na kuiwezesha Kampuni kutoa huduma bora na zenye ufanisi, Kampuni imenunua samani kwa ajili ya ofisi, vifaa vya kuandikia, malipo ya umeme kwa vituo vyake saba (7) kwa Unguja na Pemba pamoja na ununuzi wa mafuta kwa ajili ya majenereta.

Mhe. Naibu Spika, Kampuni ya Uunganishaji Maudhui kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 120,000,000/= na imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 86,000,000/= sawa na asilimia 72 hadi kufikia Mei 2014.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Kampuni ya *ZMUX* imepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni Kupitisha matangazo ya televisheni na redio kwenye miundo mbinu yake yanayotumia mfumo wa dijitali na kuwa na mazingira bora ya kazi ili kuiwezesha Kampuni kutoa huduma bora na zenye ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza malengo hayo Kampuni imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuunganisha vipindi vinavyopendwa na watazamaji kupitia mtandao wa dijitali;
ii. Kuongeza idadi ya watumiaji wa huduma za malipo, na kuongeza chanali katika miundombinu;
iii. Kutunza zana na vifaa vilivyomo katika miundo mbinu ya dijitali, na kuondoa kukatika katika kwa matangazo kisiwani Pemba;
iv. Kuwapatia wafanyakazi stahiki zao;
v. Kuipatia ofisi vitendea kazi; na
vi. Kuwaongezea ujuzi na utaalamu wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, ili Kampuni ya *ZMUX* iweze kutekeleza malengo yake naomba kuidhinishiwa makusanyo ya shilingi 140,000,000/= na kutumia shilingi 96,000,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

CHUO CHA UANDISHI WA HABARI

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Chuo cha Uandishi wa Habari ni kutoa mafunzo ya taaluma ya uandishi wa habari na mawasiliano kwa ngazi ya Cheti na Diploma kwa kuzingatia matakwa ya soko la ajira sambamba na kufanya tafiti mbali mbali na kutoa ushauri unaotokana na matokeo ya tafiti hizo kwenye tasnia hiyo. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Chuo cha Uandishi wa Habari kilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuongeza wataalamu wa fani ya Habari na Mawasiliano ya Umma yanayokidhi mahitaji ya soko la ajira; na
ii. Kuandaa mazingira bora ya kazi na kutoa huduma bora kwa wafanyakazi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Chuo cha Uandishi wa Habari kimefanya shughuli zifuatazo:-

i. Chuo kimewapatia taaluma vijana 122 ambao wamehitimu ngazi ya Cheti na Diploma. Kati ya hao wanawake 83 na wanaume 39 ambapo ngazi ya Cheti ni 60 na Diploma 43 na 20 wanafunzi wa ngazi ya cheti cha msingi;
ii. Chuo kimeweza kusimamia shughuli za uendeshaji wa kila siku kwa kugharamia ununuzi wa vifaa na kuipatia huduma za ofisi, gharama za ufanyaji wa mitihani, ununuzi wa redio za kufundishia, kuajiri walimu wapya wanne na Afisa Manunuzi mmoja, kufanya mahafali ya tano ya kuwatunuku vyeti wanafunzi wa Diploma na Cheti;
iii. Katika kusimamia upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi, Chuo kimeweza kutayarisha na kuchapisha nakala 5000 za gazeti la mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi na pia kushiriki katika maonesho ya Sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar; na
iv. Chuo kimewasomesha wafanyakazi watano kwa ngazi za Shahada ya Uzamili wawili (2) mmoja fani ya Uongozi na Utawala na mwengine fani ya Uongozi wa Fedha, Shahada ya Kwanza ya Mawasiliano ya Kimataifa mmoja (1) na Stashahada ya kawaida mmoja (1) na Shahada ya Udaktari wa Falsafa ya Mawasiliano kwa Umma mmoja (1). Aidha, wafanyakazi watatu wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nchini China.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014. Chuo kiliidhinishiwa jumla ya shilingi 275,000,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Mei 2014 imefanikiwa kupata shilingi 188,540,000/= sawa na asilimia 69. Chuo kilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 103,153,000/= na hadi kufikia Mei 2014 shilingi 117,618,000/= zimekusanywa sawa na asilimia 114.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Chuo cha Uandishi wa Habari kimepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni Kuimarisha kiwango cha rasilimali watu katika taaluma ya habari kwa kuimarisha mtaala wa kufundishia na mafunzo kwa ajili kuongeza uwezo wa utoaji wa habari. Kuwa na mazingira mazuri ya kazi na kujifunza kwa kusimamia tafiti za wanafunzi, kutoa ushauri elekezi na kuandaa na kushiriki mijadala ya kimafunzo.

Katika kutekeleza malengo hayo Chuo kimepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kudahili wanafunzi wapya 100 kwa ngazi ya Cheti na Diploma;
ii. Kendelea kupitia mtaala wa kufundishia pamoja na kuzipitia kanuni na miongozo mbali mbali kwa ajili ya kuifanya iwe bora zaidi;
iii. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na kufanya tathmini ya shughuli za Chuo;
iv. Kukuza na kuimarisha mahusiano na taasisi mbali mbali kwa kukitangaza Chuo ndani na nje ya nchi;
v. Kuongeza uwajibikaji kwa kuajiri walimu wapya watatu katika fani ya Mawasiliano kwa Umma, Uhusiano na Ukutubi;
vi. Kuliimarisha darasa la Lugha ya Kichina kwa kuanzisha programu ya muda mfupi kwa wanafunzi wa nje ya Chuo kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka China; na
vii. Kujenga madarasa mapya ya Chuo katika eneo la Kilimani.

Mhe. Naibu Spika, ili kukamilisha vyema malengo ya Chuo cha Uandishi wa Habari katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, nakiombea kuidhinishiwa jumla ya shilingi 254,810,000/= kwa kazi za kawaida. Aidha, Chuo kimepanga kukusanya jumla ya shilingi 126,250,000/=.

SEKTA YA UTALII

Mhe. Naibu Spika, Sekta ya Utalii inajumuisha Kamisheni ya Utalii, Chuo cha Maendeleo ya Utalii na Hoteli ya Bwawani. Taasisi hizi zimepewa jukumu la kupanga mikakati, kusimamia, kuendeleza Utalii na kuitangaza Zanzibar ili Sekta hii iende sambamba na Sera na Mikakati ya Serikali katika kufikia malengo makuu ya kuimarisha uchumi wa Taifa na kupunguza umasikini.

KAMISHENI YA UTALII

Mhe. Naibu Spika, jukumu la msingi la Kamisheni ya Utalii Zanzibar ni kupanga mikakati, kuratibu, kusimamia, kuendeleza na kutangaza shughuli za Utalii ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Kamisheni imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuifanya Zanzibar kuwa kituo bora cha utalii katika Ukanda wa Bahari ya Hindi;
ii. Kuhakikisha wananchi wengi wanashiriki katika shughuli za utalii ili kutekeleza dhana ya utalii kwa wote ; na
iii. Kuiwezesha Kamisheni ya Utalii kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kujenga mazingira bora ya kazi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Kamisheni ya Utalii imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Ofisi ya Uwanja wa Ndege imetengenezwa na kuwekewa kipoza hewa. Aidha, kwa msaada wa Kampuni ya SS Bakhresa ofisi ya Bandarini imefanyiwa matengenezo makubwa. Aidha jitihada za kupata ofisi katika kiwanja cha ndege cha Julius Nyerere zinaendelea kufanyiwa kazi;
ii. Kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Kamisheni imefanya kazi ya uwekaji wa madaraja hoteli 71 zilizofikia vigezo vilivyowekwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kazi hiyo, hoteli za nyota tano hoteli 16, nyota nne hoteli tisa, nyota tatu hoteli 43 na nyota mbili hoteli sita;
iii. Kamisheni imeandaa warsha mbili kwa watembezaji watalii pamoja na wadau wengine huko Pemba kwa lengo la kuwaelezea umuhimu wa utoaji wa taarifa sahihi za vivutio vya utalii;
iv. Kamisheni imeendelea kushiriki katika maonesho tofauti ya kitaifa na kimataifa kwa lengo la kuitangaza nchi kiutalii. Maonesho hayo ni pamoja na Saba Saba mjini Dar es Salaam, Maonesho ya Siku ya Utalii mjini Mwanza, '*World Trade Market'* London, *ITB* mjini Berlin, *Arabian Travel Market* (*ATM*) Dubai na *INDABA* Afrika ya Kusini. Lengo la kushiriki maonesho hayo ni kuitangaza Zanzibar na kuwavutia watalii wengi zaidi kutembelea nchini.
Mafanikio ya maonesho hayo ni kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaotembelea Zanzibar ambapo Januari hadi Disemba 2013 imepokea idadi ya watalii 181,301 tofauti na mwaka 2012 ambapo ilipokea watalii 169,223. Kadhalika Zanzibar imeweza kuwaalika waandishi wa habari wa vyombo tofauti vya kimataifa kwa lengo la kutolewa taarifa za vivutio vya Zanzibar katika vyombo vya habari, magazeti na majarida ya masoko husika.
Kutokana na ziara hizo Zanzibar imeendelea kuandikwa na majarida tofauti kama vile *Petite Fute France, Exclusive Destination Netherland, Timeless Memories and Exceptional Destination_ Hilton World Wide* Afrika Kusini. Aidha katika ushiriki huo Kamisheni imefanikiwa kuchapisha nakala 6500 za vipeperushi kwa lugha tofauti zikiwemo Kirusi (1500), Kijerumani (1500), Kichina (1500) na Kiingereza (2000);
v. Kamisheni imefanikiwa kushiriki katika ziara zilizofanyika nchini Seychelles na Singapore. Kufuatia ziara hizo Singapore imeahidi kuisaidia Kamisheni kuufanyia mapitio Mpango Mkuu wa Utalii Zanzibar;
vi. Kushiriki katika utafiti uliofanyika baina ya Kamisheni ya Utalii na Wizara ya Maliasili na Utalii (T. Bara), Benki Kuu ya Tanzania, Idara ya Takwimu na Idara ya Uhamiaji kwa lengo la kubaini idadi halisi ya uingiaji na utokaji wa wageni wanaotembelea nchini. Utafiti huo sasa uko katika hatua ya uandishi wa ripoti.
Aidha, utafiti uliofanyika katika kipindi cha mwaka (2012/13) unaonesha kuwa soko la Tanzania bado linategemea zaidi bara la Ulaya na Amerika, japo kuwa kuna ongezeko la wageni kutoka bara la Asia na Mashariki ya Kati. Idadi ya siku za ukaazi kwa wageni bado imebaki kuwa siku 9 kwa Tanzania Bara na siku 6 kwa Zanzibar.;
vii. Mafunzo ya wajumbe wa Kamati za Utalii za Wilaya yametolewa kwa ajili ya kuwawezesha kufahamu wajibu na majukumu yao kulingana na sheria;

viii. Katika kuhakikisha wananchi wanashiriki katika utalii kupitia mpango wa utalii kwa wote, Kamisheni imeandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 36 vya utalii pamoja na kuandaa ziara za kimafunzo kwa wananchi katika maeneo ya utalii. Aidha, imeendesha mashindano ya resi za ngalawa kwa lengo la kuifufua michezo ya asili ikiwa ni sehemu ya vivutio vya utalii; na

ix. Katika kuendeleza taaluma kwa wafanyakazi, Kamisheni imewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wanne (4), ngazi ya Stashahada mmoja (1), ngazi ya Shahada mmoja (1), na ngazi ya Shahada ya Pili wawili (2). Vile vile wafanyakazi wanne wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi, watatu (3) nchini China na mmoja (1) nchini Uholanzi.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014. Kamisheni iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,628,003,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 100,000,000/= kwa kazi za maendeleo na hadi kufikia Mei, 2014 imefanikiwa kupata shilingi 861,043,086/= sawa na asilimia 53 kwa kazi za kawaida na shilingi 30,000,000/= sawa na asilimia 30 kwa kazi za maendeleo. Aidha, ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,202,000,000/= katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kufanikiwa kukusanya shilingi 1,354,091,365/= sawa na asilimia 113.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Kamisheni ya Utalii imepanga kutekeleza malengo yake makuu matatu nayo ni Kuendelea kuifanya Zanzibar kuwa kituo bora cha utalii katika ukanda wa Bahari ya Hindi, kutekeleza dhana ya Utalii kwa Wote ili uwe na tija zaidi kwa wananchi na kujenga mazingira bora ya kazi yatakayoiwezesha Kamisheni ya Utalii kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Katika kutekeleza malengo hayo Kamisheni imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuipatia ofisi zana bora za kufanyia kazi;
ii. Kufanya safari za kikazi kwa ajili ya kufuatilia utendaji wa kazi, utekelezaji na kuongeza mashirikiano na taasisi nyengine;
iii. Kushiriki katika maonesho ya matatu ya Kitaifa, manne ya Kimataifa;
iv. Kuendelea na utafiti wa kubaini vivutio vipya vya utalii;
v. Kuandaa vipindi mbali mbali vya redio, televisheni na makala katika magazeti na kutengeneza vipeperushi;
vi. Kutangaza Utalii kwa njia ya mtandao;
vii. Kuendeleza dhana ya utalii kwa wote kwa kufanya semina, makongamano kwa wananchi pamoja na taasisi za umma na za binafsi;
viii. Kuziwezesha Kamati za Utalii za Wilaya kukutana na kuandaa Vikao vya Makamishna na Wadau wa Utalii;
ix. Kupitia Sera ya Utalii, Mpango Mkuu wa Utalii, Mpango Mkakati, Kanuni na Marekebisho ya Sheria; na
x. Kufanya ukaguzi kwa miradi ya utalii.

Mhe. Naibu Spika, ili Kamisheni iweze kutekeleza malengo yake, naiombea iidhinishiwe matumizi ya shilingi 1,389,200,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha Kamisheni imepanga kukusanya shilingi 1,387,658,000/= kwa ajili ya kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2014/2015.

CHUO CHA MAENDELEO YA UTALII ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, jukumu la msingi la Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar ni kutoa taaluma itakayowezesha kujenga rasilimali watu wenye ujuzi, utaalamu na stadi zinazohitajika na kukubalika katika viwango vya kimataifa ili kuimarisha Sekta ya Utalii Zanzibar.

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar kilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuwajengea wanafunzi uwezo wa kuwasiliana kwa Lugha ya Kiingereza kwa kuwapatia moduli za kusomea stadi za mawasiliano katika shughuli za utalii (English for Hospitality and Tourism Level I & II);

ii. Kutangaza dhana ya utalii kwa wote kwa kufanya mazungumzo na vijana wa kizanzibari na kuwashajiisha kujiunga na Chuo kwa kuwaonesha shughuli mbali mbali zinazofanywa na Chuo katika Skuli tisa (9) za Wilaya tisa (9) za Unguja na Pemba; na
iii. Kuwajengea uwezo walimu kwa kuinua viwango vyao vya taaluma, mmoja Shahada ya Kwanza fani ya Utalii na Usafiri, watatu Stashahada fani ya Utalii, Ukarimu na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimeweza kutekeleza yafuatayo:-

i. Chuo kimewapatia wanafunzi moduli za kusomea stadi za mawasiliano katika shughuli za Utalii (*English for Hospitality and Tourism level I & II*). Moduli nane (8) za "*level I*" na "*level II*" zimepatikana na bado ununuzi huo utaendelea kufanyika kadiri fedha zitakapopatikana katika makusanyo ya Chuo;
ii. Katika kutekeleza dhana ya utalii kwa wote, Chuo kimefanya mazungumzo na wanafunzi wa skuli za sekondari Unguja na Pemba kwa lengo la kuwashajiisha kujiunga na Chuo ili waweze kufaidika na utalii. Utekelezaji wa kazi hiyo ulifanywa katika Skuli 8 za wilaya nane (8) za Unguja na Pemba, ambazo ni Micheweni, Gando, Uweleni na Shamiani kwa Pemba na skuli za Bububu, Mkwajuni, Uzini na Fumba kwa Unguja. Chuo kitaendelea na kazi hiyo kwa skuli nyengine zikiwemo za wilaya mbili zilizobaki za Unguja;
iii. Ili kuinua viwango vya elimu vya wakufunzi, Chuo kimesomesha mwalimu mmoja Shahada ya Kwanza fani ya Utalii na Usafiri katika Chuo Kikuu cha Kenyatta nchini Kenya, walimu wawili Stashahada katika fani ya Utalii na Ukarimu na mwalimu mmoja Stashahada fani ya Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Uhasibu;
iv. Katika kutoa taaluma bora ya Utalii nchini, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014. Chuo kilitoa wahitimu 163 kati ya hao Stashahada 53, wanawake 30 na wanaume 23 na kwa ngazi ya Cheti 110, wanawake 73 na wanaume 37; na
v. Chuo kimetiliana saini hati ya ushirikiano baina yake na Chuo cha Utalii cha Nairobi-Kenya (KUC) kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na taaluma.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014. Chuo kiliidhinishiwa jumla ya shilingi 423,479,359/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Mei, 2014 imefanikiwa kupata shilingi 336,627,307/= sawa na asilimia 79. Chuo kilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 280,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 316,496,350/= sawa na asilimia 113.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni: Kuendeleza upatikanaji wa rasilimali watu watakaoweza kutoa huduma bora zenye viwango katika shughuli za utalii. Kuandaa mazingira bora ya kazi, ufundishaji na usomaji kwa kuimarisha shughuli za taaluma pamoja na kuwajengea uwezo wakufunzi na wafanyakazi. Katika kutekeleza malengo hayo Chuo kimepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kudahili wanafunzi wapya 300, wakiwemo Stashahada 60 na 240 wa ngazi ya Cheti;
ii. Kuimarisha shughuli za taaluma ikiwemo mitihani, kuongeza vipindi vya mafunzo ya vitendo (*practical sessions*), kuchapisha vyeti vya wahitimu 203 na kutunuku vyeti na stashahada kwa wahitimu 203, wanaume 148 na wanawake 57;
iii. Kuendelea kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi sita wakiwemo mmoja ngazi ya shahada ya kwanza fani ya Utalii na Usafiri, mmoja ngazi ya stashahada fani ya Uongozi wa

shughuli za Utalii na Ukarimu, mmoja ngazi ya stashahada fani ya Mapishi (*Culinary Arts*) na wafanyakazi watatu – mmoja ngazi ya cheti fani ya Utunzaji kumbukumbu, mmoja ngazi ya cheti fani ya Mahusiano ya Umma na mmoja ngazi ya shahada ya pili fani ya Uongozi wa Fedha;

iv. Kuzipatia ofisi vitendea kazi kwa mujibu wa mahitaji;
v. Kutoa mwamko wa utalii kwa wote kwa wanafunzi wa skuli za sekondari kwa kuonesha shughuli zinazofanywa na Chuo cha Maendeleo ya Utalii ili kuwashajiisha kujiunga na chuo;
vi. Kufanya mikutano miwili na wawekezaji wa hoteli za kitalii na taasisi nyengine zinazotoa huduma za kitalii; na
vii. Kukusanya taarifa za uchambuzi wa hali halisi (situation analysis) kuangalia uwezekano wa kufungua Tawi la Chuo Pemba.

Mhe. Naibu Spika, ili chuo kiweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya shilingi 419,029,000/= kwa kazi za kawaida na kukusanya shilingi 360,000,000/=.

HOTELI YA BWAWANI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Hoteli ya Bwawani ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kupokea idadi kubwa ya wageni katika Hoteli ya Bwawani; na
ii. Kutoa huduma bora kwa wateja wa kitaifa na kimataifa.

UTEKELEZAJI HALISI

i. Katika kuitangaza hoteli vipeperushi 15,000 vya matangazo vya kuweka vyumbani vimechapishwa, kutayarishwa kadi za maoni 2,500 zinazojazwa na wageni na kutayarisha bango la matangazo. Vile vile vipindi 32 vimetayarishwa na kuoneshwa;
ii. Huduma za upatikanaji wa maji katika maeneo ya hoteli zimeimarishwa kwa kufunga mashine tano za kusukumia maji, kuimarisha miundombinu ya umeme pamoja na kufanyia matengenezo mashine za kufulia, kupigia pasi na kuimarisha huduma za jikoni;
iii. Ofisi ya mapokezi imeimarishwa kwa kutoa mafunzo maalum ya uwekaji takwimu za wageni wanaopokelewa hotelini na kuweka kompyuta maalum inayoweka takwimu hizo;
iv. Matengenezo ya vyumba 32 yamefanyika, kati ya hivyo, vyumba 26 matengenezo madogo madogo na vyumba 6 matengenezo makubwa, pamoja na matengenezo ya hita 10 za vyumba vya wageni. Aidha ukumbi wa Salama umefanyiwa matengenezo kwa kuwekwa vipoza hewa viwili, seti moja ya mapazia na zulia sehemu ya wageni mashuhuri; na
v. Hoteli imeendelea kuwalipia ada ya masomo wafanyakazi wake 12 katika fani ya utunzaji nyumba wawili, Chakula na Vinywaji wawili, manunuzi mmoja, mapokezi mmoja, mapishi wawili, uongozi wa shughuli za utalii na ukarimu watatu na rasilimali watu mmoja.

Mhe. Naibu Spika, Hoteli ya Bwawani kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 950,000,000/= na imefanikiwa kukusanya shilingi 850,154,351/= sawa asilimia 89 hadi Mei 2014.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Hoteli ya Bwawani imepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni:-

Kuwa na idadi kubwa ya wageni kwa kuitangaza hoteli kwa njia ya mtandao, vipeperushi na vipindi vya televisheni na redio, kutoa huduma bora kwa wateja wa kitaifa na kimataifa pamoja na kuanzisha "*Internet Café*", kuweka takwimu sahihi za wageni wanaoingia na kutoka na kuimarisha mazingira ya hoteli.

Kuwa na mazingira bora ya kazi kwa kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma katika fani ya Hoteli na kuipatia Hoteli vitendea kazi vitakavyowezesha Hoteli kufanya kazi kwa ufanisi. Katika kutekeleza malengo hayo Hoteli imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuitangaza Hoteli kwa njia ya mtandao, vipeperushi na kuandaa vipindi vya televisheni na redio kwa lengo la kuongeza idadi ya wageni;
ii. Kuipatia Hoteli huduma ya "*Internet Café*";
iii. Kufanya ukarabati wa maeneo ya Hoteli vikiwemo vyumba na kumbi; na
iv. Kuwapatia wafanyakazi mafunzo na kuipatia Hoteli vitendea kazi vyenye ubora.

Mhe. Naibu Spika, ili hoteli iweze kutekeleza malengo yake itahitaji kuidhinishiwa makusanyo ya shilingi 995,000,000/= na kutumia shilingi 850,000,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

SEKTA YA UTAMADUNI NA MICHEZO

Mhe. Naibu Spika, Sekta ya Utamaduni na michezo imeundwa na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, Baraza la Kiswahili, Baraza la Sanaa, Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho, na Baraza la Taifa la Michezo. Taasisi hizi zimepewa jukumu la kusimamia, kuratibu, kufufua, kuendeleza na kudumisha shughuli zote za Utamaduni na Michezo Zanzibar.

KAMISHENI YA UTAMADUNI NA MICHEZO

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Kamisheni ya Utamaduni na Michezo ni kuratibu na kusimamia maendeleo ya utamaduni na michezo hapa Zanzibar kwa kushirikiana na Idara na Mabaraza yaliyo chini yake. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendeleza shughuli za Utamaduni na Michezo nchini; na
ii. Kujenga mazingira bora ya kazi yenye kuleta ufanisi zaidi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kamisheni imeufanyia matengenezo Uwanja wa Amaani pamoja na kuweka nyasi bandia katika kiwanja hicho. Kazi ambayo imefanywa kwa ufanisi mkubwa na Kampuni ya Ekika ya Dar es Salaam na Viva Turf ya China;
ii. Katika kushajiisha wanamichezo kuwa na ari ya kushiriki katika mashindano ya kitaifa na kimataifa na kuiletea nchi ushindi na sifa, Kamisheni imewazawadia wanariadha walioshiriki katika mashindano ya Afrika ya Mashariki na Kati.
Vile vile Kamisheni imegharamia Timu ya Taifa ya Zanzibar kushiriki katika mashindano ya Kombe la Chalenji yaliyofanyika nchini Uganda na kuiwezesha timu ya Chuoni kwenda kushiriki mashindano ya kombe la washindi Barani Afrika. Aidha, Kamisheni imesaidia kufanikisha mashindano ya kimataifa yaliyoandaliwa kwa ajili ya kuadhimisha Sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.
iii. Kamisheni imeshiriki katika vikao vya mchakato wa kuanzishwa kwa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika ya Mashariki ambayo makao makuu yake yatakuwa Zanzibar;
iv. Kamisheni imegharamia mafunzo ya wafanyakazi wake watano (5) kati ya hao mmoja Stashahada ya Uzamili ya Ustawi wa Jamii na watatu (3) wamejiunga na mafunzo ya Stashahada ya Rasilimali Watu na mmoja ni Shahada ya Pili ya Takwimu;
v. Kamisheni ilizindua kitabu cha "Urithi wa Utamaduni Usioshikika" kilichojumuisha utamaduni wa ngoma za asili na sanaa za Zanzibar. Kazi hii imefanywa na Kamisheni kwa kushirikiana na Shirika la *UNESCO*;
vi. Kazi ya ununuzi wa vifaa vya kurikodia sauti na picha kwa ajili ya Studio ya Muziki na Filamu inaendelea;

vii. Kamisheni imefanya mapitio ya Sera ya Michezo kwa kushirikisha wadau Unguja na Pemba. Hatua za kuikamilisha Sera hiyo kupitia vikao vinavyohusika zinaendelea; na
viii. Kamisheni imeratibu matamasha yaliyofanyika Zanzibar yakiwemo Tamasha la Mwangapwani na Kojani, Tamasha la Nchi za Jahazi na Sauti za Busara.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014. Kamisheni iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,470,503,024/= kwa kazi za kawaida na shilingi 80,000,000/= kwa kazi za maendeleo, hadi kufikia Mei 2014 imefanikiwa kupata shilingi 1,178,165,048/= sawa na asilimia 80 kwa kazi za kawaida na shilingi 80,000,000/= sawa na asilimia 100 kwa kazi za maendeleo.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni:- Kuwa na maendeleo ya Utamaduni na Michezo kwa kuanzisha Programu ya Bonanza za Utamaduni na Michezo, kuwezesha ushiriki wa timu katika mashindano ya kitaifa na kimataifa, kuendeleza Nyumba ya Sanaa na kufanya tafiti za utamaduni. Kuwa na mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi nafasi za masomo na kuipatia ofisi vitendea kazi ili kuleta ufanisi zaidi. Katika kutekeleza malengo hayo Kamisheni imepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kuratibu na kusimamia ushiriki wa timu katika mashindano ya kitaifa na kimataifa;
ii. Kuanzisha Programu ya Bonanza ili kuendeleza Utamaduni na Michezo katika Skuli za Unguja na Pemba na kusimamia Tamasha la Mzanzibari;
iii. Kuipatia nyezo za kufanyia kazi Nyumba ya Sanaa;
iv. Kuendeleza tafiti za Urithi wa Utamaduni Usioshikika;
v. Kutafuta maeneo ya kuanzisha viwanja vya michezo katika ngazi za Wilaya;
vi. Kukagua na kutathmini Programu za Michezo nchini.
vii. Kuratibu siku ya mazoezi ya viungo kitaifa; na
viii. Kuifanyia marekebisho sheria ya Ngoma na Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho.

Mhe. Naibu Spika, ili Kamisheni ya Utamaduni na Michezo iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, naomba iidhinishiwe shilingi 901,531,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Idara hii ni kuenzi, kuhifadhi na kuendeleza historia ya Zanzibar kwa kutumia Makumbusho, na maeneo ya kihistoria. Pia kuelimisha jamii juu ya umuhimu na faida za matumizi ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha maeneo ya kihistoria ili yawe na hadhi ya kitaifa na kimataifa;
ii. Kuyatangaza maeneo ya kihistoria kwa manufaa ya wadau wote na maendeleo ya nchi; na
iii. Kuandaa mazingira bora ya kazi yatakayowezesha Idara kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kazi za maendeleo zilizofanywa na Idara katika maeneo ya kihistoria Mangapwani ni ujenzi wa choo, uchimbaji wa kisima cha maji, na uungaji wa umeme. Shughuli nyengine zilizofanywa na Idara ni uwekaji wa nguzo za mipaka katika maeneo ya kihistoria ya Pete, Bungi, Unguja Ukuu, Chuini, Dunga na Shakani; Vile vile maeneo saba (7) ya kihistoria ya Mangapwani, Mnarani, Kisima cha Chini kwa Chini, Chemba ya Watumwa, Bi Khole, Kuumbi na Mwana Mpambe yamepimwa na kupatiwa hati miliki. Aidha maeneo ya kihistoria ya Mkamandume na Msikiti Chooko yameendelezwa ili kuyaweka katika hali nzuri;

ii. Idara imehifadhi eneo la Chuini kwa kulifanyia uchunguzi kutambua athari za urithi wa utamaduni na historia wa jamii zilizoishi katika eneo hilo "*Cultural Heritage Impact Assessment" (CHIA)*;

iii. Idara kwa kushirikiana na watafiti kutoka Uingereza wanaendelea na kukusanya taarifa na takwimu za akiolojia na kugundua mabaki ya historia na utamaduni katika eneo la Unguja Ukuu, Fukuchani na Kuumbi. Matokeo ya tafiti hizi zimeshatolewa, lakini taarifa zaidi za kimaabara zinaendelea kufanyiwa kazi. Vile vile taarifa za utafiti wa "geophysical research" kwa eneo la Unguja Ukuu ripoti yake tayari imeshakamilika kwa hatua za mwanzo;

iv. Idara imetoa mafunzo ya awali kwa viongozi wa vijiji vya Fukuchani, Mangapwani, Bungi na Mwanampambe juu ya umuhimu wa kuyatunza na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria. Mafunzo kwa vijiji vyengine yataendelea;

v. Idara imekusanya taarifa za awali za maeneo matano ya kihistoria ya Pango la Kuumbi, Mwanampambe, Pango la Machaga Pete, Mwinyi Mkuu na Ras Mkumbuu kisiwani Pemba;

vi. Katika kuyatangaza maeneo ya kihistoria, Idara imetengeneza filamu (5) za vielelezo kwa maeneo matatu ya kihistoria ya Mangapwani, Mwanampambe na Hamam la Hamamni. Pia imetayarisha na kurusha hewani vipindi kumi na nne (14) kupitia ZBC Redio, TV na Zenj FM vyenye maudhui ya Mahusiano ya Zanzibar na Jumuiya za Kimataifa katika Karne ya 19, Historia ya Kasri ya Mfalme wa Tumbatu pamoja na Msikiti wa Jongowe, historia ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale kabla na baada ya Mapinduzi na vipindi sita (6) vya redio kuhusu Urithi wa Utamaduni wa Baharini. Aidha, Idara imesambaza vipeperushi vya maeneo manne (4) ya historia ya Mangapwani, Kisima cha Chini kwa Chini, Mahandaki ya Vita vya Pili vya Dunia pamoja na Mnara wa Vita, Mahodhi ya Kidichi. Pia Idara imetengeneza mabango ya matangazo kwenye maeneo ya Bandarini na Ngome Kongwe. Idara imeandika makala 12 kupitia Zanzibar Leo juu ya umuhimu wa maeneo ya kihistoria;

vii. Idara imekamilisha hatua za awali za kuwasiliana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali juu ya uingizaji wa somo la uhifadhi katika mitaala ya elimu. Hatua za kuwapatia mafunzo wanafunzi zinaendelea kwa kuyatembelea maeneo ya kihistoria;

viii. Pia Idara imegharamia mafunzo ya wafanyakazi kumi na tatu, ngazi ya cheti fani ya Ukutubi (1), Stashahada Uhifadhi wa Kumbukumbu (2), Manunuzi na Ugavi (1) Kazi za Kijamii (1), Urithi wa Utamaduni na Utalii (2), Utawala wa Umma (2) na Mahusiano ya Kimataifa (1),Shahada ya Kwanza ya Sayansi na Ualimu (1), Shahada ya Mawasiliano katika Uhandisi (1) na Shahada ya Uzamili ya Historia (1); na

ix. Idara imeshiriki maonesho ya kitaifa ya miaka 50 ya Mapinduzi na Siku ya Wafanyakazi Duniani.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014. Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 748,209,200/= kwa kazi za kawaida na shilingi 230,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Mei 2014 imefanikiwa kupata shilingi 404,973,500/= sawa na asilimia 54 kwa kazi za kawaida na shilingi 230,000,000/= sawa na asilimia 100 kwa kazi za maendeleo. Pia ilipangiwa kukusanya shilingi 210,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 73,042,959/= sawa na asilimia 35 hadi kufikia Mei 2014. Utekelezaji halisi umeelezwa ukurasa wa 13na 15

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imepanga kutekeleza malengo makuu matatu nayo ni Kuwa na Makumbusho yenye ubora wa kimataifa kwa kuyaendeleza, kuyafanyia matengenezo na kuyawekea uzio ili kuhifadhi na kuendeleza Urithi wa Utamaduni na Historia nchini.

Kuwa na maeneo ya kihistoria yalio endelevu kwa kuandaa mafunzo kwa viongozi wa Shehia katika kila Wilaya, kuanzisha programu zitakazowajengea wananchi mwamko juu ya umuhimu wa kuhifadhi na kulinda maeneo ya kihistoria kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini**.**

Kuwa na mazingira bora ya kazi yatakayowezesha Idara kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuipatia vifaa muhimu vya kutendea kazi na kuwajenga wafanyakazi kielimu na kitaaluma. Katika kutekeleza malengo hayo Idara imepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kuyafanyia matengenezo, maeneo ya kihistoria Unguja na Pemba na kuyawekea uzio Vitongoji na Ole Mandani;

ii. Kuanzisha programu zitakazowajengea wananchi muamko wa kulinda, kuhifadhi na kutunza maeneo ya kihistoria kupitia sinema, kufanya semina za wadau, vipindi vya televisheni na redio na filamu;
iii. Kuwapatia mafunzo masheha na Madiwani katika kila Wilaya;
iv. Kufanya utafiti wa maeneo ya kihistoria kwa ajili ya maendeleo ya utalii;
v. Kuendeleza Makumbusho ya Mnazimmoja ili kutoa huduma bora;
vi. Kushiriki katika matamasha ya kitaifa na kimataifa; na
vii. Kuandaa mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi wake.

Mhe. Naibu Spika**,** ili Idara ya Makumbusho iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naomba kuidhinishiwa matumizi ya shilingi 718,440,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 150,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Aidha, Idara imepanga kukusanya shilingi 210,000,000/=**.**

BARAZA LA KISWAHILI LA ZANZIBAR:

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Baraza la Kiswahili la Zanzibar ni kukuza, kushajiisha na kufuatilia matumizi na maendeleo ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Baraza hili lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kukuza na kuendeleza matumizi ya Kiswahili sahihi na fasaha kitaifa na kimataifa; na
ii. Kuweka mazingira mazuri ya ofisi kwa kuipatia vifaa bora na vya kisasa.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Baraza la Kiswahili limetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Katika kutoa taaluma kwa umma kuhusu matumizi ya Kiswahili fasaha, Baraza limetayarisha na kurusha vipindi 24 vya "Kiswahili Lugha Yetu" kupitia *ZBC TV* na Redio na vipindi sita (6) kupitia "Hits FM Redio" kwenye kipindi cha "Kasha la Kiswahili". Baraza limechapisha jarida la "*BAKIZA*" toleo namba mbili, Kitabu cha Mawasiliano ya Misingi ya Kiswahili kwa Wageni na vitabu vidogo vidogo vya lugha tatu (Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa) na vipeperushi kwa ajili ya kuyasambaza ndani na nje ya nchi;
ii. Baraza linaendelea na kazi ya utafiti wa majina ya viumbe vya baharini na mazingira yao kwa lengo la kuandika kamusi ambapo kukamilika kwake kutasaidia kuhifadhi msamiati na kutoa fursa kwa watumiaji wa lugha, watafiti na wanaojifunza Kiswahili kuyaelewa majina hayo na kuyatumia ipasavyo;
iii. Baraza limegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watendaji wake watatu, kati ya hao mmoja (1) ni Shahada ya Pili ya Fasihi ya Lugha na wawili ni Diploma ya Usimamizi wa Fedha;
iv. Katika kuadhimisha siku ya Kiswahili Zanzibar, mashindano ya uandishi wa insha katika ngazi za Wilaya yamefanyika kwa skuli 33 za Serikali na binafsi Unguja na Pemba; na
v. Maktaba ya BAKIZA imeimarishwa kwa kuongezwa vitabu na majarida jambo ambalo limepelekea kuongezeka idadi ya watumiaji.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza la Kiswahili liliidhinishiwa jumla ya shilingi 76,900,000/= kwa matumizi ya Mengineyo na hadi kufikia Mei 2014 imefanikiwa kupata shilingi 9,000,000/= sawa na asilimia 12. Baraza lilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 41,580,000/= na kufanikiwa kupata shilingi 1,038,000/= sawa na asilimia 2. Utekelezaji halisi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 umeelezwa katika ukurasa wa 60 na 61.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Baraza la Kiswahili limepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni Kukuza, kuendeleza na kutangaza matumizi ya Kiswahili sahihi na fasaha kitaifa na kimataifa na Kuwa na mazingira mazuri ya kazi kwa kuipatia ofisi vitendea kazi na kuwapatia wafanyakazi fursa za masomo. Katika kutekeleza malengo hayo Baraza limepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kuandika na kuchapisha majarida, makala na vitabu vyenye maudhui mchanganyiko na kuvisambaza ndani na nje ya nchi;
ii. Kukitangaza Kiswahili kupitia vyombo vya habari, machapisho na maonesho ya kitaifa na kikanda;
iii. Kuendelea kukusanya msamiati wa viumbe vya baharini na ule wenye mnasaba na mazingira ya baharini; na
iv. Kufanya mashindano ya uandishi wa Fani za Kiswahili utakaoshirikisha waandishi chipukizi na wanafunzi wa sekondari na kutambua michango ya watu na taasisi zinazoendeleza Kiswahili katika kuadhimisha Siku ya Kiswahili Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ili Baraza la Kiswahili Zanzibar liweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naomba liidhinishiwe shilingi 40,800,000/= kwa ajili ya matumizi Mengineyo na kuchangia shilingi 40,000,000/= kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

BODI YA SENSA YA FILAMU NA SANAA ZA MAONESHO

Mhe. Naibu Spika, jukumu la msingi la Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho ni kukagua na kuhakiki filamu na sanaa za maonesho, ili kuhakikisha kuwa haziharibu maadili ya jamii zinapooneshwa hadharani na kusikika kwenye vyombo vya habari na rekodi (*CD*,***DVD***). Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Bodi hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuongeza idadi na ubora wa filamu na Sanaa za maonesho zinazozingatia mila na silka za utamaduni wa Mzanzibari; na
ii. Kuimarisha mazingira mazuri ya kazi na wafanyakazi pamoja na kuipatia ofisi vitendea kazi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Jumla ya vipindi vitatu (3) vilitayarishwa na kurushwa kwenye vyombo vya habari vya Shirika la Utangazaji la ZBC pamoja na kuandaa mikutano na wasanii kwa lengo la kuwaelimisha ubora wa sanaa zao katika kulinda maadili;
ii. Bodi imeendelea na uhakiki na ukaguzi wa filamu na kazi za sanaa mbali mbali zikiwemo matamasha mawili ya Tamasha la Jahazi Literary lililovishirikisha jumla ya vikundi tisa (9) kutoka mataifa mbali mbali ya nje ya nchi na Tamasha la Sauti za Busara ambalo lilivishirikisha jumla ya vikundi 38 navyo kutoka mataifa mbali mbali wakiwemo wenyeji Zanzibar. Uhakiki ulifanyika kwa filamu za michezo mchanganyiko na vikundi vya sanaa za maigizo Zanzibar ili kuhakikisha hazendi kinyume na maadili ya Zanzibar *(Tafadhali angalia kiambatisho namba 4);*
iii. Katika kuendeleza mikakati ya ukaguzi ili kuweka mazingira yatakayoiokoa jamii na wimbi la mmong'onyoko wa maadili kupitia fani ya sanaa, Bodi ilifanya kikao kimoja na watendaji wa Bodi ya Filamu ya Tanzania kwa lengo la kurahisisha utendaji wa pamoja. Maamuzi yaliyofikiwa katika vikao hivyo yameanza kutekelezwa. Pia imetengeneza vipeperushu vyenye kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa maadili pamoja na matayarisho ya msingi ya matangazo mafupi ya elimu yatakayotumika kwenye vyombo vya habari na maeneo mbali mbali nchini; na
iv. Filamu maalumu ya kutoa elimu juu ya usimamizi na uendelezaji wa maadili imetayarishwa na itaanza kuoneshwa hivi karibuni katika shehia mbali mbali za Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014. Bodi iliidhinishiwa jumla ya shilingi 38,000,000/= kwa matumizi Mengineyo na hadi kufikia Mei, 2014 imefanikiwa kupata shilingi 8,000,000/= sawa na asilimia 21. Utelezaji wake unaonekana katika ukurasa wa 63 na 64.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho imepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni Kuwa na kazi za sanaa zilizo bora zenye kuzingatia mila, silka na utamaduni wa Kizanzibari. Kuwa na mazingira bora ya kutendea kazi kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuipatia ofisi vitendea kazi muhimu. Katika kutekeleza malengo hayo Bodi imejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kukagua filamu na sanaa zinazooneshwa hadharani ili kuhakikisha zinaendana na maadili ya Kizanzibari;
ii. Kuandaa vikao viwili kwa vikundi vya sanaa katika kuwajengea uelewa juu ya kutayarisha kazi zinazoendana na maadili ya Kizanzibari; na
iii. Kuratibu maendeleo ya sanaa na utamaduni wa Mzanzibari kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya ndani na nje ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ili Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho iweze kukamilisha shughuli zake, naiombea shilingi 21,500,000/= kwa ajili ya matumizi Mengineyo kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

BARAZA LA SANAA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Baraza la Sanaa Zanzibar ni kusimamia na kuratibu maendeleo ya shughuli za sanaa Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Baraza la Sanaa lilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuwafanya wananchi wengi kushiriki na kutekeleza shughuli za sanaa kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na
ii. Kuimarisha mazingira ya kazi yatakayowezesha Baraza kufanya kazi zake kwa ubora na ufanisi zaidi.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Baraza la Sanaa limetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Baraza limewahamasisha wasanii kwa kuwapatia taaluma ya utengenezaji wa bidhaa bora ili kuweza kupata soko kubwa zaidi ndani na nje ya nchi. Pamoja na kurusha hewani vipindi 6 kwa *ZBC* Redio, *ZBC – TV* na "*Hits FM*" vinavyozungumzia mambo ya sanaa na utamaduni;
ii. Baraza limeshiriki kwenye maonesho na fensi ya sherehe ya miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar;
iii. Mafunzo yametolewa kwa wasanii wa fani tofauti kuhusu maradhi ya Ukimwi kwa lengo la kuwapa taaluma na njia salama za kujikinga na maambukizi ya maradhi hayo;
iv. Kwa kuadhimisha miaka 50 ya Muungano Baraza kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo limeandaa mashindano ya sanaa katika fani za Ushairi, Tenzi, Taarabu Asilia, Taarab ya Kisasa, Muziki wa Dansi na Ngoma Asilia pamoja na kuwazawadia washindi;
v. Baraza limeshughulikia malalamiko kuhusu ghasia za muziki na matendo yasiyoridhisha katika vijiji vya Nungwi, Jambiani, Paje, Tunguu na Bwejuu na kuyapatia ufumbuzi;
vi. Mashindano ya sanaa za uchoraji yamefanyika ili kuibua vipaji kwa wanafunzi wa skuli za Mwanakwerekwe 'A hadi E' ambapo wanafunzi 180 wameshiriki; na
vii. Utafiti kwa ajili ya kuangalia vikwazo vinavyowakabili wasanii katika kuendeleza kazi zao umefanyika kwa Wilaya mbili za Unguja. Utafiti huo umebaini kwamba vipaji vipo, vinahitaji kuendelezwa na kutafutiwa soko la bidhaa zao. Utafiti wa aina hiyo utaendelea kwa Wilaya nyengine.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza liliidhinishiwa jumla ya shilingi 30,466,925/= kwa ajili ya matumizi Mengineyo na hadi kufikia Mei 2014 limefanikiwa kupata shilingi 7,000,000/= sawa na asilimia 23. Aidha, Baraza la Sanaa lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 7,000,000/= na limeweza kukusanya shilingi 4,800,000/= sawa na asilimia 68 hadi kufikia Mei 2014. Utelezaji halisi umeelezwa katika ukurasa wa 66 na 67.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Baraza la Sanaa limepanga kutekeleza malengo makuu mawili nayo ni Kuwa na maendeleo ya sanaa na wasanii kwa kuwafanya wananchi wengi kushiriki na kutekeleza

shughuli za sanaa kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kuimarisha mazingira ya kazi kwa kuipatia ofisi vitendea kazi ili kuwezesha Baraza kufanya kazi zake kwa ubora na ufanisi zaidi. Katika kutekeleza malengo hayo Baraza limejipangia shughuli zifuatazo:-

i. Kuendelea kuibua vipaji vya sanaa kwa watoto na vijana katika Wilaya nane za Zanzibar;
ii. Kuwashajiisha wasanii kuziendeleza kazi zao na kuyatumia masoko yaliyopo kujiongezea mapato; na
iii. Kuendelea kufanya utafiti wa maendeleo ya kazi za sanaa katika Wilaya nane zilizobakia.

Mhe. Naibu Spika, ili Baraza liweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naliombea jumla ya shilingi 20,800,000/= kwa ajili ya matumizi Mengineyo kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 na kukusanya shilingi 10,000,000/=.

BARAZA LA TAIFA LA MICHEZO

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya msingi ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar ni kusimamia maendeleo ya michezo yote iliyosajiliwa. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Baraza hili limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuchangia upatikanaji wa vifaa vya michezo kwa vyama 10 vya michezo;
ii. Kutoa mafunzo kwa walimu na waamuzi wa michezo 10 (Mpira wa Miguu, Mikono, Pete, Wavu, Meza, Kikapu, Magongo, Mchezo wa Kuogelea, Judo na Riadha);
iii. Kutoa zawadi kwa wanamichezo waliofanya vizuri katika michezo ya kitaifa na kimataifa;
iv. Kusaidia uanzishaji wa viwanja vinne (4) vya michezo katika Wilaya ya Micheweni, Mkoani, Magharibi na Kusini Unguja;
v. Kusaidia uendeshaji wa mashindano ya ndani kwa vyama 10 vya michezo;
vi. Kuandaa mashindano ya michezo ya watoto na vijana chini ya umri wa miaka 21; na
vii. Kusimamia mashindano ya michezo ya watu wenye ulemavu.

Malengo yaliyopangwa katika mwaka 2013/2014 yameelezwa katika ukurasa wa 68 na 69.

UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Baraza la Taifa la Michezo limefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Baraza limewapatia vifaa vya michezo vyama vya Mpira wa Pete, Mpira wa Kikapu, Karati, Mpira wa Wavu, Mpira wa Mikono, Bao, Karata, Mpira wa Meza, Chama cha Michezo cha Viziwi na Walemavu wa Akili. Vifaa hivyo ni jezi, meza, mabao, karata, nyavu na mabusati ambavyo vilitolewa kwa kujiandaa na mashindano ya kitaifa na kimataifa. Mashindano mbali mbali kwa timu za Zanzibar zilizoshiriki kitaifa na kimataifa angalia kiambatisho namba 5;

ii. Baraza kwa kushirikiana na Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar kwa ufadhili wa Shirika la "Save the Children" limewapatia mafunzo walimu 150 wa michezo ya mpira wa miguu. Walimu hao ni wa michezo kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wanaofundisha timu za mitaani. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia mradi wa "*International Inspiration*" mafunzo ya makocha wa michezo ya mpira wa wavu na riadha yametolewa;

iii. Katika kuhakikisha michezo inaendelea kukuwa nchini. Baraza kwa kushirikiana na Idara ya Ardhi, Mipango Miji na Vijiji wametenga maeneo ya viwanja vya michezo midogo midogo kwa Unguja na Pemba. Kwa Wilaya ya Kaskazini eneo la Nungwi limetengwa na kupimwa kwa ajili ya shughuli hizo, kwa Wilaya ya Mjini eneo la Uwanja wa Tumbaku limepimwa na kupewa hati miliki. Kwa upande wa Pemba katika eneo la Uwanja Gombani, kuna eneo limetengwa kujengwa viwanja vitakavyoweza kutumika kwa michezo midogo midogo *Multipurpose Stadium*;

iv. Baraza kupitia Kamisheni ya Utamaduni na Michezo limewapatia zawadi wanamichezo walioshinda katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati ya Judo na Riadha, pamoja na washindi walioshinda katika mashindano ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar na miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar;

v. Baraza limesaidia vyama 20 vya michezo kushiriki katika mashindano ya kitaifa pamoja na kukiwezesha Chama cha Mpira wa Pete kuandaa mashindano ya ligi kuu ya Zanzibar. Aidha, Baraza limegharamia Uchaguzi Mkuu wa Chama cha Riadha na kupata viongozi wapya;

vi. Mashindano ya timu za watoto za kombaini za Wilaya 10 yamefanyika kwa kushirikiana na Kamati ya *Central* Taifa kwa ufadhili wa Taasisi ya *Arma Promotion* ya Zanzibar; na

vii. Mashindano ya michezo ya Watu wenye Ulemavu wa uziwi yamefanyika. Aidha, Baraza limeandaa utaratibu uliowezesha kupatikana fedha zilizotumika kuwapeleka wanamichezo wa Chama cha Ulemavu wa Akili kwenye mashindano yaliyofanyika Kibaha Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza liliidhinishiwa jumla ya shilingi 141,699,406/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Mei 2014 imefanikiwa kupata shilingi 11,646,350 /= sawa na asilimia **8**. Utekelezaji uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2013/2014 umeelezwa kutoka ukurasa wa 69 hadi 71.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Baraza la Taifa la Michezo limepanga kutekeleza malengo makuu mawili ambayo ni kuwa na mazingira bora ya shughuli za maendeleo ya michezo na kuwa na mazingira bora ya utendaji kazi yatakayowezesha Baraza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Katika kutekeleza malengo hayo Baraza limepanga shughuli zifuatazo:-

i. Kutoa mafunzo kwa walimu na waamuzi kwa vyama 15 vya michezo;
ii. Kuwapatia vifaa vya michezo vyama 15 vya michezo;
iii. Kushajiisha na kuhamasisha kuandaliwa kwa mashindano ya watoto na vijana chini ya umri wa miaka 19;
iv. Kusaidia shughuli za maendeleo ya michezo kwa watu wenye ulemavu; na
v. Kufanya mapitio ya Katiba za vyama vinne vya michezo ya Karati, Judo, Kuogelea na *Trithlon* na kusimamia kanuni zake.

Mhe. Naibu Spika**,** ili Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar liweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naliombea kuidhinishiwa shilingi 90,000,000/= kwa ajili ya matumizi Mengineyo kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

SHUKRANI

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu naomba kuwashukuru wote waliochangia katika kutayarisha hotuba hii. Shukurani maalumu ziwaendee Mhe. Naibu Waziri Bihindi Hamad Khamis, Katibu Mkuu Dk. Ali Saleh Mwinyikai, Naibu Katibu Mkuu Nd. Issa Mlingoti, Afisa Mdhamini Pemba, Wakurugenzi, Wakuu wengine wa Taasisi za Wizara na wasaidizi wao wote kwa kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na uadilifu mkubwa. Kwa kweli wamekuwa wakinisaidia sana kutekeleza majukumu yangu. Pia nawashukuru Wenyeviti wa Mabaraza na Bodi mbali mbali kwa kusimamia vyema taasisi zetu na kunishauri kwa hekima na busara.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwashukuru wafanyakazi, wanamichezo, wasanii, wadau wa utalii na wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa michango yao katika kufanikisha shughuli za Wizara.

Mhe. Naibu Spika**,** nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuishukuru Wizara ya Fedha pamoja Tume ya Mipango kwa ushirikiano mkubwa waliotupa kwa mahitaji ya fedha na ushauri.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu nizishukuru nchi mbali mbali na Mashirika kadhaa ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Serikali ya Misri, Japan, Serikali ya Oman, *UNESCO* na Shirika la Utangazaji la Ujerumani (*DW*) tuliyoshirikiana nao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini mkubwa. Aidha, naomba kuishukuru Kamati ya Mifugo, Habari, Uwezeshaji na Utalii kwa namna ambavyo muda wote imekuwa ikinisaidia katika kuiongoza Wizara hii.

Mhe. Naibu Spika**,** naliomba sasa Baraza lako tukufu kujadili kwa kina matumizi jumla ya shilingi 15,366,575,000/=. Fedha hizo ni pamoja na miradi iliyoibuliwa kwenye maabara ya Utalii *(Tourism Laboratory).* Kati ya hizo shilingi 9,371,200,000**/=** kwa kazi za kawaida na shilingi 400,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Pia naomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 5,595,375,000/= kwa utekelezaji wa Programu ya Utalii. Aidha, naliomba Baraza lako liidhinishe makusanyo ya mapato ya shilingi 1,718,658,000/= kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia makusanyo ya shilingi 2,236,250,000/= ambazo hukusanywa na taasisi zilizoruhusiwa kutumia makusanyo hayo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za taasisi hizo**.**

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa heshima kubwa na taadhima nawaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili, watushauri, watuelekeze na baadae watupitishie bajeti hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa kabla hatujaanza utaratibu wa kuchangia tumepata wageni wapo hapa juu, wageni hao ni wa Mhe. Mahamoud Thabid Kombo kutoka jimbo la Kiembesamaki na ni wasanii saba wa kikundi cha *Nyota Video Product.* Msanii wa kwanza anaitwa Ndugu Muhusin Salum jina la kisanii Mudi, wa pili ni ndugu Shaana Ramadhani jina la kisanii Mzee Nyali, wa tatu Ndugu Abdul-latif Abdalla jina la kisanii Abduli, wa nne ndugu Saleh Shaibu jina la kisanii... watano ndugu Said Jina la kisanii Samora, wa sita Ndugu Ali Omar jina la kisanii Msauth, na wa saba (wa mwisho) ndugu Halfan Jina la kisanii mister Mathu. Kwa hivyo karibuni sana.

Waheshimiwa mpaka sasa tuna wachangiaji watatu wa kwanza namwita Mwenyekiti wa kamati ya Mifugo Utalii, Uwezeshaji na Habari, baadae ajiandae Mhe. Makame Mshimba Mbaoruk na wa tatu Mhe. Muhammedraza Hassanali.

Mhe. Asaa Othman Hamad (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru *Allah subhana wataala* kwa kutuwezesha leo hii kuwa wazima wa afya njema na kuweza kukutana tena katika Baraza lako tukufu. Vile vile kwa kuniwezesha kusimama hapa kutoa maoni ya kamati yangu ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika**,** Pili napenda kuendeleza shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuniruhusu nitowe mchango kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari na pia kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Bumbwini. Aidha, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa heshima na busara zake za kuiongoza Nchi yetu ya Zanzibar, kwa kuheshimu Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, Naomba pia uniruhusu kuipongeza Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Pongezi hizi zimuendee Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wake, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mashirikiano yao waliotupatia kipindi chote wakati Kamati ilipokutana nao mpaka leo tunawasilisha maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, Kabla ya kuendelea mbele, naomba niwashukuru Wajumbe wanaounda Kamati hii, kwa mashirikiano yao pamoja na fikra ambazo zimenifanya leo niwe nawasilisha maoni ya Kamati hii. Naomba niwatambue Wajumbe hao kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Mwenyekiti
2. Mhe. Abdalla Mohammed Ali	M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Bakari Makame	Mjumbe

4. Mhe. Kazija Khamis Kona — Mjumbe
5. Mhe. Amina Iddi Mabrouk — Mjumbe
6. Mhe. Asaa Othman Hamad — Mjumbe
7. Mhe. Mussa Ali Hassan — Mjumbe
8. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali — Mjumbe
9. Ndg. Himid Haji Choko — Katibu
10. Ndg. Rabia Juma Shaaban — Katibu

Mhe. Naibu Spika, baada ya utambulisho huo naomba nianze kutoa maoni na michango ya kamati yangu kwa utaratibu ufuatao:-

SHIRIKA LA MAGAZETI

Mhe. Naibu Spika**,** Shirika la Magazeti Zanzibar kwa muda mrefu sasa wamekuwa na kilio kikubwa cha kukosa mtambo wa uchapishaji. Inafahamika kwamba Shirika limekuwa likizalisha magazeti ya Zanzibar Leo, Zanzibar Leo jumapili na Zaspoti lakini uchapishaji wa magazeti hayo unafanyika Tanzania Bara ambapo asilimia 71 ya mapato ya gazeti yanatumika katika uchapaji. Kamati inapendekeza Shirika kutengewa fungu kwa ajili ya ununuzi wa mitambo ili kuondokana na kadhia wanayoipata.

Naamini Waziri atakubaliana na Kamati yetu na kulishajihisha suala hili kwani kwa kuwa na mitambo yetu wenyewe Shirika litazalisha ajira mpya na fedha zitakazopatikana zitabaki hapa Zanzibar kwa mantiki hiyo zitawanufaisha Wazanzibari, ni jambo la aibu kuona hadi leo bado tunashindwa kuchapisha magazeti hapa nchini. Kuchapisha magazeti mbali na Zanzibar ni kitendo cha kusikitisha mno na mitambo hiyo ya uchapishaji inahitajika haraka iwezekanavyo.

KAMISHENI YA UTALII

Mhe. Naibu Spika, naomba Serikali ifahamu maendeleo ya utalii yanatagemewa na kamisheni hii, lakini hadi leo kamisheni hii ina mapungufu mengi ya kiutendaji, ni jambo la kushangaza kuona kuwa Bodi ya Utalii chombo ambacho kinatoa miongozo ya utendaji kinakutana mara moja kwa mwaka badala ya mara tatu kwa mwaka. Hivyo Serikali ina jukumu maalum la kuiwezesha Bodi pamoja na Kamisheni hii kupanga kazi zake kikamilifu. Hivi sasa tunahitaji tuoneokane na tabia ya kusubiri watalii waje wenyewe, tunahitaji miuondombinu ya uhakika ya kutafuta masoko nchi za nje.

Mhe. Naibu Spika, moja katika changamoto kubwa Kamisheni ya Utalii ni takwimu; hadi leo Kamisheni inashindwa kupata takwimu sahihi za uingiaji na utokaji wa wageni. Suala hili ni suala mtambuka kunahitajika mashirikiano ya hali ya juu kati ya sekta mbali mbali zinazohudumia watalii nchini, upatikanaji wa takwimu sahihi utasaidia Serikali kufahamu, ni eneo gani linahitajika kupewa kipaumbele zaidi katika sekta hii.

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu inategemea utalii katika kuongeza pato la taifa ambapo kwa hivi sasa utalii unachangia asilimia 30 za fedha za kigeni, kwa maana hiyo ikiwa taifa letu linategemea sekta ya utalii kama chanzo cha mapato. Ni vyema basi sekta ya utalii ikatazamwa kwa mtazamo maalum na kuwa ni kipaumbele namba moja katika vipaumbele vya taifa.

SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (*ZBC*)

Mhe. Naibu Spika**,** ni jambo la kutia moyo sana kuona *ZBC* kuendelea na mfumo huu wa *digitali* katika matangazo yake ingawa kuna changamoto nyingi sana hasa katika kipindi hiki cha mpito kutoka analojia kwenda *digitali*.

Mhe. Naibu Spika**,** Uwezo wa kibajeti unaokasimiwa kwa Shirika hilo ni mdogo kabisa . Aidha, Kasma hiyo inapelekea Shirika kushindwa Kabisa kuingia katika mikataba ya kimataifa na hivyo kukosa hakimiliki ya kuliwezesha Shirika kuonesha moja kwa moja yaani *live* Matukio makubwa na Muhimu ulimwenguni ambayo mengine huwa yanalipiwa. Mhe. Naibu Spika, ni vyema kulitazama kwa jicho la huruma Shirika hili la utangazaji kwa kuingiziwa pesa zote walizoziomba shilingi 1,814,536,000 kwani lina jukumu kubwa sana kuliko tunavyofkiria.

Mhe. Naibu Spika, suala ya kulipia matangazo ya kibunge si geni kwani sote ni mashahidi wakati tulipokua katika Bunge la Katiba, sote tunakumbuka siku kikao kilipohirishwa baada ya kukatika kwa matangao ya moja kwa moja ya TBC1, na Mwenyekiti wa Bunge maalum la katiba alithibitisha kwamba walikua na Mkataba na TBC ambapo Bunge limelipia kwa ajili ya matangazo hayo. Hapa tulijifunza sana umuhimu wa matangazo ya moja kwa moja pamoja na umuhimu wa kulipia matangazo hayo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yako ya Uongozi ya Baraza la wawakilishi nayo ni mashahidi wa jambo hili. Hivi karibuni wakati inapokea ripoti ya awali inayohusu uandaji wa miongozo ya Kanuni na taratibu za kusikiliza maoni ya wananchi katika Kamati za Baraza, suala hili la kulipia matangazo lilisisitizwa sana. Tunaiomba Serikali ione umuhimu huu ili kuliwezesha shirika kufanya kazi zake vizuri na kwa umakini zaidi.

Mhe. Naibu Spika, wakati tunasubiri ombi hili kutekelezwa na Baraza lako tukufu, ombi ambalo linahitaji mashirikiano na mazingatio ya pamoja kati ya Wizara ya Fedha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Kamati yangu inalishauri Baraza lako tukufu kuwafikiria wafanyakazi hawa wa ZBC kama vile wanavyowafikiria wafanyakazi wa taasisi nyengine zinazotoa huduma wakati wa Vikao vya Baraza la Wawakilishi ikiwemo Afya, Umeme, Wakalimani na Taasisi za Kiusalama.

HOTELI YA BWAWANI

Mhe. Naibu Spika, kamati imefurahishwa sana kuona mpango wa serikali kuiendeleza hoteli ya Bwawani ili iwe ya kisasa zaidi katika kiwango cha kimataifa. Kamati inaiomba sana Wizara pamoja na Waziri wake kuhakikisha kuwa malengo ya hoteli hiyo yatimie katika bajeti 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, hii ni hoteli pekee ya serikali iliyobakia hivyo, serikali ihakikishe kwamba inaitunza na inaiendeleza na kuiweka katika hali nzuri ili ibakie kama ni kumbukumbu ya matunda ya mapinduzi ya 1964.

IDARA YA MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale ina majukumu mbali mbali pamoja majukumu yake ya msingi ni kuenzi, kuhifadhi na kuendeleza historia ya Zanzibar kwa kutumia makumbusho na maeneo ya kihistoria. Pia kuelimisha jamii juu ya umuhimu na faida za matumizi ya makumbusho na mambo ya kale. Kwa msingi huo, Kama Idara ilivyojipangia malengo yake katika mwaka 2014/2015, Kamati inaomba malengo hayo yatekelezwe kwani kwa kuimarisha maeneo ya kihistoria na kutafuta maeneo mengine ambayo yana sifa ya kihistoria inawavutia idadi kubwa ya wananchi na wageni kutembelea maeneo hayo.

KAMISHENI YA UTAMADUNI NA MICHEZO

Mhe. Naibu Spika, Suala la michezo hapa kwetu limekuwa kitendawili kisichokuwa na jibu. Nchi nyingi sana duniani zimekuwa zikijitangaza kupitia michezo. Isitoshe michezo imekuwa ikitoa ajira mbalimbali kwa vijana. Lakini ni kinyume kwa nchi yetu hususan katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara kujipanga na kuweka mikakati maalum ya kuimarisha michezo iliyopo na kuifufufa michezo mingine ambapo katika miaka ya nyuma michezo hiyo iliipa sifa kubwa nchi ya Zanzibar na kutoa ajira kwa wananchi.

CHUO CHA MAENDELEO YA UTALII

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Utalii ni taasisi iliyopewa jukumu la kutoa taaluma itakayowezesha kujenga rasilimali watu wenye ujuzi, utaalamu na stadi zinazohitajika na kukubalika katika viwango vya Kimataifa ili kuimarisha sekta ya Utalii Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilipata muda wa kutembelea Chuo cha Maendeleo ya Utalii na kupata taarifa kuwa moja wapo ya sababu ya kushindwa kuendeleza kikamilifu mashirikiano ya kikanda na kimataifa kwa kutoshiriki mikutano mbalimbali ya kimataifa ni kutokana na uhaba wa fedha. Kamati yetu inaamini kufanya jambo kwa usahihi ni matokeo ya kujifunza kutoka kwa watu au sehemu mbalimbali. Kamati inaomba Chuo kupatiwa fedha ili kutekeleza malengo yaliyojiwekea, ikitiliwa maanani kuwa kukiwezesha chuo hiki ni kutoa upeo wa vijana wetu kujifunza na kujipatia ajira zaidi ndani na nje ya nchi.

CHUO CHA UANDISHI WA HABARI

Mhe. Naibu Spika, majukumu ya chuo cha Uandishi wa Habari ni kutoa mafunzo, ushauri na taaluma ya uandishi wa habari. Kamati ilipokwenda kutembelea chuo hiki na kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake, kamati iligundua kua chuo hicho kina uhaba wa nafasi za ofisi pamoja na madarasa kiasi ambacho kinachukua wanafunzi kidogo sana; hivyo kinakosa mapato kutoka kwa wanafunzi wengine wengi. Kamati inapendekeza kupewa jengo kwa chuo hicho ili kuweza kufanya shughuli zake za kutoa elimu na kuleta maendeleo nchini kwetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba nitumie wasaa huu tena kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Aidha, Napenda kuwashukuru pia Wajumbe wote kwa usikivu na utulivu wao wakati nasoma maoni ya Kamati yangu.

Mhe. Naibu Spika, Kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wete ninaunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ambayo ina mambo mengi katika majukumu hasa ya michezo na utalii ambayo ni roho ya nchi yetu.

Nianze na ukurasa wa 68 katika Baraza la Taifa la Michezo. Hapa sina hoja nyingi sana lakini nilikuwa na mawazo ya fikra na mara nyingi sana huwa napendelea kutoa ushauri wangu bure sio kwa malipo. Mhe. Naibu Spika, naomba sana maoni yangu katika hali ya Mwenyekiti, mara hii ningeomba sana serikali iangalie awe Mwenyekiti sasa ashuke chini kwa kwenda kugombaniwa na wana michezo wote. Sio kuwe na uteuzi wa Rais kwa sababu kuna mambo ambayo yanahitajika kwa mujibu wa sheria kwa sababu uteuzi wa Rais kwa mujibu wa utaratibu hakuna mtu mwengine yeyote ambae anaweza kutengua kanuni kama kukitokea jambo ambalo linaweza Mwenyekiti kufanya jambo lililokuwa kinyume na kanuni zenyewe.

Sasa kuwepo sheria hiyo ya kuweza kushuka chini Mwenyekiti kwenda kuchaguliwa basi naamini kutakuwa na sheria ambayo aidha imlinde au kumuondoa ili kuleta ufanisi. Tunaomba sana suala hilo na mimi naamini Mheshimiwa wangu anaweza akafanya jambo hilo, niseme Mheshimiwa nampenda sana lakini tofauti yetu moja yeye CUF mimi CCM basi, lakini naamini hivyo kuwa anaweza akatekeleza hili suala kwa mujibu wa utaratibu na kuwasaidia hasa wapenda michezo wa Zanzibar wanapotaka kupata maendeleo.

Nikiendelea tena ukurasa wa 51 hapa mimi huwa ninasikitika sana na hapa tunasema kuwa nikichukua kifungu ambacho kilichokuwa asilia na mimi ninachokipenda hasa katika fani yangu katika mambo ya kushajiisha wanamichezo kushiriki hasa wanariadha. Riadha Zanzibar tukitaka tusitake tumeiangusha, tumeivuruga tunasahau sana kwamba katika ulimwengu ni sehemu moja kubwa sana michezo ya riadha. Pia nchi inakua ni kioo kizuri kwa michezo ya aina hii ya riadha, lakini ninasikitika sana hata katika zile sherehe za miaka 50 riadha waliambiwa na wao washiriki hatukupata kushiriki kwa sababu gani na pesa zilikopeshwa nyingi na Mhe. Raza? Alivyosema hapa milioni sabiini *including* na hiyo michezo ya riadha, ninasikitika sana haikuwepo michezo hiyo, sijui tumekosa nini jamani.

Kama uongozi tumeweka uongozi mzuri nikiwemo mwenyewe Makamu wa Rais wa riadha. Leo tumekuwa na riadha omba omba wakati chombo tunacho cha kutusaidia; kwa kweli mimi ninasikitika sana. Ninaomba sana Mhe. Waziri umejitahidi vya kujitahidi, unatutafutia kocha kutoka nchi za nje, umetafuta mambo mengi sana lakini bado Mheshimiwa hili jambo halijafikia pahali pa *standard* tuna viwango vizuri, watoto wazuri wana viwango vizuri wako *serious* katika masuala haya. Mheshimiwa

mimi naomba sana tuwajali vijana wetu kama tunavyojali michezo ya mipira na hiyo nayo inatia *fund*, tena sisi tunazidi zaidi kuliko mchezo wa mpira.

Sisi tunaingia kwenye Jumuiya ya Madola, tunakwenda nje. Tunakuja na medali za dhahabu Mheshimiwa hapa na wewe mwenyewe ndie mmoja ambae unawapokea watoto na unakwenda kule kuwafanyia tafrija. Nitatoa fungu, nitalisogeza huko. Mimi naomba sana Mheshimiwa hili suala tulipe kipaumbele ili kuweza kufanikisha masuala haya ya michezo.

Mhe. Naibu Spika, niende katika hoteli ya Bwawani. Hivi karibuni nimesikia pale kulikuwa na *tender* au niseme kulikuwa na wafadhili ambao wanataka kuitengeneza Hoteli ya Bwawani. Mhe. Naibu Spika, kumefikia wapi, kulikuwa na wafadhili wawili, *challenge* ilikwenda ikapata mfadhili mmoja na mpaka leo Mheshimiwa mambo haya ya ku-*delay* ndio tunakufa maskini Wazanzibari. Tuna urasimu mkubwa sana Mhe. Makamu wa Pili, tunawafanya vijana wetu wawe maskini, wawe wizi, wawe wavuta bangi kutokana na sisi wenyewe hatuja-*maintain* vizuri kuwa-*control* watoto wetu katika masuala kama haya.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana nipewe jibu la suala hili tumefikia wapi muekezaji huyu mpaka leo hii. Kuna maneno ambayo wengine wanasema kwamba sehemu ile ikivunjwa ikijengwa nyengine tutamuondoa mzee wetu Hayati Abeid Karume, hapana. Tunakwenda na *model* ya kisasa tutamuenzi, tutamuekea kijumba cha historia kama ndie muanzilishi. Kama ikiwa tatizo ni hilo basi tutafanya *special* kitu hicho cha kumbukumbu cha kujua ndivyo wanavyofanya wenzetu huko nchi za nje kwa *history* ya hapa palikuwa moja, mbili, tatu. Naomba sana Mheshimiwa hili suala lifatilie na kuja kunipa jibu ili kuondoa umaskini Zanzibar. Urasimu uondoke bwana tumechoka. Wawekezaji wanakimbia Zanzibar kutokana na urasimu wetu tuna-*delay* sijui kitu gani. Mimi kwa kweli Mhe. Naibu Spika, ninasikitika sana.

Niingie katika masuala ya Chuo cha Utalii na Maendeleo. Chuo hiki kizuri sana, lakini walimu wao wanapokwenda nje fedha zao hamuwakamilishii kwa nini, na ile ni haki ya yule mtu. Pengine na yeye kenda kukopa anaingia hatiani huko au mpaka msikie kaingia vitunduni huko Mahakamani. Ninaomba sana Mhe. Waziri hili suala ulikamilishe vizuri sana.

Nimesema mimi juzi kwa kupitia Idara ya Kazi na nikasema utalii isiwe udhalilishaji wa Wazanzibari. Lakini ukiona kimantiki sasa hivi utalii huu haunufaishi watu wa Zanzibar, hili niliseme Mheshimiwa. Sababu ya kwanza hata watembezaji wageni; watu wa nje wanatembeza wageni je, wanaijua historia ya Zanzibar wanatupotoshea bwana. Mhe. Waziri ninamuomba sana awe *serious* na suala kama hili usikubali. Ninaomba sana Mhe. Naibu Spika, tuwape wenyewe wazawa kiupaumbele ili waweze kupata; kwanza anapata ajira na baadae wanaitangaza historia ya Zanzibar kwa sababu wanajua tangu asilia na wazee wao. Ninaomba sana Mheshimiwa kama kuna vibali vya watu wa nje futa, hakuna kuweka Mheshimiwa naomba sana, futa. Hiki kitu ukakamavu lazima, ninakuaminia Mheshimiwa wangu.

Mheshimiwa twende kwenye mahoteli; kwenye mahoteli nishachoka kusema Mhe. Naibu Spika, naheshimu sheria na kama ingekuwa si sheria basi ningekuwa Rais wa maandamano ya vijana wote, ningewakusanya tukaandamana kutaka haki yetu.

Sasa mimi ninaomba sana Mhe. Waziri tufanye mazoezi ya kwenda hoteli hadi hoteli hilo suala ninakuamini uko tayari kweli, ninaamini hivyo lakini sasa hivi niko *serious* kwa kweli. Sasa hii kazi tuifanye nimechoka kwa sababu utakuta kuna mahoteli mengine nimekwenda kule kuna *Sea Cliff*, utakuta kuna Wakenya hawana vibali wapo nchi hii. Anatoka muhindi yuko kwa *account* tu analipwa ma-*foreign money* chungunzima.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana Mheshimiwa. Mtu analipwa mapesa chungunzima anatoka nchi za nje; analipiwa nyumba, analipiwa simu, analipiwa kila kitu, mguu wake akiweka kwenye

ardhi analipiwa. Hapa wazanzibari maskini ya Mungu wana mavyeti wamesoma Chuo cha Hesabu Chwaka, wamekaa na vyeti vyao wamevitia mfukoni. Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana, tumechoka sasa uchumi tule wenyewe. Uchumi tunao lakini wazanzibari tumeukalia.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri nimeshasema sana, nimeshachoka kukwambieni Mawaziri jamani, hebu kuwa na uchungu na hawa vijana wetu. Juzi nimesema hapa kuna mtwana mmoja anawadhalilisha watu wa *United Petrolium* mpaka leo hajaondoka. Tunaambiwa kesho ataondoka, vibali vinatoka kiholela tu bila ya mpango wowote. Kwa kweli Mheshimiwa bado lingali linasikitisha. Mimi nitaendelea kusema wala sitoogopa kusema kabisa. Kwa sababu ninawatetea wazanzibari katika haki yao, ndani ya ardhi yao waweze kupata yale maslahi ambayo tuliyokusudia. Mhe. Naibu Spika, inauma sana.

Kwa hivyo ninaomba Mheshimiwa sasa tujiandae kabisa mimi na wewe hata *immigration* wanashindwa kutembea katika sehemu ambazo zilizokuwa tumevamiwa na wageni wengi. Mhe. Makamu wa Pili naomba nisikilize kidogo tumevamiwa na watu wageni kinyume na utaratibu wa nchi tumenyamaza kimya.

Mhe. Mtando nisikilize mwache Makamu wa Pili huku ninampa jambo lake, ninaomba sana, Mhe. Makamu wa Pili sasa hivi hali halisi ni ngumu sana. Zungumza na *immigration* ili tuweze kufanya jambo ambalo ishakuwa uingiaji kiholela umezidi Zanzibar, sasa is too much! Mwamvuli wao ni mahotelini.

Mahoteli wamefanya kama ndio kificho chao ndio vichaka vyao. Hebu twendeni siku moja tufanye hili jambo Mhe. Naibu Spika, twendeni tukakamate watu tutawakamata watu kibao na nyinyi wenyewe mtasema mimi sipigi kelele hapa isipokuwa ninasema jambo la ukweli, na uone Wazanzibari hapo hawajakupigieni kura, uone kama sisi hatujafanikiwa katika sera zetu ambazo tumepanga ili kwa kuweza kupata ushindi wa mwaka 2015 kuendelea mbele. Mheshimiwa hilo ninaliomba sana. Ninaamini Mhe. Waziri utalifanya jambo hilo kwa ustaarabu wako na kwa umahiri wako na kwa kuwapenda wazanzibari wako katika masuala ambayo tuliyokubaliana.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye ZBC. ZBC kwa kweli hupata masikitiko makubwa sana Mheshimiwa ni chombo chetu kizuri sana lakini bado watu wako wanafanya kazi muda mwingi. Kwa mujibu wa utaratibu usiku na mchana lakini bado maposho yao wanakuwa hawayapati na vyumba vyao hivi vya *server;* vina baridi kali hata maziwa wanashindwa kupewa ningeomba sana Mheshimiwa tuweze kuwasaidia hawa kwa sababu kila jambo lina uzuri wake na hatari yake. Baridi ikiwa kali Mheshimiwa inakuwa ni tatizo ndani yake, suala hilo naomba tuweze kupewa sisi.

Mhe. Naibu Spika, kuna fedha ambazo zimetakiwa tuwalipe hao watu wa hatimiliki na hao kama kuna deni lao hilo tunaomba sana uweze kuwalipia ili kuweza kufikisha pahala ili Mheshimiwa wangu upate kujisafisha katika masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, hizi *camera* sidhani kama zina-*record* kwa sababu juzi hazikuonesha siku ya bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu, hapa mchezo ulizimwa kabisa haikuweza kuonesha. Sijui kama tutakuwa na *memory* zile za *cassette* au sijui kama hizi *camera* zinarikodi Mheshimiwa wangu. Kama kweli zinarikodi naomba basi zile *cassette* angalau niwe na kumbukumbu kama tulivyokuwa na kumbukumbu za *hansard* ambazo tulikuwa tunazifanyia kazi. Ninaomba sana Mheshimiwa hizo, lakini bado *camera* zako haziendi na wakati, *camera* hizi zimeshapitwa na wakati tuna *camera* ambazo zina miaka sijui mingapi. Kwa hiyo, naomba sana twende kwenye *system* ambayo ni ya kisasa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa ninaomba sana ili uweze kufanikisha mambo yako na masuala mengine ya suti tumewabarikia wenyewe watalipa wenyewe hili sipigi kelele kwa sababu tumeshasema sana wanunuliwe mavazi mazuri lakini hilo suala nakuachia mwenyewe.

Suala la posho la hapa Mheshimiwa kama lipo nakushukuru sana kwa hivyo uweze kufanikisha kwa wakati kama inavyotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia kama nilivyosema kuwa sikunyanganyi shilingi kwa sababu ninaamini ni mtu msikivu sana, lakini ninakuomba sana mambo niliyokuambia hayo yatilie maanani na uje kunijibu kwa ufasaha. Kwa sababu leo umekuja kunizingua hapa wewe mwenyewe na mimi nilishangaa sana Mheshimiwa wangu nashindwa hata kujielewa nini ninachokizungumza hapa.

Mhe. Naibu Spika, niseme kuwa naitia barka hotuba ya Mheshimiwa wangu sijawahi kutamka hata siku moja kusema naunga mkono bajeti tangu nianze, lakini hii nitatamka kwa sababu nina mambo ambayo humu ndani yake akiyasimamia vizuri katika usimamizi wa hoteli kwa kupata ajira vijana, basi naomba nimpatie asilimia 80 ili kilichobakia aje kunijibu nimalizie.

Wajumbe wenzangu nawaombeni na nyie mgaieni hizo asilimia 80 mpaka 90, sijakupigeni hata siku moja kampeni, lakini kwa hili nitakupeni kampeni kwa sababu kuna vitu hapa ambavyo atatuokoa huyu mtu ambae ni jasiri na anakubali hili suala kulishughulikia.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa pumzi na kutupa pumzi sote hapa ambazo ndio tunaringa nazo.

Mhe. Naibu Spika, ningelipenda ku-*declare interest* chini ya kanuni 59 kanuni ndogo ya 9 naomba niisome;

> "Mjumbe hatazungumzia jambo lolote ambalo yeye yeye mwenyewe ana maslahi nalo binafsi, isipokuwa baada ya kutaja namna halisi ya kiwango cha maslahi hayo"

Mhe. Naibu Spika, nataka tukumbushane kwamba Baraza hili ni la wananchi sio letu, sisi tumeletwa hapa kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, ningelipenda kumsaidia Mhe. Waziri kwani namuheshimu sana, kutoa ufafanuzi wa kina sakata hili la *Mapinduzi Cup*.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri pamoja na mwenzake walikuwa wanazungumza kwamba *Mapinduzi Cup* ni jambo la *private* yeye halitambui wala hizi pesa hazitambui, lakini kilichonisikitisha zaidi Mhe. Naibu Spika, wakati tunakutana na kamati ndogo ya Baraza la Wawakilishi chini ya wizara yake Mhe. Mama angu Asha Bakari kwenye kamati ndogo ile ya Baraza la Wawakilishi alimuuliza Mhe. Waziri kuhusu deni langu la milioni 71,000,000. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kwa sababu nina ushahidi nasikitika sana jibu alilojibu la moja kwa moja na napenda kumnukuu, alimjibu Bi. Asha na sote tuko kwenye kamati ya Baraza la Wawakilishi kwamba "hizi pesa watajuana na rafiki yake Balozi ndiye aliyempa pesa".

Mhe. Naibu Spika, shahidi wangu ndani ya kamati alikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Wete kaka angu Asaa huyu hapa. Shahidi wangu wa pili kwa neno lile alilolitoa alikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani-Pemba wote walikuwa mashahidi wangu. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, kama mtu mwenye busara mimi sikumpelekea hizi rafiki yangu, ningelifurahi angelisema umempa Makamu wa Pili wa Rais lakini umempa rafiki yako, Balozi. Yaani hata ile heshima kusema kwamba Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mheshimiwa nikitaka kufafanua tu kusema yale ndio yaliyokuwa majibu kwamba hayatambui.

Mhe. Naibu Spika, nimekuja na kitabu hiki ambacho ningelipenda niwasilishe baada ya kumpa waziri. Yeye kama Waziri, Katibu wake Mkuu na Naibu Katibu wake mkuu walikuwa wanatoa barua *official* kwa wadau mbali mbali kuchangia *Mapinduzi Cup*. Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wakisaini humu kwa niaba, kama sio *Mapinduzi Cup* nitaziwasilisha mbele yako.

Mhe. Naibu Spika, lakini isitoshe kama nilivyosema hii nchi ni yetu sote mimi nina uchungu na wenzangu wana uchungu, hizi sherehe za *Mapinduzi Cup* imo ndani ya sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na inatambulikana rasmi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa nashangaa leo kusema kwamba hajui, moja anasema *NGO, Mapinduzi Cup* ni *NGO*?

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hii nchi ni yetu sote na tunaipenda sote tulipofika wenzangu hawa wa *Mapinduzi Cup*, dada yangu huyu ambae ni Mwenyekiti wa Baraza la Michezo na Makamu Mwenyekiti wa *Mapinduzi Cup* waliandika barua kwa Makamu wa Pili wa Raisi kwa ajili ya sherehe za *Mapinduzi Cup* Balozi Seif Ali Iddi; hii hapa barua. Walimuandikia kuomba serikalini milioni 71,410,000 hii hapa, kwa bahati mbaya au nzuri siku hiyo na mimi nilikuwa nakabidhi nilikuwepo mimi, alikuwepo Makamu Mwenyekiti dada yangu Shery ambae vile vile ni Mwenyekiti wa Baraza la Michezo, alikuwepo Mhe. Turky Mbunge ambae ndiye anayechangia katika sherehe hizo; walipoomba serikalini katika hali ile ya kawaida kwa sababu hizi pesa zilikuwa zinahitajika kwa siku mbili zikalipwe kwenye mahoteli.

Sasa kwa bahati nzuri tulipotoka kwa uzalendo wangu, kwa kuwa serikali haikuwa na pesa kwa siku mbili zile, na makusanyo ambayo walioahidi wafanyabiashara na wananchi kuchangia sherehe za Mapinduzi za Miaka 50 haikuwa tayari. Mheshimiwa kwa uzalendo wangu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akasema Raza hili suala la *Mapinduzi Cup* na sherehe za Mapinduzi ni yetu sisi, mimi kama mtendaji mkuu ninachukua dhamana. Sasa kama nyie kina Shery Katibu Mkuu Dk. Mwinyikai mukiwa tayari na kama pesa hizi hamkupata mpaka kesho basi muendeeni Raza ofisini kwake mkachukue hizo pesa, mkazilipie hizo hoteli ambazo walitaka kuzifuta.

Mhe. Naibu Spika, yaani hizi pesa zinahitajika kama hazikupelekwa *that was on Thursday* kama hazikupelekwa *on Monday within three days* hoteli watazifuta.

Mhe. Naibu Spika, hii nchi ni yetu na mimi nina uzalendo na hizi sherehe zilikuwa ni kubwa za miaka 50, na ndio maana tukawa humu ndani Mhe. Naibu Spika. Sasa kwa bahati Mwenyekiti wa Baraza la Michezo ndie Makamu Mwenyekiti wa *Mapinduzi Cup* alikuja kiwandani akaniletea na hii barua akaniambia bwana hii barua nimekuja naomba hizi pesa.

Mhe. Naibu Spika, akanipakia kwenye gari yake tukenda benki tuka-*deposit* pesa hizo Mhe. Naibu Spika kwenye mfuko wao wa wizara hii hapa, ikiwa mfuko wao wa wizara au mfuko wa Kamati ya Baraza kwa kukusudia kwamba hizi pesa nilizotoa Mheshimiwa mimi si kopeshi. Lakini kwa uzalendo wangu nikaona kwamba sherehe ni zetu na serikali ni yetu na mimi nimefika hapa kwa sababu ya serikali na wananchi basi nitaziazimisha bila ya riba. Tuakakubaliana *rate* iliyokuwa ya dola siku ile tutakuja kulipana na *rate* hiyo hiyolicha ya kwamba kuna kupanda na kuteremka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kulipa zile pesa ilipomalizika sherehe mimi nikaandika barua ya kukumbushia deni langu ambalo ni sawa sawa na dola 45,626. Mhe. Naibu Spika, nilipokumbushia deni langu kwanza nataka nimsaidie kaka yangu Mhe. Waziri, mimi nina uhuru wa kuzungumza na vyombo vya habari wakati wowote, hata kesho naweza nikazungumza hawezi kunizuia. Kunizuia kwake sana asioneshe kwenye *ZBC* na gazeti lake, lakini hana uhuru wa kunizuia mimi nisizungumze, nitazungumza kwa wakati wowote alimradi taratibu na sheria nizifuate, na aliyekuwa hajaridhika aende Mahakamani.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, baada ya kadhia yote hii imeletwa barua na Tume ya ya RUSHWA, nikajieleze nikasema *inalilahi waina ilayhi rajiun*. Nimeletewa barua nikajieleze niliyetoa pesa! Tena nimeambiwa katika hiyo barua usiporipoti Mhe. Naibu Spika, hatari kubwa... naomba dakika moja niisome.

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Rushwa iliponiandikia hii barua wameniambia hivi; "Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumi Uchumi Zanzibar..." hii hapa, mwisho wameniambia "...fahamu kwamba unalazimika kutekeleza wito huu kama ulivyopangiwa na bila ya kukosa, kushindwa kwako kutekeleza wito huu ni kosa la jinai na hatua ya kimahakama inaweza kuchukuliwa". Mhe. Naibu Spika, mimi nilifika alfajiri pale nimeona nisije nikapanda sukari kwa kuchelewa kufika, maana yake serikali Mheshimiwa komando alisema "sheria, sheria, sheria". Kwa hivyo, ilibidi nifike mapema kwa kufuata sheria.

Mhe. Naibu Spika, walimpeleka mzungu vile vile sasa ninachotaka kumwambia Mhe. Waziri hizi pesa ni watu watatu tu; Katibu Mkuu, Dk. Mwinyikai ndiye mjumbe pesa hizo ndio waliozitumia, Shery Mwenyekiti wa Baraza la Michezo ndiye Makamu Mwenyekiti wa Baraza la *Mapinduzi Cup*, na Mwinyikai ndiye Mjumbe wa *Mapinduzi Cup* na Katibu wa Baraza la Michezo ndiye Katibu wa Mapinduzi Cup. Hawa Mheshimiwa ndio wanaojua hili sakata na wanafahamu kwa sababu hizi barua za serikali kuonesha hii ni ya *Mapinduzi Cup* ushahidi umo humu.

Sasa Mhe. Naibu Spika, isitoshe hayo kwa miaka mitatu ilipokuwa baada ya kumaliza *Mapinduzi Cup* akiwemo Mhe. Waziri mzee wangu, akiwemo Naibu Waziri, nikiwemo mimi sote tunakwenda kwa Rais kueleza hesabu zetu.

Mhe. Naibu Spika, hii hapa picha Ikulu na Mwenyekiti Shery yupo hapa, tunatoa maelezo hapa na waziri mwenyewe anahusika nitampa hiyo picha aiweke mimi sina haja nayo atakaa nayo nyumbani. Waziri mwenyewe alikuwa akienda..., Naibu Waziri alikuwepo sasa Mhe. Naibu Spika, nafikiri tusifike pahali hii nchi ni yetu kama kuna jambo tunataka kufanya watu wazunguke lakini wasifike pahala hili suala si la *NGO*, huyu anasema mimi sijui mahesabu umempa Balozi rafiki yako. Mheshimiwa mimi sijampa Balozi pesa zimekwenda kwenu. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Waziri *I have respect on you* nafikiri ungelikuwa mkweli, sasa mimi ninachoomba kwamba hii kamati imo ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, ninachomuomba Mhe. Waziri aje aniambie hizi pesa zangu lini nitapata, basi! Kama anasema ijapokuwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameshajitolea kwa niaba kulizungumza kwamba Raza amekopesha na ushahidi tunao na tutamlipa. Lakini ukweli haukuonekana ulionekana kwamba waziri aliposema nimempa rafiki yangu, mimi nimesikitika sana Mhe. Naibu Spika kusema kwenye kamati. Haya ndio matatizo tunayoyakataa kuingizwa viongozi wakuu kwa maneno ya kutupa tupa, hilo ni jambo kubwa sana.

Mimi nawaheshimu viongozi wote, namuheshimu Rais wa Zanzibar, namuheshimu Makamu wa Kwanza wa Rais ambaye ni mzee wangu, baba yangu na kiongozi wangu, namuheshimu Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lazima tuheshimu. Sasa kuna maneno ya kutupa tupa, halafu hii wizara yake inathibitisha kwenda kuomba fedha na inatiwa saini kwa niaba ya serikali, hii hapa mna barua humu.

Kwa hivyo, mimi nafikiri Mhe. Waziri kwa heshima na busara ningelikuomba ukija hapa unieleze hizi pesa utanilipa lini, kama una maneno mengine utakuja kusema. Mimi siungi mkono hii, siungi mkono kabisa wizara hii, tena nitatoa shilingi tutafika hapo tutakapofika lakini siungi mkono kabisa.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuhusu mradi wa *AGAPE* wa mamilioni; nilitaka Mhe. Waziri atakapokuja anielezee mradi huu umetumia kiasi gani na umefikia wapi? Je, mradi huu Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar waliridhia na kama kuna maandishi watuletee, inawezekana Baraza la Mapinduzi likajadili wakasema pelekeni kwa Makatibu Wakuu. Inaweza kuwa Baraza la Mapinduzi kwa sababu ya haraka wakasema basi pelekeni kwa Makatibu Wakuu je, ilipata ridhaa ya Makatibu Wakuu mradi huo?

Halafu vile vile Mheshimiwa tupate kujua matumizi yake na hali halisi ilivyo na tulipofikia, kwa sababu naona hili tatizo pesa hizi Mheshimiwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikuwa kwenye bajeti ya wizara. Lakini kwa uzalendo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya kiongozi shupavu, msikivu, mwenye hekima, busara Dkt. Ali Mohammed Shein Al-haj Rais wetu aliona kwamba kuna umuhimu ikabidi watoe pesa ya *AGAPE*. Kwa hivyo, nataka kujua hizi pesa za walipa kodi, kujua utaratibu mzima huu na ridhaa ya Makatibu Wakuu.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa bahati nzuri jadi yangu nimetokana na umasikini wazee wangu wakichunga punda, sasa nataka kumuomba Mhe. Waziri katika suala la utalii nataka kuanzisha mradi mimi na Mhe. Mgeni kwa sababu sisi ni watoto wa Kikwajuni; nianzishe mradi wa gari za punda kwa ajili ya watalii. Sasa hili kama halina urasimu mkubwa basi ninamuomba Mhe. Waziri kwa sababu huu mradi Mheshimiwa hata ukienda Bombay kule kuna farasi pale unapanda mwenyewe unazunguka. Kuna sehemu mbali mbali ukienda utakuta ndio utalii Mheshimiwa, sasa utamaduni wetu Zanzibar ni mzuri tunaweza kuanzisha huo mradi wa punda wa kitalii, watalii wakifika Forodhani pale tuna gari za punda tunawatembeza Mji Mkongwe.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache mimi nashukuru sana lakini naamini Mhe. Waziri ili tupite na hali hii tuliyokuwa nayo, naamini kwamba hekima zake, busara zake na usikivu wake kwa sababu Makamu wa Pili wa Rais ameshalitolea kauli suala hili, atalipatia ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha hii picha kama inawezekana ya kamati nzima wengine hawaonekani pamoja na hiki kitabu cha kabrasha zote za mahesabu ambacho kinaonesha pesa nilizokuwa nimezitoa na pesa hizi zilizokuwa zimekusudiwa hazikutumika katika shughuli hii. Hizo milioni 71,000,000 Mhe. Naibu Spika hazikutumika kama ilivyopaswa kutumika na alipokwenda Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tulikubaliana pesa hizi zitumike kwa hatua hii, haikufanyika sio tatizo langu; mimi sitaki kuingilia Kamati ya Mapinduzi, yaani pesa hizi zilitakiwa pale aliposhituka Mhe. Makamu wa Pili kwamba zisipopatikana pesa hizi hoteli zitafuta *bookings*. Kwa

hivyo, pesa hizi penye hoteli ya shilingi milioni tisa zimelipwa shilingi milioni nne, penye shilingi milioni tatu zimelipwa shilingi milioni moja wakati sio makusudio yake na kama walikuwa na matumizi mengine ilikuwa warejee kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais au kwangu kwa kupata idhini kwa sababu pesa hizi ni kwa masuala haya aliyoyaeleza Makamu wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana naomba hii kuiwasilisha, kama *book* picha inatosha basi.

Mhe. Naibu Spika: Tunaendelea na michango picha wape watendaji hapo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia kidogo hotuba hii ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kutuletea hotuba hii nzuri yenye malengo, mikakati ya kuleta maendeleo katika sekta ya habari, utamaduni na michezo kwa mwaka huu wa 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza na mchango wangu nikuombe kwa ruhusa yako kutoa mkono wa pole kwa familia ya Marehemu mchezaji maarufu, *captain* Ali Issa ambae ametutoka hivi karibuni, Mwenyezi Mungu amjaalie mahala pema peponi, *amin*. Mchejaji huyu ambae ndiye *captain* wa mwanzo kuchukua kombe la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa timu ya Zanzibar ambayo wakati ule ilikuwa timu ya KMKM mwaka 1984.

Baada ya utangulizi huo nianze na Sekta ya Habari. Sekta hii ni sekta muhimu ambayo ulimwenguni kote tunapata habari. Kwa hivyo, niseme kwamba niipongeze sana sekta hii habari katika kufanya mikakati mbali mbali, katika kutupa habari mbali mbali kwa kupitia letu hili la Utangazaji (*ZBC*).

Mhe. Naibu Spika, masikitiko yangu makubwa kwamba bado wafanyakazi au waandishi wa habari wamekuwa hawaangaliwi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutupa habari kwa maeneo mbali mbali ya televisheni, redio, na magazeti. Watangazaji wetu au wafanyakazi wetu wa *ZBC* wamekuwa wakirusha matangazo katika Baraza lako hili tukufu, na wamekuwa wakifanya kazi kubwa kuwapelekea wananchi kujua au kuona yale yanayotokea katika ukumbi wako huu wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, chumba cha kurushia matangazo ni chumba ambacho kimekuwa kinapigwa na baridi kubwa pale wanafanya kazi kuanzia asubuhi mpaka usiku, lakini cha kusikitisha zaidi hata pesa za maziwa hawapatiwi. Sasa mimi nimuombe Mhe. Waziri kuwaangalia kwa jicho la huruma wafanyakazi wetu hawa ili na wao wapate angalau pesa za maziwa ili kujiondolea maradhi mbali mbali.

Vile vile Mhe. Waziri wakati anazindua au anaipigia debe Kampuni ya Ving'amuzi ya *AGAPE* alitueleza mengi kwa sifa nyingi, kwamba kampuni hii ina vifaa bora, vya kisasa ambavyo Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla watakuwa wakipata taarifa mbali mbali na zilizo bora kupitia Kampuni hii ya *AGAPE*. Lakini cha kusikitisha ni kwamba hakuna ambacho tunakiona; kampuni hii haieleweki, haina mbele wala nyuma na zaidi kwamba kuna kampuni nyengine ambazo zimejitokeza katika kuwapa habari mbali mbali wananchi za ndani na nje, zimekuwa hazipewi ushirikiano ulio mzuri katika kuwapatia Wazanzibari na Watanzania taarifa na vipindi mbali mbali vilivyo bora.

Mhe. Naibu Spika, taarifa zilizopo kwamba hivi karibuni Kampuni ya Azam TV ambayo ilipeleka barua rasmi kupitia wizara yake imesikitishwa na majibu yaliyotoka; yalikuwa sio mazuri, hawakupewa ushirikiano. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze sababu gani Kampuni hii ya Azam TV wasiruhusiwe kuonesha vipindi vyao kwa kuwaletea Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla vipindi vilivyo bora na kupata habari mbali mbali za michezo na habari nyengine kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Sekta ya Utamaduni na Michezo. Sekta hii ambayo sasa hivi kuna Kamishna wa Michezo; huko nyuma kulikuwa na Mkurugenzi wa Michezo, lakini mfumo tulionao sasa Mkurugenzi wa Michezo alifutwa katika sekta hii ya utamaduni. Sasa mimi niombe kwa niaba ya wanamichezo katika kuendeleza michezo basi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kurejesha Mkurugenzi wa Michezo. Nina imani kwamba atapokuwa Mkurugenzi wa Michezo yupo basi anaweza kufanya kazi nzuri zaidi katika kuendeleza michezo Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, sekta ya michezo imekufa na sote ni mashahidi. Kwa hivyo, imani yangu kwamba kama kutakuwa na Mkurugenzi wa Michezo na wapo watu wenye uwezo, wenye vipaji, wenye elimu ya kuwa wakurugenzi na kuendeleza michezo yetu Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Baraza la Taifa la Michezo, BTMZ. Baraza hili ndicho chombo ambacho tunakitegemea katika kuendeleza michezo, lakini kwa kunukuu maneno ambayo Mhe. Waziri ametueleza hapa;

"Majukumu ya msingi ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar ni kusimamia maendeleo ya michezo yote iliyosajiliwa. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza hili limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuchangia upatikanaji wa vifaa vya michezo kwa vyama 10 vya michezo; na
ii. Kutoa mafunzo ya walimu na waamuzi wa michezo 10....", na mambo mengine.

Sasa la kusikitisha ni kwamba fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kazi ya BTMZ ni shilingi 90 milioni. Ukiangalia hapa kwa kweli fedha hizi ambazo zimetengwa katika kusaidia Baraza la Michezo nadhani mimi ni fedha kidogo na inastahiki Baraza hili kupewa fungu ambalo linatosheleza katika kusaidia vyama mbali mbali vya michezo.

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Michezo lina vyama takriban zaidi ya 30, sasa ukiangalia na ukipiga hesabu ni pesa kidogo sana ambazo Baraza la Michezo linapewa fungu hili katika ruzuku ya kuendeleza michezo. Vile vile utakuta kwamba kuna vilabu vyetu ambavyo vinashiriki katika mashindano ya kimataifa yakiwemo mashindano ya Afrika, vimekuwa vikipewa ruzuku ya shilingi 15 milioni.

Mhe. Naibu Spika, timu zote ni masikini, timu zetu hazina uwezo wa kuendesha mashindano yoyote. Sasa utakuta kwamba zinapewa ruzuku ya shilingi 15 milioni wakati gharama za timu moja kushiriki katika mashindano hayo kwa mechi moja ni zaidi ya shilingi 50 au 60 milioni. Mimi ningeiomba wizara na serikali kwa ujumla kuangalia kwa jicho la huruma katika bajeti inayokuja ya mwaka 2015/2016 kuwaongezea kutoka shilingi 15 milioni angalau kufika shilingi 25 milioni. Kwa sababu angalau tuweza kuvisaidia vilabu vyetu hivi katika kufanya vizuri kwenye mashindano mbali mbali.

Hata hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kwamba katika vilabu vyetu ambavyo vinashiriki katika mashindano vya mwaka huu basi atafute fungu lolote ili kuongezea angalau shilingi 20 milioni kutoka shilingi 15 milioni. Najua uwezo huo Mhe. Waziri anao ataangalia kwa jicho la huruma angalau kuwaombea kwa wafadhili mbali mbali kuvisaidia vilabu vyetu.

Mhe. Naibu Spika, katika Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*) huko nyuma tulikuwa tumezowea migogoro mbali mbali, malumbano, lakini nishukuru kwa juhudi ambazo anazichukua Mhe. Waziri angalau migogoro ile imepungua. Lakini kuna tatizo ambalo limejitokeza na hili Mheshimiwa haliwezi kumalizika bila ya Katiba ya *ZFA* kurekebishwa.

Hivi juzi kulitokea kesi ambazo Waheshimiwa wengi humu ndani tumepewa barua mbali mbali kuhusiana na kesi ya Timu ya Mwenge ya Pemba kwa kunyang'anywa *point* na kupewa Timu ya *Hard Rock.* Sasa nimezipitia taarifa hizi kwa kina kabisa tatizo linatokana na katiba yetu ya *ZFA*. Mimi nimpongeze sana Katibu Mkuu mstaafu wa *ZFA* Mzee wangu Zam, amefanya maamuzi ambayo ni sahihi, baadhi ya viongozi wetu ndio wanasababisha vilabu vyetu vinakufa. Kwa sababu vilabu hivi ni masikini hata wale ambao wanajitolea kusaidia wanavunjika moyo, wanavisaidia vilabu vyetu mwisho wa mwaka timu imepanda daraja imekwenda *premium league* inanyang'anywa *point* kwa masuala ya kizembe kabisa, na hawa viongozi wetu ndio wanaosababisha haya.

Mhe. Naibu Spika haya ukiyaangalia utaona kwamba kuna baadhi ya watendaji wanasababisha. Mimi niseme kwamba *ZFA* ni moja, leo utakuta kuna *ZFA* Unguja kuna *ZFA* Pemba. Kisheria Katibu Mkuu ndiye mtendaji sasa utakuta *document* hizi zinaonesha Katibu Msaidizi ndiye anayefanya kazi hizo, ndiye aliyefanya utumbo huu kusababisha timu ya Mwenge kunyang'anywa *point* na kukosa kucheza ligi kuu ya Zanzibar.

Sasa haya ni matatizo na haya yatamalizaka baada ya kufanyiwa marekebisho katiba. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba Katiba ya *ZFA* inabadilishwa ili kuondoa zile kasoro zilizomo ambazo zinaleta matatizo kwa chama chetu hiki cha Mpira wa Miguu.

Niwapongeze sana viongozi wa *ZFA* Taifa angalau kuondoa migogoro ile iliyopo na niwaombe washirikiane na Mhe. Waziri katika kuinua mpira wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho ambalo nataka nilizungumzie tumekuwa tukilalamika kuhusiana na kurejeshwa ligi ya Muungano. Mpira wetu umekufa baada ya kuvunjika kwa *league* ya Muungano na mimi nimesema kwamba baada ya kuvunjika kwa *league* ile na tukaanza *league* yetu hapa Zanzibar mpira wetu wa Zanzibar ndio chanzo cha kufa kwake. Kwa sababu ule msisimko ambao ulikuwepo pale, tulikuwa tunashirikiana timu zetu na kucheza *league* hii ya Muungano na timu kubwa kama vile Simba, Yanga na nyengine. Sasa kuirejesha *league* ya Muungano ni vigumu, haya yote lazima tuzingatie faida za Muungano.

Hivyo niwaombe sana tutahadhari katika kuvunja mambo mengine ambayo huwa yanatuletea tija. Pia nimuombe Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba angalau wanafanya bidii na juhudi kurejesha ile *league* ya Muungano. Kwa sababu nina imani itakaporudi *league* ile mpira wetu Zanzibar utarudi. Sasa nimuombe sana Mhe. Waziri kutafuta mfadhili angalau kurejesha ile *league* ya Muungano kwa timu tatu za Zanzibar au nne na nne za Tanzania Bara, ili kurejesha hadhi ya mpira wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu muda wangu umekwisha nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa wenzangu kuiunga mkono bajeti hii ili Mhe. Waziri apate fungu katika kuendeleza mambo mengi yakiwemo masuala ya michezo, utalii na habari.

Mwisho nimuombe kuwaangalia kwa jicho la huruma waandishi wa habari ambao ndio leo wananchi wanatuona huko kupitia kazi ya waandishi wa habari ambayo wanaifanya hapa ndani. Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Naibu spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Mhe. Naibu Spika, pia naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimpongeze Mwakilishi makini Mhe. Hassan Hamad Omar kwa kuisaidia na kuiimarisha timu yake ya Shaba ya Kojani mpaka ikapanda daraja. Kwa kweli Wajumbe wengi humu ni mashahidi kama timu hii ni makini, na ikiwa itapata msukumo inaweza ikatusaidia katika michezo ya kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, nataka nianze mchango wangu katika Ofisi Kuu Pemba. Ofisi Kuu Pemba kuna Kamati ya Uongozi ya Wizara ambayo inaundwa na Wakuu wa Idara, Pemba. Linalonisikitisha hapa ni kuwa wakuu wote wa Idara ni wanaume, hakuna hata mwanamke mmoja. Wanawake wenye elimu na uwezo wapo, lakini sijui kwa nini wanawake hao hawapewi nafasi. Naomba nipate maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri ni lini mfumo dume utakwisha ndani ya wizara yake, Pemba.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka niligusie ni ujenzi wa Jengo la Judo Pemba. Naomba niipongeze sana Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa hatua ya kukamilisha jengo lile zuri na la kisasa katika eneo la Chake Chake, Pemba. Ile ni hatua kubwa na ni imani yangu kwamba vijana wengi wa Pemba wameridhika na hali ile.

Mhe. Naibu Spika, hat hivyo kuna jambo moja ambalo namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi. Kuna wafanyabiashara wanaidai wizara, waliikopesha wakati wa kujenga jengo lile. Namuomba Mhe. Waziri anieleze wafanyabiashara hawa watalipwa lini.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni suala la matangazo ya *digital*. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli awamu ya sita *TV* Pemba ilikufa kabisa na wananchi wengi waliokuwa na *TV* zilikuwa ni kama mapambo katika nyumba zao. Nampongeza sana Mhe. Rais hivi sasa Pemba *TV* inaonekana, na si *channel* moja, ni kiasi *channel* 20. Hata hivyo kuna tatizo na namuomba Mhe. Waziri atwambie ni sababu gani ya kukatika katika matangazo. Ni lini wataweka mitambo isiyokatika?

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mara nyengine inasikitisha, matangazo tunaona na sehemu nyengine una hamu ya kuangalia kipindi, lakini mara unakuta *no signal*. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atwambie ni lini wataweka mitambo ya uhakika ili wananchi wapate kuona matangazo yale.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo naomba Mhe. Waziri anisikilize kwa makini ni eneo la ZBC. Kwanza nataka niwapongeze sana *ZBC* kwa kazi kubwa wanayoifanya, hata kama ipo nje ya maadili yetu. Nasema hivi kwa sababu hivi sasa pale *ZBC* wafanyakazi wanawake wananyanyaswa sana. Kuna walinzi pale wakifika wafanyakazi wanawake wanawaambia wavue mabaibui. Hii si desturi yetu, mfanyakazi ile ni ofisi yake na atafika katika sehemu yake ya kazi kwa nini umvue nguo nje, usimwachie akavue ndani?

Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe nimeshuhudia hivi karibuni kipindi cha mvua kuna mfanyakazi mmoja aliroa, akafika pale mlinzi akamlazimisha avue nguo. Akamwambia siwezi kuvua baibui hapa kwa sababu nimeroa na hali yangu hairuhusu. Mlinzi akamwambia lazima utavua baibui ndio uingie ndani. Mhe. Naibu Spika, huo ni udhalilishaji, mlinzi kakusudia nini? Mtu ameshamwambia siwezi kuvua nguo hapa nitaingia ndani nivue kwa ajili ya kujistiri. Anamwambia huingii ndani mpaka uvue baibui. Mhe. Naibu Spika, nimeshuhudia mfanyakazi yule analia machozi kama mtoto mdogo lakini bado mlinzi kang'ang'ania avue baibui.

Mhe. Naibu Spika, nilipoliulizia suala hili nikaambiwa hata wale wananchi wanaokwenda kupeleka matangazo ikiwa ni wanawake wanalazimishwa wavue baibui. Kwa kweli mimi nilishangaa sana si utamaduni wetu. Wazanzibari tuna tabia; mgeni tunamkaribisha ndani ndio tukamwambia avue nguo. Leo mgeni anafika mlangoni unamwambia avue nguo, wakati mwengine amekuja na shida mtoto wake pengine amepotea anakuja kupeleka matangazo analazimishwa avue baibui, hajulikani nguo aliyovaa pale kwa wahka aliokuwa nao. Kwa kweli hili ni tatizo. Itakapofika hadi mtu yule anaambiwa ikiwa hukutoka na nguo nzuri kwako tutakwenda kukuchukulia kanga za kusalia ndani, lakini lazima uvue baibui.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninavyoelewa *ZBC* ni chombo cha wananchi, na kwa kweli kuna msemo wa kiswahili usemao "akufukuzae hakwambii toka". Kumlazimisha mtu avue baibui ni kama unamfukuza hata akiwa na shida asilete tangazo lake pale. Namuomba Mhe. Waziri anieleze utaratibu huu umetokea wapi, au huu ndio utamaduni wetu Wazanzibari. Kwa sababu hii wizara ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Kwa hivyo, ikiwa huu ndio utamaduni wetu basi atueleze wageni badala ya kuvua viatu mlangoni, sasa wavue na mabaibui.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hapa eneo la *ZBC* ni kwa kile kipindi chao muhimu cha kumkejeli Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais. Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa sababu kile tulitegemea ni chombo chetu wananchi, si chombo cha uchochezi, si jukwaa la siasa. Lakini leo chombo kile kinatumiwa kumkejeli Makamu wa Kwanza wa Rais, na hivi sasa wamepunguza kwa sababu kuna bajeti.

Mhe. Naibu Spika, nina kumbukumbu kabla ya bajeti ya mwaka uliopita alikuwa akikatwa jina Makamu wa Kwanza wa Rais na alikuwa akiitwa hivi hivi. Lakini ilipokaribia bajeti suala lile liliondoka kwa sababu kunataka kupitishwa bajeti. Ilipomalizika ndio tayari kukaandaliwa kipindi hiki. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa suala hili. Kwa sababu hapa ni kuonesha kama kile chombo ameweza kukiongoza vibaya. Kwa kuwa yeye mwenyewe alikuwa na uwezo wa kukidhibiti chombo kile na kikaenda kule tunakokusudia.

Mhe. Naibu Spika, najua hakika kile kipindi kimepumzika kidogo kwa sababu kuna bajeti, lakini ikimalizika bajeti tayari masuala ya kumkejeli na matusi yataendelea pale *ZBC*. Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri atakaposimama anipe maelezo mazuri, kwa nini anaiachia *ZBC* ifanye hivi. Haoni kama huku ni kusababisha vurugu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naomba niseme kwamba siku zote tunajua kama sanaa ni kioo cha jamii. Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri azifanyie uhakiki hizi kazi za sanaa. Kwa sababu ile kukaa kwenye TV unaangalia sanaa zetu ukakuta mavazi yaliyovaliwa hayastahiki, kule si kuelimisha, ni kupotosha. Namuomba Mhe. Waziri alisimamie hili, tukitizama sanaa zetu tujue kama unaweza ukatizama na mtu yeyote kwa sababu ni njia moja ya mafunzo. Lakini isiwe nguo aliyovaa msanii pale inasikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, pia katika kitabu hiki nimeona Mhe. Waziri ameeleza malengo yao waliyonayo ni kuimarisha miundombinu iliyopo na kujenga njia ya kukimbilia katika Uwanja wa Gombani Pemba.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri, hii michezo ni mpira tu na mbio hakuna michezo mingine. Japo Ukumbi wa Judo tumeshauona lakini kuna na michezo ya kuogelea na michezo mingine. Sasa hebu atwambie ana mpango gani wa kuiimarisha hii michezo mingine angalau nayo tukaona inathaminiwa. Ingawa kuna mmoja ananiambia imo, lakini unajua tena ukichelewa ndio umeshachelewa.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru nitaunga mkono bajeti ikiwa nitapata majibu mazuri.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa dhati jioni hii kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Mhe. Naibu Spika, mimi nina mambo kama mawili tu ya kuchangia hotuba hii ya sahiba wangu Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, mwanzo kabisa nataka nichangie buku kubwa halafu nimalizie kwenye kitabu. Naomba anisaidie maelezo katika mapato ukurasa wa 22 fungu 0501, Sauti ya Tanzania Zanzibar. Tangu mwaka 2011/2012 ndio tumewekewa mapato yaliyokusanywa milioni 40,898,300/=. Idara ya Televisheni fungu 0901 sijaona mapato yaliyokusanywa. Sasa nilikuwa najiuliza basi hata yale matangazo ya vifo pia hayalipiwi, au yale matangazo yoyote tunayokuwa tunapeleka. Nashangaa kwamba hili fungu lina maziro matupu. Kama kuna eneo jengine ambalo wameliweka mimi sijaliona Mhe. Waziri akija atanisaidia.

Pia naomba nisaidiwe katika ukurasa wa 345 fungu 220400 Gharama za Petroli. Mhe. Naibu Spika, fungu dogo 220401 Gharama za Petroli mwaka jana lilitengewa milioni 28,800,000/=, mwaka huu milioni 43,200,000/=. *Diesel* 220402 mwaka jana ilikuwa milioni 14,400,000/=, mwaka huu milioni 25,000,000/=. Mhe. Waziri atakapokuja kujibu hoja anisaidie sababu za kupanda maradufu karibuni mara mbili, tatizo nini? Kama *diesel* imepanda bei na petroli, au kama wameongeza magari basi nielezwe.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 346 fungu 311100 mali isiyohamishika, ujenzi wa majengo. Mwaka jana katika ujenzi wa majengo mapya walitengewa milioni 80, na mwaka huu wameomba milioni 643,400,000/=. Nilitaka kujua tu hatua zilizofikiwa mwaka jana za milioni 80, na kupelekea mwaka huu kuomba moja kwa moja milioni 643,000,000/=.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoka katika buku kubwa, sasa niende katika kitabu na zaidi nizungumzie *ZBC*. Mhe. Naibu Spika, wenzangu wameipongeza *ZBC*, mimi nasikitika kwa kuwa siku niliyoitizama siijui kwa sababu sioni faida yake. Hata wanangu ukifungua *ZBC* wananuna, wanasema baba fungua *ITV*. Yaani mpaka watoto wadogo wameanza kutokana na haiba na televisheni yetu kwa sababu ya vipindi. Unajua kila kitu kina mvuto wake.

Mhe. Naibu Spika, zaidi nililokuwa nataka kulizungumzia ni mashirikiano madogo yaliyokuwepo *ZBC* pamoja na watendaji wa wizara. Lile ni shirika lakini linaonekana kwamba hatulipi fursa ya kufanya kazi zake na wizara imekuwa inawaingilia zaidi katika shughuli zao za kazi za kila siku. Nampa pole sana Mwenyekiti wa Bodi mama yangu Tatu Ali kwa namna anavyofanyakazi katika mazingira magumu, katika suala zima la muingiliano baina ya wizara na watendaji.

Nitakuja kuzungumza kwa kina zaidi baadhi ya matatizo ambayo yanaonekana katika muingiliano wa kazi baina ya shirika na wizara.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuingia zaidi huku chini mimi nilikuwa nataka nielezee athari inazopata shirika hili. Kwa sababu pahala popote ambapo hapaoneshi mafanikio kama nilivyosema, huwa hapaleti haiba, na pahala popote palipokuwa hapana manufaa mazuri, basi hasara inapatikana.

Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukipigia kelele sana katika maendeleo yaliyokuwa si mazuri kwa shirika letu la *ZBC* Televisheni, hata kimaslahi kwa wafanyakazi. Hali halisi ya kimafao kwa wafanyakazi pia inarejesha nyuma. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa najaribu kuandika dondoo ya wafanyakazi wetu hapa ambao walikuwa ni wafanyakazi mahiri, wenye mapenzi, na wenye kutuletea maendeleo na waliokuwa wakileta mvuto kwa shirika hili, lakini sasa hivi wafanyakazi hawa wameamua kutoweka na kukimbilia sehemu mbali mbali. Wamekimbilia katika zile televisheni ambazo hivi sasa wananchi wengi wanapenda kuziangalia.

Mhe. Naibu Spika, tulikuwa na kijana wetu anaitwa Ali Issa, pamoja na kwamba alikuwa hajapata ajira rasmi lakini alikuwa anafanyakazi pale, sasa hivi amekimbilia *Star TV*. Tulikuwa na ndugu yetu Rajab Abdalla, yeye amekimbilia *PBZ*. Tulikuwa na ndugu yetu Maryam Hassan sasa hivi yupo *TBC*. Tulikuwa na ndugu yetu Shinuna Said Bakari Jecha sasa hivi nae yupo *TBC*. Tulikuwa na ndugu yetu Hassan Suluhu Hassan sasa hivi yupo *Star TV*. Othman Maalim Mhariri nae ametoweka. Juma Dau amekimbilia Uhamiaji. *Engineer* Cistod Barito yeye amesingizia kwamba ana matatizo ya kiafya ili apate sababu ya msingi ya kupata haki zake ametoweka. Ndugu yetu Mussa Kheri amekataa kuajiriwa kwa mkataba sasa hivi yupo *AGAPE*. Haji Abdalla kaka yangu Abdillah Jihad Hassan kamchukua Wizara ya Mifugo na Uvuvi, bora aende akapige *camera* huko kwenye samaki.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hii ni athari ya kuwa na watu ambao tunawategemea kwamba shirika limewasomesha kwa gharama kubwa lakini hatimae watu hawa wameamua kutoweka kutokana na hali na ukwasi wa wizara hii. Kwa taarifa kwamba shirika hilo lilikuwa kubwa na lilifika katika hatua ya juu na waliambiwa watengeneze *scheme of service* ya mambo yao lakini hadi hivi sasa hakuna kinachoeleweka.

Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio kadhia ya *ZBC* natarajia baada ya miaka mitatu na hawa waliobakia kila mmoja atatafuta pahala aende na tufikie pahala shirika tulibinafsishe. Mimi nafikiri haja ya kuibinafsisha *ZBC* imefika sasa hivi. Nilikuwa nampongeza sana Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwa maamuzi magumu aliyoyachukua. Unajua unafikia pahala Serikali inaingiza pesa lakini mafanikio hayapo. Mhe. Mazrui alifanya maamuzi magumu kwa kubinafsisha Shirika la Magari kwa sababu tulianza kuona kitu tumekizoea, ilikuwa kazi yetu pale kulipa mishahara ya wafanyakazi lakini halifanyi kazi. Kwa hivyo, tunachokitoa kilikuwa kikubwa kuliko kile ambacho tunakitegemea. Sasa nafikiri itafikia pahala tutaona tuanze kubadilishana mawazo na kulibinafsisha hili shirika la *ZBC* kwa faida. Kwa sababu ndugu zetu wa *cable* wamefikia katika hatua nzuri tuwape hili eneo wafanye kazi.

Mhe. Naibu Spika, nilizungumza suala la kutokuwa na maelewano *ZBC*. Maelewano ya *ZBC* hivi sasa, limefikia pahala lile shirika linaendeshwa katika mambo ya makundi, sio baina ya shirika na wizara peke yake. Hasa wafanyakazi wenyewe kwa wenyewe pia kunakuwa na makundi ambayo hayaleti mustakabali mzuri katika taasisi yetu ile tunayoitegemea.

Mheshimiwa chuki hizi za makundi *ZBC* zinapelekea kupoteza wafanyakazi wetu ambao tunawategemea, wafanyakazi ambao wana sifa katika zile fani zinazowahusu. Matokeo yake mtu anahamishwa anapelekwa katika eneo jengine ambalo halihusiani na shughuli zake. Sio kama anapelekwa kwa sababu ya kawaida tu lakini anapelekwa kwa sababu ya chuki. Lakini lile eneo lililokuwepo mheshimiwa watendaji wakuu wa wizara hii wanajaribu pia kupotosha wananchi kwa ku-*quote* vifungu vya kisheria.

Mheshimiwa kuna mfanyakazi alihamishwa *ZBC*, sina haja ya kumtaja wenyewe wanamuelewa. Watendaji wa wizara katika kumuhamisha kwa chuki tu zisizokuwa za msingi, wakaamua mpaka ku-*quote* vifungu vya sheria ya utumishi Nam. 2 ya 2011 kwa kumuandikia barua mbali mbali kuondoka kwake hilo eneo.

Mheshimiwa hivi sasa watu ni waelewa, watu wanafahamu sheria na kila mtu anajua kinachoendelea. Aibu iliyopatikana baadae ninafikiri itakuwa Mhe. Waziri kama sikosei, kuona tatizo hili na akawaambia kama hapa munakwenda pahala ambapo hapastahiki. Wao wenyewe Mheshimiwa wakaona kwamba wametumia vifungu vya sheria kinyume na vinavyotafsiri na wakaamua wao wenyewe kuandika barua za kutaka yule mfanyakazi kurejeshwa tena. Hii ndio aibu. Maana yake mtu munamuondosha lakini yule mfanyakazi Mheshimiwa ana-*document* hapa ambazo zinazoonesha.

Baada ya kupewa barua ya kuhamishwa kwa kunukuu kifungu hicho nilichokieleza cha sheria Nam. 2 ya 2011 na kwa uelewa wa mfanyakazi akawaambia kama hapa tafsiri muliyotafsiri ipo tofauti na inavyotakiwa. Mimi mumenihamisha kimakosa, kwa makundi yenu na ubinafsi. Nikasema mimi bado sihami na ninataka muitafsiri vizuri sheria hii.

Baada ya kutafsiriwa wao wenyewe wameona kwamba wamefanya makosa na wizara ikaamua kumrejesha pale pale. Sasa hii ni aibu Mheshimiwa. Makundi hayatufikishi pahala Mheshimiwa na makundi hayajengi nchi hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa mimi nilisema sitaki nizungumze mengi sana. Swahiba wangu sina matatizo naye lakini ninamuomba sana Mhe. Waziri iangalie sana *ZBC* namna ya makundi yanavyobagua na kufikia pahala kile chombo kutaka kufikia katika hali ambayo iliyokuwa sio nzuri. Ninajua wewe ni miongoni mwa walioandika barua ya mfanyakazi huyu kurejeshwa, lakini ninasema kwamba tutafikia pahala tutakuwa tunazungumza lugha ambazo si nzuri, lugha ambazo hatuzipendi, lugha ambazo wakati mwengine zinakatisha tamaa. Maana wakati mwengine tutafika pahala tutasema tumechoka na watendaji wasiokuwa na uwezo au na watendaji waliokuwa wabinafsi. Sasa si lugha nzuri kuzungumza katika pahala kama hapa Mheshimiwa. Zaidi tunapenda kusema kutokana na *ages* zetu kuelekeza zaidi ili chombo chetu kipate kuimarika na kufanya vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, hayo ndio yaliyokuwa machache sana. Nilisema sitaki kuzungumza mengi lakini pia nimuombe Mhe. Waziri aangalie maslahi ya ndugu zetu wa *ZBC*, atafikia pahala atakuwa hana muandishi wa habari na kituo atakifunga.

Mhe. Spika, ninaunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana mheshimiwa. Sasa nafasi tutampa Mhe. Saleh Nassor Juma na kama muda utabaki Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na kuwepo hapa leo.

Pili nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi. Sasa niende katika hoja iliopo mbele yetu. Mhe. Naibu Spika, nianze na ukurasa wa 8 wa kitabu chetu hiki katika ibara ya 18 hapa ambapo tunazungumzia sekta ya michezo.

Mhe. Naibu Spika, niliposoma hiki kitabu nimeona maeneo ya kipaumbele. Nimeona maeneo ya vipaumbele katika suala zima la sekta ya michezo ambavyo vipaumbele hivi ni pamoja na kuimarisha miundo mbinu ya michezo katika kujenga *tantan* pale katika uwanja wa Gombani na kukamilisha sera ya michezo na kuviimarisha vilabu vya michezo.

Mhe. Naibu Spika, lazima tukubali kwamba michezo mbali na kusaidia kuwaweka vijana wetu katika afya nzuri, lakini kwa sasa michezo ni biahara. Tena michezo ni uchumi Mhe. Naibu Spika. Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, katika kasma ya michezo ulimwenguni, michezo tunaweza kusema ni biashara. Tena sio kwa mchezaji mmoja mmoja lakini hata kwa nchi anayotoka Mheshimiwa.

Nilipoangalia vipaumbele hapa inaonekana serikali yetu haipo *serious* katika hili. Mhe. Naibu Spika, kuna nchi za wenzetu, wameeka vipaumbele suala la michezo na wachezaji wanakuwa wachezaji wa kimataifa na wanasaidia sasa sio maisha tu lakini hata uchumi wa nchi zao. Tumuangalie mchezaji kama Didier Drogba. Yule mchezaji mbali ya kujipatia mapato lakini katika nchi yake anajenga taasisi ya afya na anaisaidia serikali katika kupeleka maendeleo nchi yake na kadhalika, sio yeye peke yake tu lakini na wengine kadhaa.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha kwamba eti sisi tukishaweka *tantan* pale ndio basi tushaimarisha michezo na kuleta sera hapa tukaipitisha. Katika kasma ya michezo Mhe. Naibu Spika, kimataifa, kuna michezo ambapo sisi hapa kuna mazingira hasa ya ku-*install* michezo hiyo. Kwa mfano, katika michezo ya *olympic* ya kuogelea inasikitisha kwamba sisi tuna bahari pana sana hii bahari ya *India Ocean*. Lakini vijana wetu wakienda kule wanashindwa na Rwanda ambao hawana hata bahari wao.Ni kwamba hatukujikita katika hili.

Michezo ya kuogelea hapa kama tungewatayarisha vijana wetu, tulikuwa nao zamani walikuwa wakifanya vizuri akina Fidel Ali hapa, alikuwa akifanya vizuri katika tasnia ya michezo ya kimataifa ya kuogelea. Lakini sasa vijana wale wanavunjika moyo kwa sababu hawaendelezwi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi ninadhani ili kuleta michezo katika nchi yetu na kuwaendeleza vijana wetu pamoja na taifa letu, lazima ijipange vizuri kwa kupeleka mitaala ya michezo katika skuli za *primaries* na *secondaries*. Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tukifanya *diploma in physical education* pale Nkrumah. Tulikuwa tukitoa wataalamu katika sekta hii hapa hapa nchini. Imefutwa ile *diploma in physical education* hayatolewi tena mafunzo yale.

Sasa mimi ninaomba Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wawanasihi wataalamu wetu wa *SUZA* watoe *first degree in physical education* kusudi kuweza kupata wataalamu wa kuendeleza michezo pamoja na kuboresha mitaala katika *primaries* na *scondaries* zetu.

Mhe. Naibu Spika, programu nyengine ambazo wenzetu wa nchi nyingi zikiwemo hata hapo Tanganyika, wameanzisha katika kuiendeleza michezo yao, na zimewasaidia programu hizi. Juzi juzi nilisema hapa ndani kwamba wenzetu Tanganyika wameanzisha programu kwa kushirikiana na kampuni ya watu binafsi tu, wameita *Airtel Raising Star*. *Airtel Raising Star* inapita vijijini huko, kampuni ile kwa kushirikiana na taasisi za michezo za kule, wameibua watoto wadogo wenye vipaji vya michezo na vikasaidia vipaji hivi kuwatoa hata wale watoto waliokuwa wako katika mazingira magumu., wakenda wakacheza kombe la dunia na wakashinda. *Airtel* tu, kampuni ya simu kwa kushirikiana na secta ya michezo. (*Maikofi*)

Mhe. Naibu Spika, leo hapa Mhe. Waziri tunazo kampuni kadhaa nyengine zimo humu humu ndani ya hili Bunge. Kuna *Hassan and Sons*, hapa ukiwaambia tuanzishe *Hassan and Sons Raising Star*, ninahakikisha Mhe. Naibu Spika, tungeweza kupata vipaji na sisi timu zetu zikawa nzuri. Ninahakikisha hapa Mhe. Naibu Spika, kama tungeanzisha *Bhaa Raising Star* tukamshirikisha kijana wetu Bhaa hapa na kampuni yake, nina hakika kwamba tungepata vipaji vingi. (*Makofi*)

Halikadhalika kuna makampuni makubwa sana, kama Azam Marine tungewaambia ndugu zetu wa *Azam Marine* tunataka tuibue vipaji tukaanzisha *Azam Marine Raising Star*, tungeweza kupata vipaji na kuwa na wana michezo wazuri. Lakini *we are not creative*! Mimi ninaamini tungewaambia hata *ZANTEL*, tunataka tuanzishe *ZANTEL Raising Star* tukapita vijijini huko, ninakuhakikishia tungekuwa na vipaji na tungeweza kufanya vizuri katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, katika hili mimi ninaishauri serikali jambo jema huigwa. Misifumbe macho katika kuiga mambo. Hebu waigeni ndugu zetu wa damu hapo Tanganyika kwa kuanzisha mambo kama haya, ili tuweze kuinua vipaji vya vijana wetu na hatimae kujiinua katika soka. Hapa vijana wanaweza; tumewahi kutoa wachezaji wazuri hapa katika nchi hii na wakatamba katika medali ya kimataifa. Hebu tuangalie watu kama Dua Said walivyofanya vizuri, hebu tuangalie vijana wetu akina wale Marehemu aliyekuwa *goalkeeper* yule Riffat Said, alikuwa ni *international goalkeeper*. Tumemzaa hapa hapa na wengi tu mbona! (*Makofi*)

Mimi ninadhani tunavyo vipaji katika nchi hii na vyengine mpaka sasa hivi vinafundisha Oman kule akina Abdul-Wakat Juma nao kule, wapo kule wengi tu. Wametoka hapa hapa Zanzibar na hatukuwafyatua kutoka Bara au kuwatengeneza kutoka Kenya, tumewazaa sisi hapa hapa Zanzibar. (*Makofi*)

Ikiwa munataka ushauri tupo wataalamu ambao tumebobea katika masuala haya. Tuambieni tuje tuwashauri musitufungie macho ijapokuwa tupo *back beacher* huku, njooni tu tutakuja kuwapa ushauri kabia kabisa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninadhani niende katika mambo ya sekta ya habari. Mhe. Naibu Spika, sekta ya habari nayo vile vile ni muhimu mno. Katika suala zima la kupashana habari baina ya mtu na mtu na baina ya serikali na raia zake. Hiki ni chombo muhimu sana. Anayeongoza chombo hiki anatakiwa awe makini sana katika kusimamia, sio akae ofisini tu.

Mhe. Naibu Spika, vyombo vya habari kama havikusimamiwa vyema katika nchi vinaweza vikasababisha tatizo sana. Yapo mambo mengi sana tumejifunza katika nchi kadhaa za karibu karibu yetu ambapo machafuko makubwa yamesababishwa na vyombo vya habari. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, katika hili nimnasihi Mhe. Waziri asiwaonee haya hawa watendaji wake. Tatizo lililosababishwa na redio *Interahamu* pale Rwanda, mpaka sasa wakajiweka katika historia mbaya hawakuwa makini katika kusimamia majukumu yao.

Mimi ninadhani ukiangalia *historical background* ya siasa za nchi hii, unapokuwa chombo cha habari cha nchi kikaanza kumtolea maneno mabaya kiongozi mkubwa, ni tatizo. Mimi sitaki kiongozi kama Maalim Seif ambaye ukiangalia hata zile takwimu za uchaguzi kuanzia mwaka 1995, 2005, utaona nguvu aliyonayo katika nchi hii. Ninataka kujitolea mfano tu mimi mwenyewe ambae ni mwanasiasa katika Jimbo la Wawi muangalie, yaani mimi

tu, kama redio itanisema vibaya, televisheni itanisema vibaya, magazeti yatanisema vibaya, wanaweza wakasababisha *chaos* katika jimbo la Wawi kule.

Cheche ya moto inaweza ikaanza padogo tu, halafu ikaendelea. Sasa ikiwa hukuwa makini wewe unamtolea maneno mtu kama Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa nchi aliyekuwa na wafuasi kadhaa. Nearly 49% ya Wazanzibari ni *supporters* wake, kwa takwimu hizi hizi za Tume ya Uchaguzi tu. Unaweza ukasababisha vurumai na pakaja kuzuka kivumbi hapa.

Waziri upo unatoa macho tu, Mkurugenzi huyu wa Habari umemchukulia hatua gani au mupo pamoja wewe? Utakapokuja uniambie hapa. Ikiwa mupo pamoja na Mkurugenzi wako wa Habari anayetaka kusababisha kama Rwanda vile, basi utawajibika wewe na Mkurugenzi wako. Hukuwajibika tutakuwajibisha sisi. Hili ninakwambia hapa ujue. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala zima la Shirika la Magazeti. Shirika la Magazeti Mhe. Naibu Spika, ni muhimu nalo. Lakini kabla ya hapo niendelee na wale jamaa wa *ZBC*. Hawa wana matatizo jamani pamoja na ubaya. Unajua wana ubaya lakini na vile vile tunatakiwa tuwatetee. Haya marekebisho ya mishahara hawa wafanyakazi wao hadi leo hii, ile nyongeza iliyotolewa na Rais hawajaingiziwa hawa hasa kule Pemba.

Waongezeeni sisi si vibaya kuwasemeya kwa sababu wanatupigia kura, tutawatetea tu humu. Waongezee Mhe. Waziri maslahi yao hawa *ZBC*. Hata wale wanaostaafu pale. Kuna mama mmoja maskini ya Mungu mwezi wa tatu amekwishakustaafu anaitwa Bibi Tatu Khamis anafanya kazi *TVZ* pale, hata pesa zake za likizo hadi leo hajapata. Hana mume yule mama mnyonge wa Mungu, na alikuwa akiitumikia serikali, jamani huo si uadui huo!

Ninataka akalipwe pesa zake za likizo na kesho nitampigia simu kama hajalipwa Bi. Tatu basi tutabanana katika kupitisha hivi vifungu hapa.

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Magazeti. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kama kuna nchi iliyokuwa na historia nzuri katika suala zima la vyombo vya magazeti basi ni hapa Zanzibar. Inasikitisha kwamba kabla ya mapinduzi sisi tulikuwa na magazeti 17. Baada ya mapinduzi tukawa na magazeti mawili. Lakini yote Mhe. Naibu Spika, magazeti haya yalikuwa yakichapishwa hapa hapa nchini. Hayakuwa yakivuka bahari, hata hapo Pemba. Tukiyachapisha makao makuu ya nchi ambapo ni hapa Unguja. (*Makofi*)

Inasikitisha sasa hivi tumebakiwa na gazeti moja kama ulimi. Mtu hana milimi miwili ana ulimi mmoja tu. Hilo pia halichapishwi hapa. Mpaka liende Tanganyika. Munaweza mukaweza ati kwa sababu siku hizo za ukoloni walikuwa ni wakoloni wakisimamia wenyewe, *no* ilikuwa ni sisi wenyewe. Mhariri wa gazeti la..., hebu ngoja niangalie kidogo, Mhariri wa Afrika Kwetu alikuwa ni Mzanzibari halisi na aliyekuwa Meya wa jiji la Zanzibar Mhe. Mtoro Rehani Kingo, mzaliwa wa hapa hapa. Dogo hilo. (*Makofi*)

Wajumbe: Kubwa. (*Kicheko/Makofi*)

Mhe. Saleh Nassor Juma: ...na alikuwa hana elimu kama nyinyi, aah! Na alimudu kulihariri gazeti hapa. (*Makofi*)

Inasikitisha sana. Nchi ya mwanzo kihistoria kumiliki gazeti la serikali lake mwenyewe ni Zanzibar. *Since* 1892 tulikuwa na gazeti letu la serikali hapa, lilikuwa linaitwa *The gazzette of Zanzibar of East Africa*. Mhariri wake alikuwa ni Maalim Khalili Mzanzibari. (*Makofi*)

Leo kigazeti kutoka 1800 *up to date*, tunashindwa yaani tumerudi nyuma kiasi hiki jamani! Maana yake hawa vijana wadogo wadogo hawajui historia akina mjukuu wangu Mhe. Wanu Hafidh Ameir pale, Mhe. Viwe Khamis Abdalla walikuwa hawajui lakini niwatajie.

Magazeti tuliyokuwa nayo siku za nyuma; Africa Kwetu ni gazeti mwanzo ambalo lilikuwa mhariri wake ni Mzee Mtoro Rehani Kingo, kulikuwa na gazeti la Kipanga, Kibanda, Sauti ya Afro Shirazi, Jogoo lilikuwa likiitwa Adal el Safu; hili lilikuwa la Hizbul-Watani, Maalim Maisara ndiye aliyekuwa Mhariri. Kulikuwa na gazeti la Agozi, lilikuwa Mhariri wake ni muasisi wa Afro Shirazi, Bwana Jamal Ramadhan Nasib marehemu, unaona kulikuwa na Muongozo. Kulikuwa na Zanzibar Boys, kulikuwa na *Summer Charry*; hili lilikuwa ni la Kiingereza, lilikuwa na

Kiingereza na Kibrahania. Unaona hili lilikuwa likichapishwa hapo Minara Miwili. Musije mukafikiria likichapishwa India, aah! (*Makofi*)

Sasa sisi tumerudi nyuma mpaka kigazeti kimoja tunashindwa kukichapisha hapa. Utakapokuja Mhe. Waziri ninataka unipe maelezo kina pamoja na mashine mpya ambapo pesa za walipa kodi tumesema zimetumika kujenga kile kiwanda, ni kwa nini munashindwa ku-*install* mitambo mikubwa na ya kisasa ya kuweza kuchapisha hicho kigazeti kimoja cha Zanzibar Leo. Utakapokuja uniambie hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa niendelee niache kwenye Shirika la Magazeti sasa nije katika sekta ya mambo ya utamaduni ukurasa wa 51 mpaka 91. Kama wenzetu wanasema sanaa ni kioo, wataalamu tunasema hivyo hivyo ambapo jamii huitumia na baadae kujirekebisha. Kama sanaa utaitumia vizuri basi taifa litakuwa na mwelekeo mzuri. Lakini sanaa unapoitumia vibaya Mheshimiwa basi taifa letu litakuwa litapoteza utamaduni na tutapoteza mila na silka zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa katika miaka ya sitini pale Pemba kulikuwa na bendi moja ikiitwa bendi ya Binti Kibakora Chake-Chake. Bendi hiyo ilikuwa ikitumbuiza katika jiji la Chake Chake na vitongoji vyake. (*Makofi*)

Ulikuwa unaweza kuja wewe na mkeo mukacheza, na watoto wenu mukacheza pamoja, kwa sababu kila mmoja amevalia vizuri tu. Munaburudika hapo tu halafu munarudi. Hiyo ilikuwa miaka ya sitini. hata hapa kulikuwa na mambo haya ya taarabu, tulikuwa na miaka ya 60 na 50 huko mwishoni, tulikuwa na mama yetu Siti Binti Saad.

Huyu Siti Binti Saad alikuwa akitoa burudani katika maeneo kadhaa. Lakini ilikuwa yeye anatuburudisha huku kajifunika uso kwa kutokana na heshima. Wengine wakasema kwa sababu ya sura mbaya; sio kwa sababu ya sura mbaya alikuwa ni mzuri sana yule mama. Pia alikuwa akilinda mila, silka na utamaduni wa Kizanzibari. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, sura aliyokuwa nayo ilikuwa ni nzuri na inavutia lakini alikuwa akijifunika, mpaka wakajaribu ati kumwambia kwamba alikuwa hana sura nzuri, kama si sauti angelikula nini. Aah! si kweli. Sauti yake ilikuwa nzuri na sura yake ilikuwa nzuri vile vile, picha zake mukizihitaji munaweza mukazipata kwa Mhe. Mohammed Haji Khalid ambae yeye alikuwa akifuatilia sana habari hii ya taarabu. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nimelazimika kusema hivyo kutokana na jinsi, mila na silka za nchi hii zinavyopotoshwa. Watu wanadengua wakiwa nusu uchi. Lengo letu sisi ni kuufikisha ziro ukimwi, maambukizi yawe ziro, tusifike ziro tatu. Leo wamekuja watu, wanaume utakuta wamevaa vizuri lakini wanawake mwanangu aah! Haifai kusimulia katika chombo kikubwa kama hiki. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wewe upo unaziona televisheni zinaonesha mambo yale, minenguo ile na TV unaona, tena TV zetu *ZBC*. Ni tatizo. Munaitia aibu *ZBC* kwa sababu ninataka muone nyinyi vijana wadogo wadogo, si vijana ni waheshimiwa mulio na umri mdogo. Ninataka muone kwamba katika nchi hii iliyojijengea historia kwa nchi hizi za Afrika na hata hizi zilizopo katika Kusini mwa jangwa la Sahara ni Zanzibar kuwa ni wamiliki wa mwanzo wa TV ya rangi.

Ilikuwa ukifungua mpaka mvunguni, ukiitia kwenye mabonde huko Vitongoji Umangani, chini ya vitanda ulikuwa unaona. Lakini sasa hata ukiiweka kwenye mnara kule Kigomasha wapi, huoni *ZBC- TV*. Sasa munapotosha mila na silka za Wazanzibari. Naomba wawe *assessed* wanaounda vikundi, muwa-*assess* ili wasituharibie utamaduni wetu.

Mhe. Naibu Spika, mwisho ni maslahi ya wasanii. Mhe. Naibu Spika, wasanii wetu wanapata shida sana pale wanapokuwa hawajiwezi tena kufanya sanaa zao. Tena ninakwambia katika uzima wao na umri wao huwa wanatuburudisha vizuri, kwa sababu ninadhani hapana asiyejua hapa jinsi ya Marehemu Bibi Kidude alivyokuwa akistarehesha.

Maskini kafa katika mazingira magumu sana ya kimaisha. Sasa hivi kuna kijana mmoja anaitwa Halikuniki. Yeye hata kama hajaigiza, wewe utacheka tu! Sikwambii akiigiza! Unaweza ukapitwa mpaka na haja ndogo. (*Kicheko/Makofi*).

Watu kama wale tutawaenzi vipi jamani mtu kama Halikuniki, mtu kama Bi. Tele, wapo vijana wengi tu wanafanya vizuri. Sasa haya maslahi ya wasanii munayaweka wapi. Naomba mimi muangalie maslahi ya wasanii ili watakapostaafu wasihangaike. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Nitaiunga mkoni hii hoja pale atakaponieleza kuhusu *ZBC* kile kipindi chao amechukua hatua gani mpaka wakamsema vibaya Maalim Seai Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Raisi wa Zanzibar na ikiwa hukuchukua hatua utawajibika. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wajumbe ninawashukuru kwa ushirikiano wetu mulionipa kwa jioni hii. Wizara hii Waheshimiwa mumehamasika, nina wachangiaji 20, wameshachangia Waheshimiwa 6. Kwa hivyo kesho tukijaaliwa tuje mapema tuweze kuendelea.

Ninaakhirisha kikao chetu hadi kesho tarehe 18/06/2014, saa tatu za asububu.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 18/06/2014 saa 3:00 asubuhi)